

8

**UTENZI^{WA}
VITA VYA
UHURU**

UMETUNGWA NA

**SHAABAN
ROBERT**

7

Utenzi wa Vita vya Uhuru

1939 hata 1945

Umetungwa na

Shaaban Robert

Nairobi

OXFORD UNIVERSITY PRESS

London New York

1967

Oxford University Press, Ely House, London W.1

GLASGOW NEW YORK TORONTO MELBOURNE WELLINGTON
CAPE TOWN SALISBURY IBADAN NAIROBI LUSAKA ADDIS ABABA
BOMBAY CALCUTTA MADRAS KARACHI LAHORE DACCA
KUALA LUMPUR HONG KONG TOKYO

© *Oxford University Press 1967*

Printed by Kenya Litho Ltd., P.O. Box 775, Nairobi

Published by Oxford University Press

P.O. Box 12532, Nairobi

KWA

BWANA A. A. M. ISHERWOOD

C.M.G., O.B.E., M.A.

MKUU WA IDARA YA ELIMU

TANGANYIKA TERRITORY

JINA HILI KATIKA KITABU HIKI

NI ALAMA YA HESHIMA

KWA UZURI WA TABIA NA WEMA WAKE

LIMEANDIKWA NA MTUMISHI

WAKE MNYENYEKEVU

UTANGULIZI

Hiki ni kitabu cha mashairi kilichoandikwa na mwenyeji wa nchi ya Tanganyika kwa lugha ya Kiswahili.

Kwa desturi mashairi hutaka usahihi wa maendelezo kama maandishi ya wazi; isipokuwa kwa sababu mbili zilizo muhimu. Sababu ya kwanza mashairi ana ruhusa kufupisha neno refu iwapo hapana neno jingine lenye tamko jepesi na maana anayokusudia katika kazi yake. Mafupisho hutokea mwanzo au kati ya neno. Pili ana ruhusa kuongeza au kupunguza endelezo la neno fulani hata kulibadili kwa ajili ya kutengeneza kina au mlingano wa sauti. Maongezo na mgeuzo hutokea mwishoni mwa maneno. Mabadilisho yoyote ya maendelezo ni ruhusa tu ikiwa maneno mengine yafaayo hayapatikani kabisa. Bora ni kuzuia mabadilisho kama iwezekanavyo katika mashairi yasimuliayo habari za historia.

Wakati nilipokuwa nikitunga mashairi ya kitabu hiki nilifanya desturi kupeleka nakili mara kwa mara kwa Bwana A. A. M. Isherwood, C.M.G., O.B.E., M.A., Mkuu wa Idara ya Elimu, Tanganyika Territory. Barua za kushangilia nilizopata kutoka kwa mtu huyu wa heshima ndizo zilionipa moyo mkuu wa kuendelea na kazi hii. Kwa hivi sina budi kumshukuru bwana huyu kuwa ndiyo nyota iliyoniongoza kizani hata katika mwanga huu. Bwana wa pili wa heshima ninayemshukuru ni Padre W. W. Jones (sasa Askofu) aliyekuwa Bwana Mwalimu wa Skuli ya Arusha, Tanganyika Territory. Bwana huyu aliniashiria kuwa sikufanya kazi ya bure kwa kuandika mashairi mafupi. Kadhalika nimefadhiliwa sana na Mtengenezaji wa *Mambo Leo* kwa kupigisha chapa baadhi ya mashairi yaliyo humu katika gazeti lake mara kwa mara. Fumba Salim, Mwalimu wa Skuli ya Serikali, Pangani, na ndugu yangu Mwidau Ulenge walikuwa wakisoma maandishi yangu ili niweze kulinganisha vina. Mabwana hawa nawashukuru pia.

Sasa naweka kitabu hiki mbele ya watu kwa matumaini kuwa wapo wengine ambao kitawafurahisha kama wale waliotangulia kusoma habari zake kwanza.

Shaaban Robert

1

Amina nipe wino,
Natamani tunga ngano,
Nieleze kwa mifano,
Vita vilivyotokea.

2

Nipe na karatasi,
Hima nataka upesi,
Nawe uje ujilisi,
Nisije nikasinzia.

3

Tena nataka kalamu,
Vita vitatu fahamu,
Hivi vikisha timu,
Niombee na dua.

4

Dua yako naitaka,
Kabla ya kuandika,
Ama nitasumbuka,
Katika kuhadithia.

5

Kisha uwe karibu,
Ukitazame kitabu,
Asaa nikiharibu,
Upate kuniongoa.

6

Usichelee muhali,
Nataka useme kweli,
Maana watu wawili,
Shida kupotea njia.

7

Wajua nimekukiri,
Awali hata aheri,
Usinihini shauri,
Ambalo laelekea.

8

Niwie radhi huduma,
Zote ninazokutuma,
Jambo hili la heshima,
Vibaya likipotea.

9

Hayo ukisha niridhi,
Tamwomba Mungu radhi,
Azidi kutuhifadhi,
Atuokoe na baa.

10

Kisa cha kuwa vitani,
Waingereza na Jermani,
Nakitia kitabuni,
Kisije kikapotea.

11

Nakitia kitabuni,
Kisikae ufichoni,
Wasome wana chuoni,
Wote wapate elewa.

12

Kisa hiki maarufu,
Nataka kukisharifu,
Kiwe mahali nadhifu,
Wasome wajao nyuma.

13

Nataka shairi hili,
Nilitunge Kiswahili,
Pasiwe na mushkeli,
Kutamka na kujua.

14

Nitunge kwa mashairi,
Minne minne mistari,
Niwaeleze habari,
Islamu na Masihiya.

15

Basi sasa nabaini,
Jamii sikilizeni,
Niwaanzie mwanzoni,
Mambo yalivyotokea.

16

Taeleza kwa utenzi,
Unyooke kama uzi,
Wasome wote wapenzi,
Watoto tunaozaa.

17

Asili ya machafuko,
Ni Slovakia na Cheko,
Hayo ndiyo mapasuko,
Ya amani ya dunia.

18

Kwanza mtanisamehe,
Niwatajie tarehe,
Wasisahau mashehe,
Watu wanaosikia.

19

Mwaka wa elfu moja,
Na tisa mia pamoja,
Thelathini ikija,
Nane ikazidia.

20

Tarehe hiyo sikia,
Ndipo yalipotokea,
Matata hayo Ulaya,
Kwa bahati yakavia.

21

Waziri Chamberlain,
Maarufu wa amani,
Akafika Berlin,
Kusuluhisha udhia.

22

Bwana huyu kwa siasa,
Mambo akayatakasa,
Na kila lililopasa,
Alitenda hakutua.

23

Ili kufanyiza dia,
Hilter akaridhiwa,
Atakalo akapewa,
Bali haikuwa dawa.

24

Ingawa aliahidi,
Katika yake fuadi,
Kupunguza uhasidi,
Tamaa ilimjaa.

25

Elfu na mia tisa,
Na thelathini na tisa,
Ilianza vita hasa,
Watu wakashuhudia.

26

Waingereza na Wafaransa,
Wasihimili mkasa,
Wakasema "Sisi sasa,
Vitani tutaingia."

27

Warussia walichelewa,
Hasa walighilibiwa,
Hata wakaja tambua,
Mambo yamewakulia.

28

Wajermani walikwenda,
Kufuata nchi kindi,
Jina lake ninapenda,
Nanyi kuwahadithia.

29

Jina yaitwa Polandi,
Hali vita haipendi,
Ikarukiwa na kundi,
Pasipo kuhurumiwa.

30

Kijeshi chake kidogo,
Kilipata nyingi togo,
Hakikuwapa kisogo,
Adui kumkimbia.

31

Hawakurudi hatua,
Nchi yao kutetea,
Ila mtu kuuawa,
Hapo alipozuia.

32

Poland ilijilinda,
Karibu ingalishinda,
Msaada haukwenda,
Mara ikadidimia.

33

Ndipo wakaja Wafini,
Taifa dogo na duni,
Likatiwa mtihani,
Uliotoka Russia.

34

Waingereza walitaka,
Msaada kupeleka,
Lakini haukufika,
Hawakupata njia.

35

Basi moto uliwaka,
Mwingi usiozimika,
Cheche yake ikaruka,
Norway ikaingia.

36

Huko Norway sikiza,
Walishika Waingereza,
Vita wakenda vikaza,
Wanyonge kuwaokoa.

37

Vita vikawa vikali,
Pasipo kwenda mahali,
Zote pande mbili,
Watu walizuia.

38

Mara ikaja habari,
Kuwaita askari,
Wale walio jusuri,
Pamoja na mabaharia.

39

Waliitwa Uingereza,
Ilipasa kusikiza,
Ingawa waliwaviza,
Adui waliojia.

40

Waingereza walitoka,
Ingawa hawakuchoka,
Nchi ikawa mateka
Adui akaachiwa.

41

Denmark na Sweden,
Msaada walihini,
Wakamwacha Jermani,
Wenzao kuwarukia.

42

Yakatambaa matata,
Holland yakenda kita,
Vikapiganwa vita,
Vya ajabu sikia.

43

Walikuja parachuti,
Wakashuka katikati,
Wakauana umati,
Kuzidi siku pia.

44

Vita vikashikana,
Wadachi wakabana,
Nafasi kukosekana,
Ya kutoka Malkia.

45

Waingereza kwa juhudi,
Nyuma hawakurudi,
Sana wakajitahidi,
Kumpata Malkia.

46

Hili walipotimiza,
Wakakiepuka kiza,
Mioyo wakawakuza,
Wale waliodhulumiwa.

47

Yakazidi mauaji,
Kama mfano wa maji,
Yakafika Belgiji,
Shujaa wakazuia.

48

Wakapigana kwa ari,
Maadui na Wahuri,
Beligiji akakiri,
Adui kuangukia.

49

Waingereza pale pote,
Wakawa katika pete,
Wangalikamatwa wote,
Lakini walizuia.

50

Zilikuja manowari,
Kuchukua askari,
Na wanahewa hodari,
Watu wakaokolewa.

51

Adui kafadhaika,
Kwa kuwakosa mateka,
Uingereza wakafika,
Jamii ya mashujaa.

52

Wadachi wakenda saga,
Watu wa Luxembourg,
Damu yao wakamwaga,
Nchi wakaichukua.

53

Adui kaepa ngome,
Zilizo na wanaume,
Akatokea, kinyume,
Ufaransa kaingia.

54

Basi akaja kwa kasi,
Kuelekea Paris,
Ili kutoa kisasi,
Kile walichotendewa.

55

Kisasi ninawambia,
Cha elfu tisa mia,
Na kumi na nne sikia,
Wadachi waliposhindwa.

56

Wakasema Wafaransa,
"Vita ni hivi sasa,
Na tuuawe kabisa,
Shime kuzuia njia."

57

Wakaipiga mizinga,
Mizito kuliko nanga,
Yenye nguvu ya kugonga,
Mafaru kuyazuia.

58

Wakazidi kuwakinga,
Njia wakazifunga,
Kila mtu akakinga,
Nchi kuipigania.

59

Askari maarufu,
Wakazipiga sufufu,
Risasi elfu elfu,
Adui kuwamwagia.

60

Huu usiwe uganga,
Njia hazikufunga,
Maana katika anga,
Kulichafuka ajaa.

61

Hawakuchoka kupigana,
Lakini hila hapana,
Marefu hata mapana,
Mafaru yalienea.

62

Wakasema Marafiki,
"Mafaru hayapigiki,
Chuma chake kina maki,
Ambacho yameundiwa."

63

Sasa ikazidi kazi,
Bila kupana pumzi,
Kama nyoka mtambazi,
Mafaru yakasogea.

64

Waitalia kubaini,
Wafaransa taabani,
Na wao wakatamani,
Vita kuwatangazia.

65

Wakalipiga kwa nyuma,
Jeraha la uhasama,
Wafaransa wakasema,
"Inshala tutalipiwa."

66

"Lazima Waingereza,
Kisasi watalipiza,
Vita havitatuza,
Mpaka tuwe huria."

67

Watu wakaona shani,
Waitalia kuhuni,
Na kutaka upigani,
Hasara kuiwania.

68

Tamaa yao ya pato,
Ikageuka majuto,
Ukawawakia moto,
Wa Waingereza sikia.

69

Turudi nyuma kabisa,
Kule kwa Wafaransa,
Tukavitazame visa,
Tujumlishe pamoja.

70

Wafaransa walitangaza,
Kuwambia Waingereza,
"Vita hatutaviweza,
Twahitaji kujitoea."

71

"Si kama twawakimbia,
Lakini hapana njia,
Na nyinyi mwashuhudia,
Hali yetu mwaijua."

72

"Twaona kujizuzua,
Si jambo lenye murua,
Na haya ni majaliwa,
Yamekwisha kutimia."

73

"Tkiwa mmehiari,
Twataka kwenu shauri,
Tuokoe askari,
Hawa waliosalia."

74

Hili wakaamuriwa,
Na ahadi wakapewa,
Kuwa watatetewa,
Hata wawe wahuria.

75

Wale waliokiri,
Ni shujaa mashuhuri,
Katika uaskari,
Dunia nzima yajua.

76

Baadhi ya wenye ari,
Ya kutetea uhuri,
Wakachagua shari,
Kuliko kujitolea.

77

Nia zao walikaza,
Wakenda Uingereza,
Jeshi wakalifanyiza,
Jina lake Wahuria.

78

Mmoja wa maamiri,
Ambaye hakuhiari,
Kuuachia uhuri,
Jina lake tawambia.

79

Jina lake De Gaulli,
Shujaa hana muhali,
Maarufu hata mbali,
Watu wote wamjua.

80

Jermani kajigamba,
"Nimekwisha vunja mwamba,
Nchi zote tazikumba,
Nitakalo litakuwa."

81

Turudi nyuma tuseme,
Tuzuie yasizame,
Tukaishia magome,
Kiini kikapotea.

82

Kuondoka kwake kitini,
Waziri Chamberlain,
Akaja Winston,
Vita akaviandaa.

83

Jina lake maarufu,
Vizuri niwaarifu,
Huyo si mtu wa hofu,
Churchill mwasikia.

84

Hotuba yake ya kwanza,
Kuwambia Waingereza,
Heri nikuieleza,
Mjue ilivyokuwa.

85

Hotuba ilifanya maki,
Mioyoni mwa halaiki,
Ikawa haifutiki,
Kwa watu waliosikia.

86

“Nataka tuwe washindi,
Katika kila upande,
Dola yetu tuilinde,”
Churchill kawambia.

87

“Tunapigania haki,
Kuokoa halaiki,
Mungu atatubariki,
Inshala hatutavia.”

88

“Shime shikeni bunduki,
Moyo msitaharuki,
Na Mwamuzi wa haki,
Atatuongoza njia.”

89

“Itamiminika damu,
Hili limelazimu,
Bali mwisho ukitimu,
Ushinde tutachukua.”

90

“Tutapigana hewani,
Tutapigana baharini,
Tutapigana barani,
Kabisa hatutaachia.”

91

Kawambia maamiri,
Na jamii askari,
“Hii ndiyo saa nzuri,
Kufanya historia.”

92

Kisha akawasalimu,
Kwa maneno ya muhimu,
Akaipeleka simu,
Amerika sikia.

93

“Silaha hima twataka,
Kwetu zikisha fika,
Vita tutavishika,
Hata mwisho kuujua.”

94

Kiliudhi kisa hiki,
Wadachi wakahamaki,
Wakenda Atlantiki,
Vyombo kuvizua.

95

Basi akenda jiwamba,
Peke yake sasa simba,
Mungu akamwomba,
Adui kuwazua.

96

Jermani alidhani,
Mwingereza hapigani,
Ila afanya utani,
Wenziwe kuwachochea.

97

Hapo wakajishaua,
Kukutanisha mashua,
Za kutaka kuvukia,
London kushambulia.

98

Mashua kulipokucha,
Zikawa kama pakacha,
Zilipigwa kutwa kucha,
Hata zikafumuliwa.

99

Eropleni makundi,
Zilikwenda England,
Zikaonyeshwa ufundi,
Nyingi zikatungulia.

100

Kisiwa cha Waingereza,
Vizuri ni kueleza,
Nyinyi mnaosikiza,
Wote mpate kujua.

101

Kiko kati ya bahari,
Tena kina manowari,
Zimejiweka tayari,
Adui kumpokea.

102

Ukitaka kwenda huko,
Sharti upate kivuko,
Na hayo sasa hayako,
Adui akalemewa.

103

Kila njia ya kuvuka,
Wadachi ikawatoka,
Ndipo wakazunguka,
Pengine kuparukia.

104

Sasa nitarudi nyuma,
Nipate eleza vyema,
Watu wanaosoma,
Wazidi kuzingatia.

105

Turudi kwa Taliani,
Alipokuja vitani,
Akadhani Wayunani,
Aweza kuwavamia.

106

Vita vikaja kusaki,
Nchi ya Magiriki,
Ingawa hawavitaki,
Lazima kujitetea.

107

Magiriki walizua,
Maadui wakaua,
Wengine wakakimbia,
Upande wa Albania.

108

Waitalia walijua,
Watakayo shida kuwa,
Bali walijizuzua,
Kutamani ushujaa.

109

Kadiri ya miezi sita,
Walipigana vita,
Jermani akaleta,
Msaada Italia.

110

Muda wa siku kidogo,
Taifa hili dogo,
Likaonyeshwa mapigo,
Ajabu kuhadithia.

111

Adui alipozidi,
Ikawa hapana budi,
Magiriki wakarudi,
Kusonga wakaachia.

112

Vita vikenda Kreti,
Kikafanywa kizingiti,
Wakashika madhubuti,
Watu wa Australia.

113

Waingereza wakaketi,
Wakayapiga magoti,
Pasipo na tofauti,
Kila mtu kanuia.

114

Walinuia shari,
Wakashikana hodari,
Jermani na Wahuri,
Damu ikenda milia.

115

Kila mtu haibidi,
Mimi nyuma sirudi,
Wakazuia jadidi,
Kila upande sikia.

116

Vita hivi vya Kreti,
Vilileta parachuti,
Kikaenea maiti,
Pande zote kisiwa.

117

Vita vilifanya pito,
Hata bara ya fukuto,
Katika nchi toto,
Afrika mwasikia.

118

Walifurahi Wahabeshi,
Kukutanisha majeshi,
Wakaupuliza moshi,
Kwenda kwa Waitalia.

119

Tena nataka niweke,
Kila neno peke yake,
Ili yasichanganyike,
Haya ninayowambia.

120

Sasa tunayo nafasi,
'Tawaeleza ya Hess,
Ambaye aliwaasi,
Nazi akawakimbia.

121

Huyu ni Nazi wa tatu,
Wakihesabiwa watu,
Ambao ni watukutu,
Katika Ulaya nzima.

122

Nazi huyu mashuhuri,
Tena ndiye msiri,
Katika hizi shari,
Hitler alizozua.

123

Aliona utukutu,
Na kuwadhulumu watu,
Moyoni hutia kutu,
Chama akakikataa.

124

Hodari alisifika,
Kwa vitabu kuandika,
Nazi wakaona shaka,
Siku aliyokimbia.

125

Stadi wa kuandika,
Maneno yenye kuwaka,
Ambayo yalitumika,
Wadachi kuwachochea.

126

Maneno yake huvuta,
Moyo ukataka vita,
Na mambo yenye matata,
Ya ufili na hadaa.

127

Alikikataa chama,
Wenziwe akawahama,
Njia akaiandama,
Kwa eropleni sikia.

128

Ghaffa aliwatoka,
Nazi wakafadhaika,
Pasiwe mwenye kucheka,
Wote wakaajabia.

129

Alikwenda Uingereza,
Moyo wake kuupoza,
Ikawa ni miujiza,
Dunia ikashangaa.

130

Wakasema "Laitani,
Hatujui kuna nini,
Ametendwa jambo gani,
Hata akawakimbia!"

131

Habari ikanadiwa,
Kuwa Hess augua,
Akili amepotewa,
Akaitwa mkichaa.

132

Hili si kweli sikiza,
Ni hoja ya kupuuza,
Hess alipatilizwa,
Uwongo akabuniwa.

133

Alibuniwa uongo,
Mweusi kama mpingo,
Kuwatia watu chongo,
Kuzidi kuwahadaa.

134

Panya kushuka chomboni,
Akajitosa majini,
Chombo kimo msibani,
Nataka watabiria.

135

Kuondoka kwake Hess,
Ukenda mbio utesi,
Hata nchi ya Warussi,
Bunduki zikalia.

136

Hawa Warussia taibu,
Katika hiki kitabu,
Nizionyeshe sababu,
Msome na kuelewa.

137

Warussia walijihesabu,
Kuwa wao masahibu,
Wadachi hawatasharibu,
Kwao hawatashambulia.

138

Kumbe walijighilibu,
Msiba ukawasibu,
Wakaionja taabu,
Nzito kuvumilia.

139

Wakatoka shirikani,
Pamoja na Jermani,
Ikawa ni nuksani,
Ghafla wasiwe bia.

140

Akanena Stalin,
"Maarifa ya vitani,
Wenzangu sikilizeni,
Nataka wahadithia."

141

"Miji yenu chomeni,
Mashamba yaharibuni,
Mali ziteketezeni,
Nyuma mkirejea."

142

"Kila hatua ya nyuma,
Pigeni ngumi ya chuma,
Wajue kuna kiamaa,
Waache kushambulia."

143

"Pigeni ngumi nzito,
Liwaingie fukuto,
Hata wafanye majuto,
Ya kuchokoza Russia."

144

"Tena pigeni mateke,
Adui awatanuke,
Teteeni wanawake,
Watoto na nchi pia."

145

"Mauti yenye fahari,
Ni ya kufa kwa uhuri,
Ndiyo mauti mazuri,
Sasa yametufikia."

146

"Ifanyeni kazi yenu,
Adui aone mbinu,
Pasibakiye kipenu,
Ikiwa mtazidiwa."

147

"Moyoni nina hakika,
Wajermani watachoka,
Kabla kutimu mwaka,
Watajuta kutujia."

148

Stalin nakariri,
Warussia walimkiri,
Hodari kwa ujasiri,
Wala hofu hakujua.

149

Kwa kujiwa na ari,
Ya kutetea uhuri,
Akaitwa mjeuri,
Na Wadachi wote pia.

150

Walifanyiza ghadhabu,
Wakataka kumwadhibu,
Na nchi kuiharibu,
Uvunjike uhuria.

151

Stalin kasimama,
Tena maneno kasema,
Sauti ikavuma,
Watu wote wakasikia.

152

"Jermani katuanza,
Kwa kutudanganya kwanza,
Sasa vita vitaanza,
Tumekwisha kutambua."

153

Vita aliwaalika,
Mashujaa kwa haraka,
Wote wakamwitika,
Adui kumzuia.

154

Kuzuia kwa Warussi,
Wadachi kama mkasi,
Wa kukata karatasi,
Wakaingia Russia.

155

Russia ina halaiki,
Watu malaki lukuki,
Na majeshi kama nyuki,
Iliyojiandalia.

156

Ina watu wabishi,
Wanaoupenda moshi,
Baruti kwao marashi,
Manukato hutumia.

157

Hao ni shujaa safi,
Wavunjao ukorofi,
Na kukomesha ulafi,
Wa wenye kushambulia.

158

Wadachi walipokuja,
Wakavunjiwa daraja,
Iliyo kubwa kioja,
Katika nzima dunia.

159

Mto huo wa daraja,
Jina lake nitataja,
Mtambue moja moja,
Ninayowahadithia.

160

Jina lake nitawapa,
Kwa kuliandika hapa,
Huo ni mto Nipa,
Maandishi Kiswahilia.

161

Warussia walibarizi,
Kuzuia shambulizi,
Kila mtu kwa mapenzi,
Nchi waliigombea.

162

Iliwapanda ari,
Jamii ya askari,
Wasichelee hatari,
Mbele wakawania.

163

Warussia walipigana,
Kwa ushujaa sana,
Watu wakazuiana,
Katika kila hatua.

164

Taifa hili hutisha,
Vita likipiganisha,
Lazima litakomesha,
Adui kushambulia.

165

Ndilo taifa jepesi,
La kurudisha kisasi,
Wengi limewafilisi,
Waliolishambulia.

166

Huko Russia zamani,
Shujaa Napoleon,
Alipofika mjini,
Moscow akakimbia.

167

Jeshi lake lilivia,
Ushindi ukapotea,
Watu wake walijeruhiwa,
Na wengi waliuawa.

168

Sasa tumefika hapa,
Nitawambia mapipa,
Yenye mfano wa papa,
Vyombo kuvilipukia.

169

Mapipa yana utambi,
Yakiguswa ni vitimbi,
Yanarusha kama wimbi,
Na kuzamisha sawia.

170

Mapipa hayo kuwaka,
Mepesi ya kufyatuka,
Kama mtego hushika,
Vyombo vikikaribia.

171

Zikaja sabmarini,
Ziwezazo kwenda chini,
Silaha za baharini,
Vyombo vikatobolewa.

172

Hizo sabmarini,
Kali haziwezekani,
Zikajilaza kinani,
Vyombo kuvivizia.

173

Kati ya maji mengi,
Vyombo vikazama vingi,
Hasara ikawa nyingi,
Siwezi wahesabia.

174

Ikawa ni mvurugo,
Bahari ikajaa jogo,
Maiti kama magogo,
Maji yakawaua.

175

Nawataka mfahamu,
Jambo jingine muhimu,
Kwa kuliandika humu,
Nje lisije bakia.

176

Jambo hili maalum,
Mjue lilihitemu,
Likawa kama wazimu,
Katika bara Asia.

177

Rashid bin Ali,
Alifanya ufedhuli,
Akajidai ukali,
Kuwapinga Wahuria.

178

Huyu Rashid sikia,
Alikwisha ghilibiwa,
Kichwa kikamkua,
Akafanya maasia.

179

Kichwa kilipomkua,
Kwa vile kughilibiwa,
Alianza maasia,
Akavunjiwa murua.

180

Vita vilitaharaki,
Vikenda hata Irak,
Nchi ya marafiki,
Kwa sababu ya hadaa.

205

Alikuja kwa dhamiri,
Ili kuzuia shari,
Kupigania uhuri,
Ndilo alilokujia.

206

Alifanya masharti,
Ya vita kuvizatiti,
Akakusanya umati,
Upande wa Wahuria.

207

Afrika ya Kusini,
Pamoja na Kasikazini,
Zilileta vitani,
Watu mamia mamia.

208

Afrika ya Mashariki,
Msaada haukubaki,
Pande zote zilishiriki,
Kuzuia Waitalia.

209

Ilipiganwa kondo,
Ya kuzuia mawindo,
Wakatolewa madundo,
Watu wa Italia.

210

Haille Selassie sikia,
Mfalme wa Abyssinia,
Enzini alirejea,
Kama alivyokuwa.

211

Ukazidi upigani,
Hata katika koloni,
Zile za Wataliani,
Pia zikachukuliwa.

212

Walikamatwa mateka,
Vigumu kuhesabika,
Vita vikawachujuka,
Hasara wakajutia.

213

Ndiyo faida ya shari,
Na majazi ya kiburi,
Apatayo mjeuri,
Mtendaji maasia.

214

Mfuasi wa jeuri,
Mwisho hutahayari,
Akatamani kaburi,
Bila nduli kumjia.

215

Majeshi ya Afrika,
Mbele aliyeyashika,
Heri ni kumwandika,
Nanyi mpate mjua.

216

Jina aitwa Wavell,
Kiongozi wa akili,
Tena shujaa wa kweli,
Ndiye aliyetangulia.

217

Akaja tena Cunningham,
Shujaa aliyetimu,
Akashika yake zamu,
Adui kumzuia.

218

Na wale waandamizi,
Kama wale viongozi,
Wakaja kushika kazi,
Afrika sikia.

219

Ndipo vikenda Libya,
Vita ninavyowambia,
Huko vikakawia,
Muda vikachukua.

220

Sasa turudi Urussi,
Tukatazame mkosi,
Ulioharibu vikosi,
Vya wenye kushambulia.

221

Msidhani twapotea,
Ndivyo yalivyotokea,
Mambo ninayowambia,
Kila upande sikia.

222

Wajibu kuyafuata,
Njia yaliyopita,
Hata yalipopata,
Tuone na kuyajua.

223

Wadachi kutaka shinda,
Warussia walijilinda,
Wafu wengi wakenda,
Ahera wakaingia.

224

Walipigana makonde,
Ya nguvu kila upande,
Wote wataka washinde,
Jermani na Russia.

225

Vita walivyopigana,
Mfano wake hapana,
Jinsi walivyoshikana,
Wadachi na Warussia.

226

Vita vilipositawi,
Mara kama kwa uchawi,
Baridi ilikata tawi,
Adui alilokalia.

227

Baridi ilipozidi,
Ikafanya uhasidi,
Upande wa wakaidi,
Wote wakalegea.

228

Iliwakausha watu,
Wasiweze shika kitu,
Kama chombo chenye kutu,
Viungo vilipumbaa.

229

Watu walipata ganzi,
Ikawashinda kazi,
Ila kuvuta pumzi,
Na macho kuangalia.

230

Russia ni maarufu,
Kuna sifa ya barafu,
Ambayo hutia hofu,
Wakati wa kuingia.

231

Tena kuna theluji,
Sikilizeni waimbaji,
Wakati wa kuhariji,
Inataka mazoea.

232

Baridi iliposhuka,
Watu wakatetemeka,
Wageni waliofika,
Maji yakawajalia.

233

Dawa walizijaribu,
Lakini hazikutibu,
Baridi hiyo harabu,
Siwezi kukusifia.

234

Baridi ilivuruga,
Ikatia moyo woga,
Kila mahali mizoga,
Nchi ikatishia.

235

Kama vile utelezi,
Theluji ikawahizi,
Zikakoma shambulizi,
Mbele kuendelea.

236

Ghafa ikaja koto,
Mwilini hamna joto,
Mwendo ukawa mzito,
Watu wakazizimiwa.

237

Kama mfano wa chui,
Wakarukiwa adui,
Wadachi wakawa hoi,
Nyuma wakarejea.

238

Haya yalipotimu,
Wakapeleka salamu,
Kuwa Russia Jahanamu,
Hitler akaambiwa.

239

“Warussia kama visiki,
Nyuma kwenda hawataki,
Na baridi ina dhiki,
Hatuwezi vumilia.”

240

“Warussia wameshika kasi,
Ujapo piga risasi,
Hawatoi nafasi,
Ila mbele kusogea.”

241

“Wanakuja kama nyuki,
Bila hofu ya bunduki,
Wala hawataharuki,
Ajabu kusimulia.”

242

“Warussia ni wafujaji,
Wanasonga hawangoji,
Kama moto kwa maji,
Shambulio linazimwa.”

243

“Miji tuliyoiteka,
Sasa inatutoka,
Shauri lako twataka,
Mambo yametuchachia.”

244

“Tujapo fanya juhudi,
Lazima nyuma turudi,
Kwa sababu ya baridi,
Kali twakusifia.”

245

“Kusema kweli thawabu,
Tumo katika aibu,
Iliyo kubwa ajabu,
Dunia kushuhudia.”

246

“Russia inatisha,
Watu wengi inafisha,
Hatuwezi bahatisha,
Lazima tutakimbia.”

247

“Warussia wana udhia,
Mno wametuzuia,
Wala hapana njia,
Kuwa tutabakia.”

248

“Kila tukipigana,
Nguvu kwetu hakuna,
Tena tumesongwa sana,
Warussia wametukamia.”

249

“Kila njia ya nusura,
Kwetu twaona hasara,
Imetutoka harara,
Vita vimetuchukia.”

250

“Vita havipiganiki,
Moscow haitekeki,
Kwa sababu ya dhiki,
Hii tunayokwambia.”

251

“Kukicha tunafariki,
Wengi hatuhesabiki,
Wote tumetaharuki,
Baa imetushukia.”

252

Hitler kajifariji,
Watu wake kawahoji,
“Lazima sasa singoji,”
Uamiri kachukua.

253
Hitler kajiapisha,
"Baridi hiyo ikisha,
Vita nitavirudisha,
Sitaacha Warussia."

254
"Russia haina salama,
Ila kwa kuungama,
Kuwa sasa imekoma,
Wadachi kuwachezea."

255
"Nitaanzisha utesi,
Urudi tena Urussi,
Kushindwa kwetu matusi,
Siwezi kuvumilia."

256
"Utarudi tena utesi,
Bara ya watu weusi,
Nikalipize kisasi,
Cha rafiki Italia."

257
"Uteshi huu siachi,
Utarudi uwe mbichi,
Hapatabakia nchi,
Zote 'tazishambulia.'"

258
Turudi tuzungumze,
Mengine niwaeleze,
Nanyi myasikilize,
Mfahamu moja moja.

259
Mapigano yalitanga,
Na sisi tusitie nanga,
Tujaribu kuyachunga,
Tuyaweke zizi moja.

260
Turudi hata Atlantiki,
Tukatazame ushabiki,
Na mitego ya fataki,
Wadachi waliyotia.

261
Wadachi walihamaki,
Wote wakajaa chuki,
Wakasema "Atlantiki,
Vyombo havitaelea."

262
Wadachi walikasirika,
Kwa sababu Amerika,
Zana ilipeleka,
Kusaidia uhuria.

263
"Waamerika hiana,
Kwetu hawaleti zana,
Basi itakosekana,
Njia ya kupitishia."

264
"Vyombo havitasafiri,
Tutazuia bahari,
Zana kwenda kwa Wahuri,
Hazitakuwa na njia."

265
Waamerika hawakuhini,
Kuuzia Jermani,
Zana walizotamani,
Ila walikosa njia.

266
Wajermani walikosa njia,
Ya zana kuzivushia,
Waingereza walizuia,
Njia za kuabiria.

267
Jambo hili lilikera,
Kwa vile kutiwa fora,
Wakaibuni dharura,
Vyombo kuvishambulia.

268
Wadachi wakatamka,
"Meli za Waamerika,
Bahari hazitavuka,
Zote zitaangamia."

269
Ikatiwa katikati,
Mitego yenye baruti,
Yakaenea mauti,
Bahari ikatishia.

270
Meli zikenda mrama,
Nyingi sana zikazama,
Kwa sabmarini za chuma,
Wadachi walizotia.

271
Ndipo alipojibari,
Bwana tena wa bahari,
Kuiondoa hatari,
Kila ilipoenea.

272
Simba alipiga kumbo,
Kwa silaha za mitambo,
Ghafla hivi kitambo,
Wadachi wakachachiwa.

273
Bahari ilipochacha,
Wadachi walipekecha,
Wakawavuta kwa kucha,
Wajapani kusaidia.

274
Hao Wajapani sikia,
Ni taifa la Asia,
Ambalo lina udhia,
Majirani kuonea.

275
Jirani yake hasa China,
Siku zote wapigana,
Taifa hili fitina,
Halijui kutulia.

276
Mara pasipo habari,
Wakaanzisha shari,
Kupigana na uhuri,
Na Amerika pamoja.

277

Waamerika washabiki,
Kwa michezo ya bunduki,
Vita hawasikitiki,
Iwapo wameanziwa.

278

Fisi kuchokoza tembo,
Na kujifunga masombo,
Jamani makeni mambo,
Haya ya Japania!

279

Jamani makeni shani,
Aliyofanya Japani,
Kubwa haina kifani,
Kadiri wala usawa!

280

Makeni hiki kimako,
Cha kutaka sikitiko,
Na kujitia mwako,
Moto kujivutia!

281

Makeni hiki kioja,
Cha Wajapani kuja
Vitani kujifuja,
Maovu kushindania!

282

Kwani kujipaka shombo,
Kwa kuchokoza mambo,
Fisi kumpiga tembo,
Ni kutafuta makiwa!

283

Tazameni tena fumbo,
Sababu kumeza chambo,
Cha ndoana ya mtambo,
Japani alighumiwa!

284

Japo fisi mgwizi,
Kadiri yake ni mbuzi,
Fisi tembo hamwezi,
Wala hawawi sawa.

285

Fisi mlaji makombo,
Ajabu kushika fimbo,
Kwa tamaa ya tumbo,
Jinsi inavyozuzua!

286

Tamaa hii ya tumbo,
Huchafua sana mambo,
Ndiyo iletayo tambo,
Ngumu sana kufungua.

287

Wajapani wasogora,
Wanajidai ubora,
Asia pwani na bara,
Kutawala wanuia.

288

Taifa hili habithi,
Kwa kutaka kurithi,
Nchi zenye warithi,
Wenyewe kuwaonea.

289

Ndilo taifa laghai,
Lifanyizalo kiso,
Kutafuta uadui,
Bure pasipo hatia.

290

Daima halitulii,
Wala halikinai,
Linapenda uadui,
Lipate cha kutumia.

291

Ni taifa badilifu,
Lenye bidhaa hafifu,
Za kunyang'anya sarafu,
Za shilingi na rupia.

292

Ajapo fanya husuda,
Japani maji ya soda,
Nguvuye haina muda,
Hufa ikizibuliwa.

293

Hawakupata faida,
Walipofanya husuda,
Machina kwa kawaida,
Cheo wakawavunjia.

294

Hawajui taamuli,
Wanajidai akili,
Hali ndiyo wakatili,
Maadui wa dunia.

295

Japo Japani aweza,
Vita kuvitengeneza,
Lakini Waingereza,
Si watu wa kuchezea.

296

Waingereza msumeno,
Mkali wa menomeno,
Kisha stadi mno,
Vita wamevizoea.

297

Wa kwanza kwa mapatano,
Wa kwanza kwa mapigano,
Tena hawana mfano,
Kwa dhiki kuvumilia.

298

Kurukia Waingereza,
Pasipo kukuchokoza,
Ni kutaka jikereza,
Msiba kujitia.

299

Wangetumia fikara,
Wasingeona dharura,
Ya kutumia kura,
Msiba kuuchumbia.

300

Kila jambo la kura,
Haba yake tijara,
Ila wingi wa hasara,
Nyuma hufuatia.

301

Kila afanyaye ngoa,
Maovu yatamjia,
Akose la kuchagua,
Jambo jema kutumia.

302

Ngoa inakashifu,
Isipofungwa mkufu,
Inafanya upotofu,
Kugombana na dunia.

303

Inataka mnyororo,
Ifungwe kama mtoro,
Ngoa ina mgogoro,
Watu wengi humia.

304

Walidai uamuzi,
Kupeleka mabalizi,
Amerika kubarizi,
Hali wanayo ngoa.

305

Hakika hiki kijicho,
Mtu akiwa nacho,
Kinapofusha macho,
Uoni ukapotea.

306

Ndivyo utendavyo wivu,
Kuleta mambo mabovu,
Ukazuia mabivu,
Yafaayo kutumia.

307

Yafaayo kutumia,
Hayaji kwa mwenye ngoa,
Maana ndiyo tabia,
Mungu anayochukia.

308

Kabla kuwa tayari,
Zilipigwa manowari,
Bora mbili za Wahuri,
Zikazama mara moja.

309

Majina yake halisi,
Ni Prinsi wa Walesi,
Inayojua utesi,
Mtazidi kusikia.

310

Ya pili yake Repulsi,
Shabaha nambari mosi,
Wala haikosikosi,
Pigo lake linaua.

311

Vyombo bora kwa wezani,
Na nguvu ya upigani,
Vikazama baharini,
Kwa bomu za Japania.

312

Prinsi wa Walesi,
Ilishiriki utesi,
Ikaziharibu kasi,
Za Bismarck sikia.

313

Ndiyo manowari tesi,
Iliyokwenda upesi,
Kulipiza kisasi,
Hood kuilipia.

314

Haikumpa nafasi,
Kurudi kwao mtesi,
Kutoa habari halisi,
Na nishani kutia.

315

Bismarck ya vita,
Iliyoitwa ukuta,
Ikafa kwa miezi sita,
Tangu ilipotumiwa.

316

Haikuwahi kuishi,
Tena kuzidisha mashi,
Ikapita kama moshi,
Au umeme wa mvua.

317

Baada ya siku chache,
Ilizama ijifiche,
Maji yasiyo machache,
Yakaipoteza pia.

318

Ilizama na nahodha,
Wa sifa kadha wa kadha,
Hasara ikawa adha,
Wadachi wakalemewa.

319

Simba mwenye makinda,
Ndivyo anavyotenda,
Pangoni mwake ukenda,
Lazima kuraruliwa.

320

Sifa za ile Repulsi,
Zaidi siwezi kisi,
Kuwa nyuma ya kiasi,
Ndivyo ninavyochelea.

321

Zilipigwa makombora,
Kwa ndege za wasogora,
Wanaotaka ubora,
Kuitawala dunia.

322

Kabla kwenda kinani,
Ziliangusha baharini,
Wanahewa wa Japani,
Wengi kuwahesabia.

323

Ndiyo mauti ya simba,
Hafi peke bila kimba,
Sauti hii humba,
Sikioni mwa shujaa.

324

Ndiyo sauti ya tamu,
Itiayo moyo hamu,
Ya kupinga udhalimu,
Kwa thamani zote pia.

325

Jamii ya mabaharia,
Wale waliorukiwa,
Wengi waliogelea,
Kwa bahari kuijua.

326

Kabla ya Singapore,
Nchi iliyorukiwa,
Mara ikapotea,
Ni Siam nawambia.

327

Japani wenye wazimu,
Waliipiga Siam,
Nchi ndogo kwa hirimu,
Siam ikaangukia.

328

Siku zote wadhalimu,
Hawachagui hirimu,
Ila kumwaga damu,
Ya wanyonge na wakiwa.

329

Hii ndiyo elimu,
Ambayo wamehitimu,
Wakuu wa udhalimu,
Wanyonge kuwaonea.

330

Ahadi zao haramu,
Sababu shida kutimu,
Dhalimu hana fahamu,
Tamaa ikimjaa.

331

Hong-Kong na Singapore,
Vita vikenda kutua,
Adui wakatokea,
Wengi wasio mithaa.

332

Walikuja kama nzige,
Katika yao madege,
Kusudi nao waige,
Wadachi wa Ulaya.

333

Kama nywele kwa kuota,
Ujapo zikatakata,
Ndivyo walivyoleta,
Madege Wajapania.

334

Walikuja wawaige,
Wapate tonge wamege,
Wingi wao wa nzige,
Moto ukawashiwa.

335

Ndipo walipouawa,
Wengi wa kuajibiwa,
Halafu wakaachiwa,
Nchi tupu za ukiwa.

336

Kusudi waliachiwa,
Nchi tupu za ukiwa,
Wapate jifaragua,
Izidi yao tamaa.

337

Guu mbele guu nyuma,
Ndivyo wanavyouzima,
Moto wa hasama,
Waingereza sikia.

338

Huu ndiyo mwendo wao,
Uwachoshao wenzao,
Yakawatoka mapayo,
Ya vita kushambulia.

339

Wana mbinu watu hao,
Wanaelewa matao,
Kila mtu mwenye payo,
Kwa vita humwagua.

340

Daima wana kituo,
Hawataharuki moyo,
Wanajua mapinduo,
Wenzao kuwafanyia.

341

Wanajua mapinduo,
Hata wakienda mbio,
Razini akili zao,
Shida sana kupotea.

342

Japo wakienda mbio,
Nyuma huziacha kwao,
Kukwaza adui yao,
Mbele wanaowania.

343

Nyuma huacha vikwazo,
Vinavyofanya mizozo,
Na wingi wa matatizo,
Nchi wakiiachia.

344

Waingereza weledi,
Wa kupiga mjeledi,
Hata nyuma wakirudi,
Usambe wataachia.

345

Ndiyo wapigao shindo,
Wakiwa katika kondo
Wakafanya matendo,
Ajabu kusimulia.

346

Kila taifa kaidi,
Wamepata kulirudi,
Japani haina budi,
Mwisho kujutia.

347

Ndiyo waliohasiri,
Majeshi ya askari,
Zamani za Kaizari,
Koloni wakachukua.

348

Ndiyo watu wa sulubu,
Vita wanaovitibu,
Ukakoma uharabu,
Dunia ikatulua.

349

Ndiyo wanaoghilibu,
Adui mwenye ghadhabu,
Akavutwa taratibu,
Mtegoni kuingia.

350

Ndiyo wajua siri,
Zinazovunja kiburi,
Na kuamua shari,
Amani ikarejea.

351

Ndiyo watu wa busara,
Wajuao njia bora,
Ya kuvunja usogora,
Mtu akiwafanyia.

352

Ni mabwana wa bahari,
Walio na manowari,
Zitawalazo bahari,
Pande zote za dunia.

353

Kisha wana makini,
Akili zao razini,
Wanajua upigani,
Wala hawana fadhaa.

354

Ni ajabu kuchezeza,
Makucha kubeuliwa,
Yawezayo kurarua,
Na maadui kuua.

355

Mahali nilipofika,
Nataka mkikishika,
Chuo ninachoandika,
Mfahamu zaidia.

356

Nataka mkifunua,
Kitabu mkipekua,
Mzidi tena kujua,
Mambo pasipo udhia.

357

Kwa hivi nitarudia,
Kule nilikoachia,
Nizidi kuyafunua,
Mambo yaliyowadia.

358

Turudi kwa Jermani,
Alipokuja Japani,
Kushiriki vitani,
Nini ilitazamiwa?

359

Alipokuja Japani,
Jermani alidhani,
Haja yake moyoni,
Mara itatimia.

360

Hitler alidhani,
Manowari Britani,
Zitakwenda kwa Japani,
Kusudi apate njia.

361

Mtego walioweka,
Kitu haukushika,
Dhiki ikaongezeka,
Kwa vita kuendelea.

362

Badala ya kulegea,
Kama walivyodhania,
Kisiwa kiliendelea,
Vita kuviandalia.

363

Waingereza kule kwao,
Walikuwa peke yao,
Wakawapata wenzao,
Sasa kuwasaidia.

364

Nataka hizi kurasa,
Ziseme habari hasa,
Isiwe ni kupapasa,
Kushika na kuachia.

365

Kabla ya kwenda mbali,
Ninaona afadhali,
Tuzitazame feli,
Nyuma zilizotokea.

366

Nitawambia safari,
Alizokwenda Waziri,
Za kufanya mashauri,
Na njia ya kutumia.

367

Safari yake awali,
Amerika Churchill,
Ilikuwa ya shughuli,
Ya zana za kutumia.

368

Alikwenda kuonana,
Na mtu mwenye maana,
Wakapata kukutana,
Baharini sikia.

369

Ilikuwa ya hatari,
Safari yake Waziri,
Katikati ya bahari,
Ndipo ilikoishia.

370

Alikwenda kwa manowari,
Safari yake Waziri,
Asihofu hatari,
Majini iliyotiwa.

371

Alikwenda kubarizi,
Pamoja na kiongozi,
Jina lake hili wazi,
Roosevelt msifiwa.

372

Habari walihubiri,
Katikati ya bahari,
Wakaagana kwa heri,
Kila mtu karejea.

373

Baraza kati ya maji,
Ilikunjisha vipaji,
Maadui wakahoji,
“Nini imetokea?”

374

Safari yake ya pili,
Kwa Marafiki wa mbali,
Ilihusu ufedhuli,
Ule wa Japania.

375

Wakati alipofika,
Churchill Amerika,
Watu walikutanika,
Baraza akafanyiwa.

376

Watu walifurahiwa,
Kwa vile kuwaendea,
Wakakutana mamia,
Wapate kumsikia.

377

Alifanyiwa baraza,
Kubwa sana kueleza,
Watu wakasikiliza,
Maneno akawambia.

378

Wote wakasikiliza,
Pasiwe mwenye kupuuza,
Kila aliloeleza,
Watu waliitikia.

379

Alinena kwa sauti,
Ya usemi madhubuti,
Unaoshika umati,
Wakati wa kusikia.

380

Alisema kwa imara,
Maneno yenye dharura,
Yaonyayo njia bora,
Ifaayo kutumia.

381

Kawambia Roosevelt,
“Waona uasharati,
Wa kuharibu umati,
Huu wa Japania?”

382

“Haifai kutulia,
Watu wakiangamia,
Ustaarabu kupotea,
Ndivyo ninavyohofia.”

383

“Haifai kutulia,
Wakiwa wanapotea,
Wajibu ni kuzuia,
Uadui wa dunia.”

384

Roosevelt mashuhuri,
Wa kufanya mashauri,
Kusema na kufikiri,
Kama kope kufumbua.

385

Mwepesi kama umeme,
Wa kutia mambo shime,
Yahusuyo wanaume,
Na kuwaza mara moja.

386

Maneno yake mufti,
Safi bila tofauti,
Hufurahisha umati,
Wakati wa kuyatoa.

387

Roosevelt alinena,
“Mambo yote nimeona,
Nami nashangaa sana,
Japani kuturukia.”

388

“Nimeshangaa ajabu,
Kutuvunjia adabu,
Hali tuna usahibu,
Sisi na Japania.”

389

“Ninavyoona ajabu,
Ni kuvunja usahibu,
Jambo hili la ajabu,
Japani kutufanyia.”

390

“Naona kama ruia,
Haya yaliyotokea,
Japani kuturukia,
Hili sikutazamia.”

391

“Kwa hivi hapana budi,
Tutafanya jitihadi,
Kuzuia uhasidi,
Huu uliotujia.”

392

“Lazima niombe Mungu,
Niuzuie uchungu,
Watasema walimwengu,
Nani mwenye hatia.”

393

Basi akatia shime,
Kawambia wanaume,
“Nguvu zetu tuzitume,
Wakati umewadia.”

394

Akazidisha kauli,
Roosevelt kule mbali,
“Sasa hivi sikubali,
Tena kuvumilia.”

395

“Uvumilivu una mwisho,
Hauhimili kitisho,
Heri tukatoke jasho,
Kwa vita kuvizuia.”

396

“Saburi hustahili,
Shari ikiwa mbali,
Lakini sasa muhali,
Kuzidi kuvumilia.”

397

“Ninaona si halali,
Kuzidi kustahamili,
Matendo ya ukatili,
Kukicha yaendelea.”

398

“Matendo yenye dhuluma,
Mioyoni yanauma,
Hapana jambo jema,
Kuliko kuyazuia.”

399

“Tumejitahidi sana,
Tuishi kwa kupatana,
Tuepuke kuuana,
Yote hayakufaa.”

400

“Kwa kuitaka amani,
Tumepata nuksani,
Sasa tumo vitani,
Sisi na Wajapania.”

401

“Kujitetea thawabu,
Mungu hatatuadhibu,
Hatukuvunja adabu,
Wala hatuna hatia.”

402

“Tutaungana kwa nta,
Tukakomeshe matata,
Hitler aliyoleta,
Kuiharibu dunia.”

403

“Ingawa tumestahi,
Tumeonywa ikirahi,
Kama hatutanabahi,
Heshima tutavunjiwa.”

404

“Tujapo fanya staha,
Hapana tena nasaha,
Heri tushike silaha,
Upande wa Wahuria.”

405

“Madhali tumerukiwa,
Wajibu kujitetea,
Mungu amehusia,
Roho kuipigania.”

406

“Lazima vita tushike,
Tukakomeshe makeke,
Dunia ipumzike,
Ndilo jambo la sheria.”

407

“Japani imetutaka,
Vita imetualika,
Wajibu ni kuitika,
Ndilo neno la murua.”

408

“Tumejitahidi sana,
Kuiepuka fitina,
Sasa tutapigana,
Maana tumetakiwa.”

409

“Lazima tutapigana,
Sababu ndiyo ungwana,
Tena ni jambo la maana,
Kufa kwa uhuria.”

410

“Nimejitahidi sana,
Na nyinyi wote mwaona,
Kuepuka kuuana,
Lakini haikufaa.”

411

“Faida niliyopata,
Kwa taabu nilizokuta,
Za kuepuka matata,
Ni vita kutangaziwa.”

412

“Ufedhuli wa Japani,
Haufutiki moyoni,
Hawapati afuweni,
Neno la kuwaokoa.”

413

Jamii ya wasikizi,
Wale waliobarizi,
Wakajibu “Kiongozi,
Maneno tumesikia.”

414

Wasikizi wakasema,
“Yaona dunia nzima,
Kuwa huna lawama,
Katika hizi ghasia.”

415

“Ghasia hizi za shari,
Si zako wewe Amiri,
Na sisi tumekukiri,
Kuwa huna hatia.”

416

“Tutaungana kwa gundi,
Twende makundi makundi,
Tukawaonye ufundi,
Adui wa uhuria.”

417

“Ingawa tuna baadhi,
Lazima vita turidhi,
Tutetee yetu hadhi,
Roosevelt kajibiwa.

418

“Zitaungana baadhi,
Tupiganiye hifadhi,
Bure kuvunjiwa hadhi,
Ni uchungu kusikia.”

419

Waamerika sikiza,
Ni hodari miujiza,
Mambo wanayofanyiza,
Ajabu ukisikia.

420

Kutwa wanafanya kazi,
Kucha macho yao wazi,
Hawalali upuuzi,
Watu hao sikia.

421
Ndiyo wanaotengeneza,
Silaha zinazoviza,
Kama vile Waingereza,
Mfano wao mmoja.

422
Ndiyo wenye merikebu,
Watu wanazohesabu,
Zinazohimili taabu,
Vitani zikiingia.

423
Ndiyo wendao utesi,
Kama kuingia arusi,
Hawana wasiwasi,
Wala hofu kutia.

424
Ndiyo waliotakasa,
Matata ya Ufaransa,
Vita vilipowapasa,
Upande wa Britania.

425
Moyoni hawana woga,
Na wepesi wa kupiga,
Kama maji ya kukoga,
Vitani wakiingia.

426
Vita walipovishika,
Watu wa Amerika,
Majeshi walipeleka,
Mengi Britania.

427
Walipelekwa vijana,
Wenye afya nzuri sana,
Wawezao kupigana,
Na dhiki kuvumilia.

428
Walipelekwa kichwani,
Kuzuia Jermani,
Ameachiwa Japani,
Vidole kujirambia.

429
Zamani za kutokea,
Hayo niliyowambia,
Vita viliendelea,
Vikarukia visiwa.

430
Vita vilikwenda mbio,
Vikaingia Borneo,
Vikafanyiwa kituo,
Mashujaa wakakaa.

431
Makusudi wasifiwe,
Ushujaa wagaiwe,
Walitaka waachiwe,
Philippines Wajapania.

432
Wakajibiwa salamu,
"Sharti itoke damu,
Kuacha bure haramu,
Tutazuia visiwa."

433
Wakajibiwa "Mawe,
Lazima vinunuliwe,
Damu nyingi itolewe,
Ndipo tuache visiwa."

434
"Lazima vita tutete,
Maadui wasipite,
Wingi wao tuukate,
Ndilo tungalongojea."

435
Vita vilikwenda Jawa,
Adui wakatokewa,
Wengi wakauawa,
Kwa thamani ya kisiwa.

436
Yalikwenda Sumatra,
Majeshi ya wasogora,
Yakakuta hasara,
Visima moto kutiwa.

437
Visima walivikuta,
Vinavyotoa mafuta,
Vyote moto vimepata,
Hakikubaki kimoja.

438
Vita vilikwenda Burma,
Shindo kubwa likavuma,
Machina wakaja nyuma,
Kuitetea India.

439
Wajibu sasa nipange,
Mataifa niyaunge,
Baadhi mbili nitenge,
Adui kwa Wahuria.

440
Niwapange kwa mafungu,
Baadhi mbili Wazungu,
Na wengine walimwengu,
Vita walionga.

441
Upande wa Jermani,
Walikaa Waitaliani,
Kiongozi Mussolini,
Adui wa uhuria.

442
Udachi tangu hapo,
Ni adui kwa kiapo,
Ajabu kubwa kuwapo,
Umoja na Italia.

443
Wakaja tena Wafini,
Lilo taifa duni,
Waingereza zamani,
Walilotaka kulisaidia.

444
Wakaja Bulgaria,
Vitani kusaidia,
Kuzuia uhuria,
Kwa Wadachi wakakaa.

445

Tena walioingia,
Ni watu wa Rumania,
Kuja kupigania,
Dhuluma na ubaya.

446

Kisha waliotokea,
Vitani wakaingia,
Wadachi kusaidia,
Ni Wayugoslavia.

447

Wengine waliokiri,
Kuja katika shari,
Kupigana na Wahuri,
Watu wa Australia.

448

Baadaye Wahungari,
Walikimbilia shari,
Bure bila takisiri,
Kwa Wadachi wakaingia.

449

Ndipo kuja kisirani,
Taifa la Wajapani,
Likajitia vitani,
Kuvirukia visiwa.

450

Estonia na Latvia,
Pamoja na Lithuania,
Serbia na Albania,
Nyuma wakaandamia.

451

Hao ndiyo watu,
Upande wa mbwa mwitu,
Ambao haki si kitu,
Kwao bora tamaa.

452

Dola nilizoeleza,
Majeshi zilieneza,
Dunia ikawa kiza,
Vita vikazidia.

453

Zilieneza kwa chuki,
Majeshi yenye hamaki,
Kuibatilisha haki,
Na kuharibu dunia.

454

Zilieneza majeshi,
Ukatapakaa moshi,
Kila njia haipishi,
Kwa vita kuenca.

455

Upande wa Waingereza,
Dola zilizotokeza,
Kuja kuzuia kiza,
Majina nitawambia.

456

Awali ya hivi visa,
Walikuja Wafaransa,
Kushindwa kukawapasa,
Wakabaki Wahuria.

457

Waingereza waliteta,
Wakazuia matata,
Siku nyingi zikapita,
Bila kusaidiwa.

458

Hawakuhofu upeke,
Wakawapiga mateke,
Maadui watanuke,
Hata wakatishiwa.

459

Adui alitishiwa,
Karibu kukaribia,
Atakayo hayakuwa,
Ila vita kuzidia.

460

Walisimama wasigwe,
Kama wavutao jugwe,
Wakakitanua kigwe,
Waingereza sikia.

461

Vita walivitanua,
Siku zikaendelea,
Maadui wakajua,
Hakika wamezuiwa.

462

Walizingirisha pete,
Meli kwao zisipite,
Manufaa wasipate,
Vitu vya kupigania.

463

Vitu vilipanda bei,
Nchi zote za adui,
Mtu kitu hanunui,
Ila posho kupimiwa.

464

Vitu viliadimika,
Vigumu kununulika,
Adui wakasumbuka,
Kwa kutiwa mazingiwa.

465

Uzito wa mazingiwa,
Begani ulizidia,
Kila ukichukuliwa,
Ulizidi kulemea.

466

Hasa huko Italia,
Viatu vilipotea,
Jozi kwa shilingi mia,
Kuipata ni udhia.

467

Ndege hutaka mafuta,
Ndipo ziweze kuteta,
Nayo shida kuyapata,
Ikaingia fadhaa.

468

Dhiki hii ya mafuta,
Ndiyo iliyokata,
Urafiki wa matata,
Wa Jermani na Russia.

469

Ghaffa bila kukisi,
Wakaja zao Warussi,
Wakazuia utesi,
Upande wa Britania.

470

Hapana aliyekisi,
Kuwa hawa Warussi,
Watashika utesi,
Shime kwa Wahuria.

471

Hapana aliyedhani,
Kuwa mwisho Jermani,
Atafanya nuksani,
Kurukia Warussia.

472

Ndivyo itendavyo haki,
Kama mtu haitaki,
Humtenga na rafiki,
Akabakiwa na baa.

473

Japo akianguka,
Lazima atainuka,
Mwenye haki kushindika,
Ni ajabu kusikia.

474

Ajapo pata misiba,
Mwenye haki mara saba,
Atanyanyuka kwa huba,
Mungu atamuinua.

475

Lazima asimame,
Mashaka yake yakome,
Yapite kama umeme,
Kama hayakutokea.

476

Mwenye haki husimama,
Kuanguka si daima,
Haki hushinda dhuluma,
Na uovu hukimbia.

477

Mwaka wa tatu wa vita,
Yakatokea matata,
Ambayo yaliwavuta,
Waamerika kuzuia.

478

Kisha wakaja Machina,
Vitani wakaungana,
Kwa Wahuri kupigana,
Uhuru kuutetea.

479

Machina na Wajapani,
Ni adui kwa yamini,
Wakajigawa vitani,
Baadhi mbili wakakaa.

480

Machina ni maarufu,
Kwa vita kuvisarifu,
Dunia nzima husifu,
Milele wanasifiwa.

481

Wale waliorukiwa,
Nchi zikachukuliwa,
Ndiyo waliozidia,
Upande wa Wahuria.

482

Turudi tena tunene,
Habari isiachane,
Kila mtu aone,
Sufi bila madoa.

483

Nataka watu waone,
Ili wasiulizane,
Matendo yote manene,
Njia yaliyopitia.

484

Kwa hivi ninafikiri,
Litakuwa jambo zuri,
Kujua kila bahari,
Vita vilikoenea.

485

Vita vya Atlantiki,
Vilifika Pasifiki,
Bahari ya Aktiki,
Nayo haikusalia.

486

Tena vilikorukia,
Vita fujo vikatia,
Ni bahari ya India,
Ilingiliwa pia.

487

Vilifanyiza kituo,
Vita Mediterraneo,
Yakaja mashambulio,
Kutoka Italia.

488

Hapa vilizohalika,
Ikapita mingi miaka,
Vita havikuondoka,
Ila kuendelea.

489

Hapa hila zilikwisha,
Wasiweze kuhamisha,
Mapigano ya kutisha,
Ya Waingereza sikia.

490

Mapigano ya bahari,
Waingereza ni nambari,
Mosi kwa uhodari,
Wala hawana mithaa.

491

Basi hapa walibana,
Baharini njia pana,
Adui ana kwa ana,
Hakuweza kutokea.

492

Ndipo ulipozuiwa,
Msaada wa Libya,
Hapa usipate njia,
Vyombo vikaangamia.

493
Kila chombo cha kuteta,
Adui alicholeta,
Njia hakikupata,
Ila moto kutiwa.

494
Kama jini la chupani,
Vyombo vya Waitaliani,
Kutoka vilitamani,
Lakini vilifungiwa.

495
Bartolomeo Kolleoni,
Ambayo Waitaliani,
Waliisifu vitani,
Hapa ilishambuliwa.

496
Waitalia walighani,
Kuwa haiwezekani,
Bartolomeo Kolleoni,
Kabisa kushambuliwa.

497
Ilisifiwa upeo,
Mwendo usio cheo,
Wakati wa kwenda mbio,
Taabu kuikaribia.

498
Siku iliyotokewa,
Haikuvuta hatua,
Mbio zilipotea,
Kama haikusifiwa.

499
Hatua zikawa fupi,
Kwenda mbio hazimpi,
Ikatahamaki wapi,
Moto imekwisha tiwa!

500
Ilipigwa ikazama,
Sifa zake za kuvuma,
Mara moja zilikoma,
Siku iliyotokewa.

501
Ilipigwa kwa mizinga,
Na mafundi wa kulenga,
Ikabukuliwa kunga,
Na Sydney sikia.

502
Sydney ni kama tai,
Sifaze milele hai,
Ilipiga Graf Spii,
Vita vya kushirikia.

503
Majeshi ya Taliani,
Yaliyokuwa barani,
Yalikuwa taabani,
Kwa bahari kuzuiwa.

504
Askari hapigani,
Bila chakula tumboni,
Nacho hakipatikani,
Adui akazidiwa.

505
Badala ya baharini,
Walijaribu hewani,
Kwenda kwa eropleni,
Libya Waitalia.

506
Zile eropleni,
Zilizoleta auni,
Kwa majeshi ya barani,
Hazikufaa pia.

507
Ulitokea ugumu,
Katika bahari Sham,
Vyombo vya mahasimu,
Hapa vilikosa njia.

508
Katika Adriatikini,
Adui hakubariki,
Ila alipata dhiki,
Msiba ukamjia.

509
Ili kukimbia dhiki,
Waliifanya handaki,
Bahari ya Baltiki,
Wadachi kujifichia.

510
Vyombo viliwaka moto,
Kwa kupigwa matopito,
Bahari zikawa nzito,
Adui kusafirira.

511
Mafuta yalienea,
Majini yakaelea,
Kwa vyombo kutobolewa,
Kila bahari sikia.

512
Bahari zilichafuka,
Kwa mafuta kumwagika,
Vyombo vingi vikawaka,
Kwa shindo lililotiwa.

513
Vyombo viliwindana,
Baharini kupigana,
Waingereza wakabana,
Maadui na kuua.

514
Walivifukuza mbio,
Vyombo vya mashambulio,
Visipate kituo,
Vingi juu vikapwewa.

515
Vyombo vingi vilipwewa,
Kwa kasi ya kukimbia,
Wala havikutambua,
Namna ya kujittoa.

516
Vilitiwa wasiwasi,
Vyombo vikenda kwa kasi,
Bila kupigwa risasi,
Vikafa kwa kukimbia.

517
Waingereza walivimba,
Baharini wakatamba,
Wakatisha kama simba,
Adui kukaribia.

518
Waingereza waliwamba,
Bahari wakazifumba,
Zote zikawa nyembamba,
Adui kuabiria.

519
Vita walivitandika,
Baharini vikawaka,
Wakazidi kuvishika,
Kwa nguvu na ushujaa.

520
Walivishika kwa nguvu,
Vita kwa uelekevu,
Wakalipwa washupavu,
Mazao yao mabaya.

521
Vita vilizidi nguvu,
Kwa kushikwa kwa ukavu,
Bahari zikawa povu,
Kama sabuni kutiwa.

522
Vyombo havikuokoka,
Ila kushikwa mateka,
Njia ya kunusurika,
Kabisa ilipotea.

523
Kila bahari arifu,
Yenye sifa ya urefu,
Ilikuwa hafifu,
Adui alidhanja.

524
Kila bahari pana,
Maadui waliona,
Kuwa ni hatari sana,
Ndani yake kuelea.

525
Ilipokuwa vizito,
Kupatikana mapito,
Akaamrisha moto,
Hitler vyombo kutiwa.

526
Hitler alihitari,
Vyombo vyake kuhasiri,
Kwa hofu ya manowari,
Za Waingereza sikia.

527
Amri hii ya moto,
Ilizidisha uzito,
Wa hasara na majuto,
Na aibu kujitia.

528
Ilikuwa ni aibu,
Kuzichoma merikebu,
Hitler alizohesabu,
Bora kwa kupigania.

529
Kwa hali ya kusumbuka,
Mujira yaliwatoka,
Mwezi ulikuwa mwaka,
Adui alidhanja.

530
Siku ilikuwa juma,
Kwa mashaka kuwauma,
Wukaanza kulalama,
"Lini mwisho wa udhia?"

531
Tena nataka niwape,
Hubari msiitupe,
Kwa kuiweka peupe,
Kitabuni kutiwa.

532
Mali ya Wajermani,
Kwa sarafu ya pauni,
Hamsini milioni,
Vita walizoanzia.

533
Daima ilipunguka,
Fedha ikatia shaka,
Njia za kuongezeka,
Zote zilizuiwa.

534
Hofu ya kufilisika,
Iliwatia haraka,
Wadachi wakataka,
Ushindi wa mara moja.

535
Waingereza mali yao,
Katika akiba zao,
Nyingi kuliko hiyo,
Hesabu nitawambia.

536
Hesabu ni bilioni,
Nane hasa za pauni,
Elfu moja milioni,
Juu ilizidia.

537
Fedha hii ilizidi,
Kila siku kwa idadi,
Ikatimiza mradi,
Kutumia kila njia.

538
Sasa nawapa undani,
Mjue hata kiini,
Tamaa ya Jermani,
Vita walipoingia.

539
Tamaa ya Jermani,
Kwa kujitia vitani,
Ni kushinda kwa hewani,
Vita hivi sikia.

540
Ndivyo walivyowaza,
Dunia kuigeuza,
Na kushinda Waingereza,
Kwa vita katika hewa.

541

Basi huko hewani,
Walikuta upigani,
Wa kuonyesha yakini,
Ushindi kuwapotea.

542

Walikuta upigani,
Mkali huko hewani,
Wao wasiwe kifani,
Kwa nguvu na ushujaa.

543

Kosa la kupeleleza,
Nguvu ya Waingereza,
Mara lilijitokeza,
Tamaa ikakimbia.

544

Kosa la kukadirisha,
Nguvu yao ya kutisha,
Mara lilitetemsha,
Maadui kwa fadhaa.

545

Wadachi walieleza,
Ndege za Waingereza,
Kwao hazitatokeza,
Kwa vita katika hewa.

546

Ndege zilipotokea,
Wadachi wakatambua,
Simba amekusudia,
Makinda kuyatetea.

547

Waingereza waliteta,
Juu kuzuia vita,
Kisha wakazifuata,
Nchi za adui pia.

548

Mahali walipotaka,
Ndege zao zilifika,
Wala hazikutoroka,
Adui kumkimbia.

549

Zikenda eropleni,
Mara kwa Wajermani,
Mara kwa Waitaliani,
Bomu kuwangushia.

550

Zilikwenda mfulizo,
Zisitue ndege hizo,
Zikafanya matatizo,
Kila zilipotokea.

551

Nchi zote za hasimu,
Ziliangushiwa bomu,
Haikubaki sehemu,
Bomu isiyotupiwa.

552

Wanahewa walipiga,
Pasipo kufanya woga,
Viwanja wakavuruga,
Vya eropleni kutua.

553

Hawakuhofu mizinga,
Chini iliyowakinga,
Walizidi kuilenga,
Ili moto kuitia.

554

Ndege zao ziliranda,
Kuma wingu zikatanda,
Kila walipopenda,
Bomu walizifyatua.

555

Waingereza waliponda,
Kila penye kiwanda,
Wakaunguza mabanda,
Ya zana kutengenezea.

556

Ndege hazikuogopa,
Bomu zake zilitupa,
Mahali hapa na hapa,
Hasara ikaenea.

557

Bomu zake zilitua,
Kama matone ya mvua,
Moto chini zikatoa,
Nchi zikateketea.

558

Bomu zilijimwaga,
Maadui zikapiga,
Kisha zikawasaga,
Kama ngano kwa kijaa.

559

Bomu chini zilishuka,
Kama mvua ya masika,
Bomu hazikupunguka,
Zilizidi kila saa.

560

Nilipofika 'taacha,
Niwape nyingine ncha,
Ambayo ikijificha,
Habari itapungua.

561

Natumai mwakumbuka,
Waingereza kutamka,
Kwa Wafaransa kuweka,
Ahadi kuwakomboo.

562

Waliopewa ahadi,
Kufanyiwa jitihadi,
Uhuru wao urudi,
Hila zao 'tawambia.

563

Hila walitengeneza,
Kuwahini Waingereza,
Ahadi kutekeleza,
Wafaransa sikia.

564

Kwanza wao walihini,
Kwa kumpa Jermani,
Kila zana ya thamani,
Adui walimwachia.

565

Walijitia shughuli,
Kwa hiana ya Lavali,
Kumzuia De Gaulli,
Ufaransa kukomboa.

566

Walipitisha hukumu,
De Gaulle kumdhulumu,
Wala kwao si hasimu,
Ila aliwatetea.

567

Hukumu waliifunga,
Ya De Gaulle kumnyonga,
Sababu alijitenga,
Vichy hakisikia.

568

Ndivyo ilivyo dunia,
Taabu inapotokea,
Marafiki hukimbia,
Haba wanaobakia.

569

Wakumbukao ahadi,
Taabu ibishapo hodi,
Ni wachache kwa idadi,
Watu katika dunia.

570

Mpenzi huwa mwasi,
Dhiki ishikapo kasi,
Au huwa mtesi,
Mara hukugeukia.

571

Mfuasi ni mtoro,
Uzukapo mgogoro,
Dunia ina kasoro,
Hupenda kufanya ria.

572

De Gaulle aliwajibu,
“Hukumu yenu taibu,
Dunia itahesabu,
Uhuru ukirejea.”

573

“Vichy sitaiheshimu,
Fanyeni kila hukumu,
Muwezayo kuhukumu,
Kunyongwa au kuchomwa.”

574

“Uhuru jambo muhimu,
Kulitetea kwa damu,
Naona kama karamu,
Hukumu ya kuuawa.”

575

“Nitakabili uchungu,
Nitete nchi yangu,
Kwa msaada wa Mungu,
Uhuru utarejea.”

576

“Ninaona siyo utu,
Kuwateroka wenzetu,
Walioweka kwetu,
Ahadi kutukomboa.”

577

“Ninaona si kanuni,
Mimi kwenda ufichoni,
Niwatupe hatarini,
Marafiki mashujaa.”

578

“Mateso yakinikuta,
Kwa vita hivi kuteta,
Si yamkini kujuta,
Ila nitafurahiwa.”

579

“Uhuru siuachii,
Nitakwenda kwa adui,
Moyo haunitulii,
Uhuru ukipotea.”

580

“Roho haikubali,
Naona sistahili,
Kukitafuta kivuli,
Vita nikavikimbia.”

581

“Kila niwapo mzima,
Moyo wangu ukipuma,
Kupigana sitakoma,
Ila kwa moyo kutua.”

582

“Dunia itahesabu,
Nani mwenye kuharibu,
Na majazi ya aibu,
Ni tuzo ya waasia.”

583

“Watalipwa shukurani,
Za aibu duniani,
Majina yazame chini,
Kama hawakuzaliwa.”

584

“Wateteo uhuru
Aibu haiwadhuru,
Watu watawashukuru,
Daima watasifiwa.”

585

“Watu watawahutubu,
Kwa kuwatetea taabu,
Mungu awape thawabu,
Na zawadi maridhawa.”

586

“Majina yao hayafi.
Wala hayawi ghafi,
Yatazidi kuwa safi,
Milele kukumbukiwa.”

587

“Kuuawa nimekiri,
Mwashindapo Wahuri,
Lakini sifikiri,
Jambo hili litakuwa.”

588

“Moyoni nina hakika,
Hili halitatendeka,
Na iwapo litazuka,
Nimekiri kuuawa.”

589

Juu ya mashaka hayo,
Kila siku yazidiyo,
Hawakuvunjika moyo,
Waingereza mara moja.

590

Kuacha ahadi yao,
Neno hili mwiko wao,
Tena siyo mila yao,
Ahadi kuikimbia.

591

Ahadi waiwekapo,
Nao hudumia papo,
Ahadi kwao kiapo,
Kuivunja ni hatia.

592

Daima hutekeleza,
Ahadi Waingereza,
Hawapendi kulipuzi,
Neno lao la heshima.

593

Kwayo walivipeleka,
Vita Madagaska,
Kuzuia kukiteka,
Kisiwa Wajapania.

594

Na Madagascar hasa,
Ni milki ya Wafaransa,
Vichy ikatenda visa,
Kuteta na Wahuria.

595

Kufika Madagaska,
Waingereza walitamka,
"Tumekuja kwa haraka,
Kukitetea kisiwa."

596

"Tumesikia habari,
Kuwa mnayo hatari,
Kwayo twawapa shauri,
Kisiwa kutuachia."

597

"Jambo hili mkitaka,
Kisiwa tutakishika,
Vita vikimalizika,
Lazima kurudishiwa."

598

"Mapatano yakitimu,
Pasipo kumwaga damu,
Sisi tutayaheshimu,
Na haja mtaridhiwa."

599

"Hamtapata hasara,
Mtalipwa biashara,
Kila jambo la tijara,
Lazima mtagawiwa."

600

Jibu walilopata,
Ni kutangaziwa vita,
Waingereza wakateta,
Kisiwa wakachukua.

601

Muda wa miaka miwili,
Ulipotimu kamili,
Waziri wa Serikali,
Watu aliwanadia.

602

Siku hiyo ya usemi,
Kwa hesabu ya Kirumi,
Mei tarehe kumi,
Mwaka wa Kimasihiya.

603

Mwaka wa elfu moja,
Kisha tisa mia taja,
Arobaini pamoja,
Mbili mwisho hutiwa.

604

Aliitoa kauli,
Ikafika hata mbali,
Siku ya Jumapili,
Baada jua kutua.

605

Alisema kwa radio,
Kwa ufasaha na kituo,
Maneno yakenda mbio,
Pembe zote za dunia.

606

Walitega masikio,
Kusikiliza mlio,
Siku ya hotuba hiyo,
Watu katika dunia.

607

Kwanza alianza nyuma,
Maneno yake kusema,
Akavuta kutazama,
Mambo yaliyotokea.

608

Katamka Churchill,
"Sasa miaka miwili,
Nimekuwa wa awali,
Waziri Britania."

609

"Kwayo wajibu wangu,
Kusema nanyi wenzangu,
Wahuri wa ulimwengu,
Pande zote za dunia."

610

"Tangu miaka miwili,
Maadui kwa ukali,
Wamefanya ukatili,
Nchi nyingi za Ulaya."

611

"Holland na Belgiji,
Zilionywa mauaji,
Zikapita kama maji,
Ghaffa zilipotea."

612

"Kwa ukatili wa nyama,
Nchi hazikusimama,
Mara moja zilizama,
Pasipo kuhurumiwa."

613

“Zilifanywa shambulizi,
Katika nchi za wazi,
Jumla mengi majoji,
Watu waliouawa.”

614

“Kama kushuka gharika,
Ufaransa ilitoka,
Bordeaux ikaitika,
Nayo ikajitolea.”

615

“Mussolini aliona,
Nguvu hatuna tena,
Akataka kupigana,
Sisi na Waitalia.”

616

“Waliposhindwa wenzetu,
Tulibaki peke yetu,
Katika kisiwa chetu,
Adui kumzuia.”

617

“Majeshi ya Dunkirk,
Watu waliobaki,
Kurudi kisiwa hiki,
Robo milioni moja.”

618

“Watu robo milioni,
Bila zana mikononi,
Walirudi kisiwani,
Wengine walipotea.”

619

“Kwa kudhani tumekwisha,
Maadui walitisha,
Wakataka kuvivusha,
Vita katika kisiwa.”

620

“Tuliwekewa zuio,
Huko Mediterreneo,
Ilifungwa njia hiyo,
Kupita tulizuiwa.”

621

“Ilibaki njia ndefu,
Yenye hatari na hofu,
Kupeleka masarufu,
Na zana za kutumia.”

622

“Hiyo ndiyo nafasi,
Tuliyopata sisi,
Rafiki yetu Smuts,
Zamu aliangalia.”

623

“Majeshi ya askari,
Ya Sudan na Misri,
Bila silaha nzuri,
Kuvunjwa yalihofia.”

624

“Adui yetu mpevu,
Akazidisha nguvu,
Tukakabili maovu,
Yake na ya Italia.”

625

“Hata wetu marafiki,
Moyoni walisadiki,
Kuwa hatuokoki,
Mwisho umetufikia.”

626

“Walikata tumaini,
Marafiki wakadhani,
Atashinda Jermani,
Sisi tutaangamia.”

627

“Kushindwa hatukukiri,
Tukajiweka tayari,
Tufe katika shari,
Hapa katika kisiwa.”

628

“Tulinuia kushinda,
Tufe kwa kujilinda,
Kila mtu akapenda,
Maadui kuzuia.”

629

“Kuanguka kupigana,
Ndivyo tulivyopatana,
Mara tukaungana,
Pasipo hofu kutia.”

630

“Ilikuwa saa bora,
Hiyo katika fikara,
Itatajwa kila mara,
Katika historia.”

631

“Tulikitoa kicheko,
Kikafika hata huko,
Maadui wakaako,
Wote wakasikia.”

632

“Maneno tulitamka,
Pasipo kutikisika,
Kwa upepo yakafika,
Mbali yakasikiwa.”

633

“Wote tulijitahidi,
Kuzuia uhasidi,
Kila siku ikazidi,
Nguvu katika kisiwa.”

634

“Tulitimiza wajibu,
Ingawa katika taabu,
Hatukupata aibu,
Mungu katuhurumia.”

635

“Hitler bila siasa,
Amefanyiza makosa,
Yaliyo makubwa hasa,
Kwa kuchokoza Russia.”

636

“Zaidi ya mwaka jana,
Sasa wana nguvu sana,
Warussia kwa kupigana,
Wamekwisha kuzoea.”

637

“Majeshi ya nchi ile,
Sasa yana zana tele,
Hitler akenda kule,
Nyuma atarejea.”

638

“Na sisi twamwandama,
Tunamfuata nyuma,
Hitler hana salama,
Njia ya kujiokoa.”

639

“Nyuma yake twamsaka,
Pamoja na Amerika,
Wote tumeunganika,
Hitler kumzuia.”

640

“Ulaya inalalama,
Kwa maovu na dhuluma,
Tena inaunguruma,
Kuasi inanuia.”

641

“Ulaya yaunguruma,
Kama simba mla nyama,
Yanua kusimama,
Hitler kumrukia.”

642

“Inanuia kuasi,
Inapopata nafasi,
Ili ilipe kisasi,
Hitler amekamiwa.”

643

“Nchi zote za Ulaya,
Kwa njaa zinaumia,
Watu wanalichukia,
Jina *Nazi* kusikia.”

644

“Wanataka litoweke,
Dunia isitamke,
Jina hili lifutike,
Kama halikutokea.”

645

“Ndege za Waingereza,
Kazi zimekwisha anza,
Amerika imekaza,
Nayo kushambulia.

646

“Twapiga bomu Udachi,
Kila siku hatuachi,
Maana ndiyo nchi,
Ya uovu wa dunia.”

647

“Wadachi wanalalama,
Kuwa hatuna huruma,
Wamesahau dhuluma,
Majuto yanawajia.”

648

“Wadachi hawakumbuki,
Walipomwaga fataki,
Wakaua halaiki,
Watoto na wake pia.”

649

“Waliua maraia,
Watu wasio hatia,
Sasa Wadachi walialia,
Huruma wahitajia.”

650

“Sisi letu shambulio,
Si kwa maraia wao,
Kama watakwenda zao,
Mashamba kujikalia.”

651

“Maraia wa Jermani,
Wakitoka viwandani,
Watakuwa nusurani,
Bomu hazitawaua.”

652

“Tulisikia zamani,
Matisho ya Jermani,
Kuleta eropleni,
Kukizamisha kisiwa.”

653

“Zamani walijisifu,
Ndege zao maelfu,
Waweza kuzisarifu,
Watushinde mara moja.”

654

“Hitler alidhani,
Anazo eropleni,
Nyingi zisizo kifani,
Katika yote dunia.”

655

“Hitler alitamani,
Kutufuta kisiwani,
Mungu akamlani,
Hili hakumjalialia.”

656

“Hili alilitamka,
Kuwa litatendeka,
Na ahadi akaweka,
Dua haikupokewa.”

657

“Ahadi aliyonena,
Hitler alikazana,
Liweze kupatikana,
Jambo alilonuia.”

658

“Kila toni ya bomu,
Tupigayo wadhalimu,
Hitler aliazimu,
Kutupiga toni mia.”

659

“Hitler alivyowaza,
Mungu hakumwongoza,
Ila alipatiliza,
Mambo kumgeukia.”

660

“Warussia wanalaumu,
Wadachi wameazimu,
Kutia upepo sumu,
Ili wateke Russia.”

661

"Kama atafanya hamu,
Hitler kutia sumu,
Sisi itatulazimu,
Kumlipa maridhawa."

662

"Tutatumia madege,
Upepo tuuvuruge,
Sumu nyingi tumwage,
Ijae katika hewa."

663

"Hewa haitavutika,
Sumu itatawanyika,
Tutamwaga kwa tabaka,
Mara tukianziwa."

664

"Tukitendwa jambo hili,
Sisi hatutakubali,
Tutamwaga sumu kali,
Kama tunavyojaliwa."

665

"Rafiki zetu wa kweli,
Wakionywa ukatili,
Sisi hatutakubali,
Lazima kuwalipia."

666

"Kifo cha Wajapani,
Kutabiri sitamani,
Lakini nina yakini,
Kuwa wataangamia."

667

"Nguvu zetu baharini,
Zitashika Wajapani,
Nguvu zetu hewani,
Chini zitawalemea."

668

Hotuba kumalizika,
Watu walifurahika,
Maneno wakatamka,
Hotuba kuisifia.

669

Hotuba hii nadhifu,
Iitoa watu hofu,
Kushindwa kwa wapotofu,
Watu walitazamia.

670

Tumaini ilitia,
Hotuba hii sikia,
Wahuri wakawania,
Kuomba kushambulia.

671

Kwa vile kujiapisha,
Baridi ilipokwisha,
Hitler alirudisha,
Vita tena Russia.

672

Safari hii ya pili,
Alianza Sevastopol,
Wakapigana kwa ukali,
Wadachi na Warussia.

673

Yalishika mapigano,
Makali bila mfano,
Kila Wadachi watano,
Kwa mmoja Mrussia.

674

Idadi hii si basi,
Walizidiwa Warussi,
Kwa kupigwa marisasi,
Juu katika hewa.

675

Lakini hawa Warussi,
Walituliza nafsi,
Wakazipiga risasi,
Hata zikawaishia.

676

Yalizuka mapigano,
Ya mkono kwa mkono,
Maadui wakafa mno,
Hesabu nitawambia.

677

Hasara ya Jermani,
Elfu arobaini,
Watu wao wa vitani,
Sevastopol sikia.

678

Warussia katika safu,
Hasara zao haffu,
Ishirini elfu,
Ndiyo waliopotea.

679

Hapa Sevastopol,
Waliuziwa ghali,
Kila Wadachi wawili,
Kwa Mrussia mmoja.

680

Wadachi mwendo wao,
Wafanyapo shambulio,
Ni kupata watakayo,
Japo wakifa pia.

681

Vita vya muda mrefu,
Hili ni kosa dhaifu,
Maana yake halafu,
Nguvu huwaishia.

682

Warussia huyakinisha,
Vita wakipiganisha,
Kwanza adui kufisha,
Kisha humpisha njia.

683

Nguvu zao hubakisha,
Hawapendi zote kwisha,
Adui zake zikisha,
Warussia humrudia.

684

Tena huko Kharkov,
Zilifufuliwa kovu,
Vikashikwa kwa ukavu,
Vita viliporejea.

685

Kwa mzinga sampali,
Mmoja siyo miwili,
Uliua wakatili,
Wadachi wengi sikia.

686

Mzinga ulihasiri,
Ukaua askari,
Wengi katika malori,
Elfu tatu pamoja.

687

Watu thelathini mia,
Mzinga uliwaua,
Kufumba na kufumbua,
Kifo kiliwatokea.

688

Mzinga huo mkali,
Wadachi uliwadhili,
Ukawatia shughuli,
Kwa hasara kuzidia.

689

Tena hasara kamili,
Ni mizinga miwili,
Ilivunjiliwa mbali,
Kwa mzinga mmoja.

690

Kwa ukali walirudi,
Wadachi Leningrad,
Wakafanya jitihadi,
Warussia huko pia.

691

Walituliza fuadi,
Kila mtu hana budi,
Ila kufanya mradi,
Mapigo kuyazuia.

692

Warussia wana kanuni,
Maarufu ya zamani,
Waingiapo vitani,
Adui humuhadaa.

693

Humuhadaa mtesi,
Anayekwenda kwa kasi,
Kwa kumpa wasiwasi,
Na kumpoteza njia.

694

Mara wakimbaini,
Adui yao machoni,
Humvuta misituni,
Nguvu kumpunguzia.

695

Tena hupinga mitoni,
Kwa vikosi vivukoni,
Wakapigana majini,
Hata katika maziwa.

696

Vikosi vyao huhizi,
Kama mfano wa uzi,
Wa buibui kwa nzi,
Adui akitokea.

697

Basi kila hatua,
Japo waliendelea,
Wadachi waliumia,
Wengi wakaangamia.

698

Vita vilifanya nyuga,
Donetz-Dona na Volga,
Sababu waliitega,
Mito hii Warussia.

699

Kila wavukapo mto,
Hupewa hasara nzito,
Inapopimwa na pato,
Hasara huzidia.

700

Kila penye misitu,
Majeshi ya watukutu,
Yalikutana na watu,
Tayari kuyazuia.

701

Wadachi wakenda mbele,
Na Warussia vilevile,
Wenda nyuma polepole,
Maadui wakiua.

702

Kila penye maziwa,
Wadachi waliuawa,
Bali hawakutambua,
Hasara walizotiwa.

703

Walizidisha safu,
Wakenda kama siafu,
Ili kuyatia hofu,
Majeshi ya Warussia.

704

Wadachi waliwaleta,
Vijana katika vita,
Ambao hawajapata,
Mwisho wao wa kukua.

705

Umri wao wapata,
Miaka kumi na sita,
Hao walikuja teta,
Na nyuma wanaliliwa.

706

Nyuma waliliwa,
Kwamba wataangamia,
Kila endaye Russia,
Udachi hatarejea.

707

Majeshi ya watukutu,
Mamilioni ya watu,
Na bunduki kama mwitu,
Yalizidi kusogea.

708

Vita vilienea,
Kushoto hata kulia,
Wadachi wakisogea,
Warussia wanazuia.

709

Mji wa chuma cha pua,
Stalingrad Kirussia,
Warussia walinuia,
Kuulinda kila njia.

710

Hapa walipigana,
Usiku hata mchana,
Vita visivyo namna,
Katika historia.

711

Usiku ulitoweka,
Kwa moto ulivyowaka,
Mchana ukazimika,
Kwa moshi juu kupaa.

712

Vilishika kila pembe,
Vita halambe halumbe,
Kwa ukali kama wembe,
Namna vilivyokuwa.

713

Katika kitisho hicho,
Walichopambana nacho,
Hawakupepesa macho,
Warussia walizuia.

714

Vita hapa vilisiri,
Kwa kuzuiwa hodari,
Warussia hawakukiri,
Mji huu kuachia.

715

Walizuia imara,
Katika mabarabara,
Wadachi ukawakera,
Ushujaa wa Russia.

716

Kuzuiwa kila mara,
Wadachi kuliwakera,
Wakaazimu hasara,
Mji wote kuutia.

717

Von Bock alisema,
"Hitler amenituma,
Niuteke kwa lazima,
Mji wa chuma cha pua."

718

"Nikishindwa ni lawama,
Jina langu litazama,
Nitavunjiwa heshima,
Kazini kuuzuliwa."

719

"Aibu ya mwaka jana,
Kama itarudi tena,
Itakuwa kubwa sana,
Sitaweza vumilia."

720

"Mwaka jana mwajua,
Hitler alichukiwa,
Kwa kushindwa kuchukua,
Moscow kwa Warussia."

721

"Hitler amenitaka,
Mji huu kuuteka,
Majeshi yake kuweka,
Baridi ikiwadiwa."

722

"Jambo hili alitaka,
Lakini naona shaka,
Kuwa taabu kufanyika,
Shida kufanikiwa."

723

"Dalili zake naona,
Kuuteka taabu sana,
Lakini hapana maana,
Bwana hili kumwambia."

724

"Dalili nikitazama,
Ninaona tumekwama,
Bali hili sitasema,
Bwana asije chukiwa."

725

"Hitler akiambiwa,
Uhaini tazuliwa,
Na hili sipendi kuwa,
Nikajitoa murua."

726

"Sina haja kughairi,
Wala kufanya jeuri,
Nitatimiza amri,
Bwana aliyonambia."

727

Kawambia wanaume,
"Nataka mfanye shime,
Mji huu uzame,
Kwa mizinga kutumia."

728

"Mizinga yote mikali,
Naitaka tasihili,
Ipige kila mahali,"
Amri akaitoa.

729

"Nataka kila mzinga,
Na ndege katika anga,
Zipige panapokinga,"
Von Bock kawambia.

730

Ulibadilika hali,
Mji kila mahali,
Mizinga elfu mbili,
Wadachi walitumia.

731

Kwa kupigwa makombora,
Mfulizo kila mara,
Uliharibika sura,
Mji ukatishia.

732

Yalizidi mapigano,
Siku mbili kwa mfano,
Wadachi elfu tano,
Hapa waliuawa.

733

Hasara ya mauano,
Ilikuwa kubwa mno,
Elfu kumi na tano,
Wadachi kwa juma moja.

734

Hasara za Soviet,
Majeruhi na maiti,
Jumlaye si katiti,
Mahali hapa sikia.

735

Kwa ushahidi sahihi,
Warussia walifurahi,
Kufa na kujeruhi,
Kwa ari ya uhuria.

736

Walionyesha dhahiri,
Thamani yake uhuri,
Kuwa jambo la ari,
Viumbe kupigania.

737

Japo walikufa wengi,
Walifanyiza msingi,
Uliopendwa na wengi,
Watu wa Russia.

738

Misingi yote ya hadhi,
Hapa katika ardhi,
Mmojawapo faradhi,
Kufa kwa kujitetea.

739

Majeshi ya Timoshenko,
Hayakuhofu vituko,
Kati ya mabomoko,
Mji yaliuzuia.

740

Timoshenko ni mtesi,
Maarufu wa Warussi,
Hofu na wasiwasi,
Vitu hivi hakujua.

741

Dunia nzima husifu,
Timoshenko hana hofu,
Ya jeraha wala ufu,
Vitani akitokea.

742

Timoshenko kwa adui,
Alikuwa kama chui,
Ambaye hofu hajui,
Ghadhabu ikimjia.

743

"Nataka kila shujaa ,
Mji huu kuzuia,
Bila kurudi hatua,"
Timoshenko kausia.

744

"Ninataka tupigane,
Dunia nzima ione,
Mpaka mwisho wa tone,
La damu ya Warussia."

745

"Hiyo ndiyo sadaka,
Kwenu ninayotaka,
Na kama itafanyika,
Adui atalemewa."

746

"Tumekwisha jiapisha,
Kama sisi hatukwisha,
Mapigo tutarudisha,"
Timoshenko kajibiwa.

747

"Japo tukibaki haba,
Hatutavunja haiba,
Moyoni tuna mahaba,
Ya sadaka kujitoa."

748

Shambulio lilidumu,
Siku nyingi zikatimu,
Ikamiminika damu,
Ardhi ikaenea.

749

Damu ilikwenda mbio,
Kama maji yashukayo,
Kwa vita vya mji huo,
Jinsi vilivyokawia.

750

Wadachi waliazimu,
Shambulio maalum,
Mradi haukutimu,
Bidii zikapotea.

751

Bidii zilipotea,
Kama mto kuzuiwa,
Maji yasipate njia,
Baharini kuingia.

752

Majeshi ya Axis,
Yalikwenda Caucasus,
Yakawakuta Warussi,
Wamekwisha jiandaa.

753

Warussia waliwakuta,
Tayari kufanya vita,
Kwa kuzuia mafuta,
Adui kuyafikia.

754

Caucasus ina jina,
Tena ndiyo hazina,
Ya mafuta mengi sana,
Huko katika Russia.

755

Mafuta kila namna,
Hapa yalipatikana,
Yenye manufaa sana,
Kwa vita kupigania.

756

Visima vinavyotoa,
Mafuta ni saba mia,
Na juu vimezidia,
Vinapata nusu mia.

757

Kwa kushindwa wachotaji,
Yaenda kwa mifereji,
Kama mfano wa maji,
Kila dakika hujaa.

758

Ilikuwa haifai,
Kumwachia adui,
Mafuta hayo uhai,
Na nguvu ya Warussia.

759

Warussia waliyalinda,
Kama chui na makinda,
Kidogo hawakupenda,
Mafuta kuchukuliwa.

760

Kiu iliwakamata,
Axis ya mafuta,
Wakachokoza matata,
Chui akawarukia.

761

Alirukiwa adui,
Kwa thamani ya uhai,
Ikawa hapana rai,
Ila nyuma kurejea.

762

Adui karudi nyuma,
Na kiu inamuuma,
Hakufikia visima,
Alivyovikusudia.

763

Alirudi akihema,
Na vidole kujiuma,
Kila akitazama,
Hasara alizotiwa.

764

Vita vya kila mpaka,
Hapa vimezohalika,
Kwa hivi tutaondoka,
Russia twende India.

765

Sasa hapa inapasa,
Niwaeleze kabisa,
Jambo lisilo siasa,
Ili mpate lijua.

766

Jambo moja Bara Hindi,
Lilighilibu Wahindi,
Kuacha kando sipendi,
Wajibu hapa kutiwa.

767

Kiongozi wa Wahindi,
Jina Mahatma Gandhi,
Ilitokea hapendi,
Ushindi wa uhuria.

768

Huyo Gandhi sikiliza,
Alipendwa Uingereza,
Watu wakamtukuza,
Mfalme na raia.

769

Alisifiwa elimu,
Kuwa mtu taalamu,
Dola ikaazimu,
Kuipa 'huru India.

770

Kumbe aliwaghilibu,
Awatupe penye taabu,
Siku ya majaribu,
Gandhi kabadili nia.

771

Alitisha Waingereza,
Kuwa atawafukuza,
Hili lilipotokeza,
Dunia ilishangaa.

772

Gandhi alitamani,
Ushindi wa Jermani,
Italia na Japani,
Ukamilike India.

773

Alikuwa na madai,
Kwa Waingereza adai,
Akadhani maadui,
Waweza msaidia.

774

Lakini hii si rai,
Bure alijilaghai,
Ushindi wa maadui,
Ungelipoteza India.

775

Kuondoka Waingereza,
Gandhi asingeweza,
Baadhi kuzituliza,
Zote katika India.

776

Zingepatana baadhi,
Waingereza wangeridhi,
Madai yake kukidhi,
Bila kufanya udhia.

777

Gandhi alinasihiwa,
Jambo hili kwanza kuwa,
Lakini hakuridhia,
Kusikiza mara moja.

778

Labda Mabaniani,
Wangeonyesha amani,
Kwa kuwekwa Baniani,
Kuitawala India.

779

Lakini kwa Islamu,
Jambo hili lingetimui,
Kwao lingekuwa gumu,
Kuweza kuvumilia.

780

Baniani kakubali,
Kuwa bwana wa awali,
Katika cheo cha pili,
Islamu kakataa.

781

Nchi ya baadhi mbili,
Na dini mbalimbali,
Inataka serikali,
Ya kuweka watu sawa.

782

Hili alipoambiwa,
Gandhi alilichukia,
Akazitafuta njia,
Za kufanya maasia.

783

Jamani makeni kisa,
Cha uchache wa siasa,
Huwaje rafiki hasa,
Kumfanyia hadaa!

784

Huwaje mustaarabu,
Na mweledi wa kitabu,
Kuacha nyuma aibu,
Vitabuni ikatiwa.

785

Kwa kuwahini Wahuri,
Bure alijihasiri,
Akavunjiwa kadiri,
Kifungoni akatiwa.

786

Hii ndiyo zawadi,
Na jambo linalobidi,
Mtu hiana hasidi,
Halali kumzuia.

787

Uhaini wa rafiki,
Ni jeraha lenye dhiki,
Linashinda la mkuki,
Wa adui shujaa.

788

Mtu wa pili Nehru,
Alinuia kudhuru,
Sheria ikaamuru,
Kifungoni kuingia.

789

Hapa tugeuze mwendo,
India tuache kando,
Tukatazame matendo,
Yaliyokuwa Libya.

790

Majeshi ya marafiki,
Chini ya Auchinleck,
Yalifika Tobruk,
Bahati ikawa mbaya.

791

Palitokea jahili,
Upande wa wakatili,
Jina aitwa Rommel,
Bahati akapendua.

792

Rommel ni mtukutu,
Alisifiwa na watu,
Inapata mara tatu,
Wahuri kuwahadaa.

793

Na Wahuri mara mbili,
Walimshinda Rommel,
Lakini hakukubali,
Kuacha kujaribia.

794

Alisifiwa upeo,
Uhodari mtu huyo,
Katika mashambulio,
Ni stadi na shujaa.

795

Ana hila za kuepa,
Mahali hapa na hapa,
Mtulivu hana pupa,
Moyoni hana fadhaa.

796

Huepa kama mwanzi,
Tofani ikibarizi,
Akaanza shambulizi,
Tofani ikitulia.

797

Tena ana ustadi,
Na moyo wa jitihadi,
Akifukuzwa hurudi,
Mahali akinuia.

798

Kushindwa hakuhesabu,
Mtu huyo wa ajabu,
Huona kama thawabu,
Watu wakiangamia.

799

Wala hajui kutubu,
Anachekelea taabu,
Dunia humuhutubu,
Jemadari katimia.

800

Pete ikimzunguka,
Hakawii kuepuka,
Mara akinusurika,
Hurudi kushambulia.

801

Rommel na Auchinleck,
Waliteta Tobruk,
Majeshi ya Marafiki,
Mji yakauachia.

802

Wahuri waliokoka,
Kushikwa wote mateka,
Misri walipofika,
Rommel akazuiwa.

803

Hapa alifurukuta,
Kwenda mbele hakupata,
Kila alichokileta,
Hakikufaulu njia.

804

Wahuri walisimama,
Wakaacha kwenda nyuma,
Rommel hapa kakwama,
Werevu ukamwishia.

805

Rommel aliruka,
Kwa Hitler akafika,
Maombi akatamka,
"Nataka kusaidiwa."

806

"Mbele yangu iko shida,
Ninatoka msaada,
Nikikosa sina muda,
Fahamu nitazidiwa."

807

"Na watu katika safu,
Wapata kumi elfu,
Wamekuwa wapungufu,
Auchinleck kachukua."

808

"Hao amewashika,
Wamekuwa ni mateka,
Watu wengine nataka,
Upesi wende Libya."

809

"Isitoshe Waingereza,
Huyu wamengeza,
Makusudi kuongeza,
Uzito kutulemea."

810

Hitler alimjibu,
"Msaada una taabu,
Kwa sababu merikebu,
Hazina pa kupitia."

811

"Mediterraneo fahamu,
Yuko Cunningham,
Daima ashika zamu,
Bahari kaizuia."

812

"Bahari nzima aranda,
Vyombo vyetu kuvidunda,
Kila chombo kikienda,
Taabu sana kurejea."

813

"Na kisiwa cha Malta,
Mediterraneo chateta,
Vyombo vyetu vikipita,
Kisiwa kinazuia."

814

"Kisiwa kimesifiwa,
Kwa sisi kutuzuia,
Na nishani kimepewa,
Nadhani umesikia."

815

"Kisiwa kinachoteta,
Kidogo kama nukta,
Njia ya kukifuta,
Bado haijanijia."

816

"Na mbele yetu Warussi,
Wametushika kwa kasi,
Naona sina nafasi,
Sasa kukusaidia."

817

"Lakini nakuahidi,
Libya ukisha rudi,
Nitufanya jitihadi,
Parachuti kukujia."

818

Akaja Alexander,
Vita vipya akaunda,
Wakati alipokwenda,
Auchinleck India.

819

Huyo Alexander,
Kama simba muwinda,
Adui akimganda,
Shida kupata wasaa.

820

Ni shujaa hana waa,
Anaelewa hadaa,
Akitegwa huambaa,
Mitego akanasua.

821

Alipokwisha kabili,
Alexander awali,
Pakaja mtu wa pili,
Montgomery sikia.

822

Montgomery shujaa,
Sifa zimetapakaa,
Kaja kuzuia baa,
La adui Misria.

823

Tena cheo cha tatu,
Kilishikwa na mtu,
Ambaye hahofu kitu,
Jina mtaambiwa.

824

Jina lake Lumsden,
Shujaa mwenye makini,
Maarifa ya vitani,
Mengi yanamwelea.

825

Lumsden kadhibiti,
Cheo kile cha Gott,
Aliyepata mauti,
Vitani kwa ushujaa.

826

Gott alipigana,
Akafa kiungwana,
Maadui wengi sana,
Na yeye aliwaua.

827

Alikufa na umati,
Yeye akawa kati,
Kila upande maiti,
Watu aliwaua.

828

Basi majemadari,
Wenye ari na dhamiri,
Wakaanzia Misri,
Rommel kumwondoa.

829

Ilitolewa kauli,
Na jemadari wa pili,
"Muharibuni Rommel,
Na majeshiye pamoja."

830

"Nataka huyo Rommel,
Afanyiwe vita kali,
Tena aonywe ukweli,
Wa nguvu ya Wahuria."

831

"Lazima kumsukuma,
Na kumfuata nyuma,
Asipate pa kuhema,
Mahali pa kupumua."

832

"Ninataka mtu huyo,
Aonyeshwe shambulio,
Nyuma arudi mbio,
Asijue pa kutua."

833

"Lazima tumwandame,
Upesi kama umeme,
Haya wanaume shime,"
Kawambia mashujaa.

834

Mashujaa kupulika,
Ari zao ziliwaka,
Wakajifunga haraka,
Kumkabili mdawa.

835

Walikuwa wana hamu,
Wakingojea utimu,
Wakati wa kuazimu,
Adui kumtokea.

836

Walitoka washabiki,
Askari wa bunduki,
Wakaandama tariki,
Rommel kumwendea.

837

Askari wa bunduki,
Waliondoa fataki,
Iliyotegwa kudhiki,
Majeshi ya Wahuria.

838

Hao walitangulia,
Mafundi wa kuondoa,
Mitego katika njia,
Adui aliyotia.

839

Mitego ni ya baruti,
Inayoleta mauti,
Na kupoteza umati,
Kama hukuitambua.

840

Nyuma yakenda mafaru,
Na majeshi ya uhuru,
Madege yanayodhuru,
Yakawa katika hewa.

841

Adul walimsonga,
Chini na katika anga,
Akukosa pa kukinga,
Tobruk kakimbia.

842

Jeshi la Marafiki,
Lilishika Tobruk,
Na wingi wa halaiki,
Muteka walizingiwa.

843

Hupa palikufa watu,
Wengi wa watukutu,
Hii ni mara ya tatu,
Wahuri kupachukua.

844

Hasara zao Wahuri,
Zilikuwa za kadiri,
Chini tu ya urari,
Wa Wadachi na Waitalia.

845

Walisema hawatoki,
Axis Tobruk,
Ukakoma unafiki,
Kweli ilipotokea.

846

Zilizidi shambulizi,
Kuelekea Benghazi,
Bila kupana punzi,
Ya dakika wala saa.

847

Benghazi ilishindika,
Wahuri wakashika,
Maadui wakatoka,
Kwa haraka na fadhaa.

848

Iifanywa vita kali,
Kuelekea Tripoli,
Kumtafuta Rommel,
Kila alipohamia.

849

Jeshi lake Rommel,
Lilionja dhiki kali,
Sababu kila mahali,
Mbio halikutulia.

850

Halikutua kuhema,
Wala kutazama nyuma,
Kila liliposimama,
Mara liliondolewa.

851

Katika mwezi Novemba,
Mwaka wa nne kugomba,
Watu waliojigamba,
Vita viliwakulia.

852

Ndiyo mwezi wa mashaka,
Axis kuwafika,
Mwezi wataukumbuka,
Katika historia.

853

Mambo yaliyotendeka,
Daima watakumbuka,
Moyoni hayatatoka,
Na kuzidi kujutia.

854

Ndiyo mwezi wa feli,
Ulionya dalili,
Kuwa mwisho wakatili,
Vita vitawapotea.

855

Dalili za huu mwezi,
Zilikuwa wazi wazi,
Kuwa zitawahizi,
Maadui wote pia.

856

Sana walibabaika,
Maneno ya kutamka,
Wakafikiri mashaka,
Ushindi ukipoteta.

857

Maneno walikariri
Ya Churchill Waziri,
Kuwa utadhihiri,
Ushindi wa uhuria.

858

Simba katika bahari,
Alileta manowari,
Na meli za askari,
Morocco na Tunisia.

859

Meli na manowari,
Kupita bila hatari,
Kulibukua siri,
Ya Wadachi kuzidiwa.

860

Merikebu mia tano,
Ndani zilijaa mno,
Mafundi wa mapigano,
Wakashuka Tunisia.

861

Morocco na Algiers,
Walishuka watesi,
Wanaopiga risasi,
Kwa shabaha za kuua.

862

Mia tatu na hamsini,
Manowari baharini,
Zilikuwa safarini,
Kuwaleta watu hawa.

863

Watu hawa kufika,
Kasikazini Afrika,
Koloni wakazishika,
Za Wafaransa jamia.

864

Kushikwa hizo koloni,
Ni kama pigo tumboni,
Wadachi na Taliani,
Vita vikawakulia.

865

Vita vilitawanyika,
Kuma moto wa nyika,
Adui akasumbuka,
Kila alipotokewa.

866

Vita vya pande tatu,
Walionywa watukutu,
Wakakamatwa watu,
Wengine wakauawa.

867

Hapa nitazunguka,
Ili nipate andika,
Zana za Waamerika,
Katika mwaka mmoja.

868

Desemba tarehe sita,
Mwaka wa pili wa vita,
Wa Amerika kuteta,
Hotuba ilitolewa.

869

Alisema Roosevelt,
Akawambia umati,
Zana zote madhubuti,
Kwa majina kuteua.

870

Risasi na bunduki,
Hivyo viliachwa baki,
Kwani havihesabiki,
Kutajwa tamko moja.

871

Aliteua majina,
Ya zana zenye maana,
Akasema kwa bayana,
Watu kuwahesabia.

872

“Arobaini na tisa,
Elfu bila makosa,
Ni eropleni hasa,
Undo la mwaka mmoja.”

873

“Tena undo la pili,
Ni thelathini na mbili,
Elfu tupu kamili,
Mafaru ya chuma pua.”

874

“Na merikebu kwa toni,
Mwaka wetu wa mwanzoni,
Kama nane milioni,
Elfu zimezidia.”

875

“Zaidi ni mia mbili,
Elfu toni kamili,
Za manowari na meli,
Amerika imetoa.”

876

“Zana ya nne nadhifu,
Ni mizinga maarufu,
Kumi na saba elfu,
Imekwisha kutolewa.”

877

“Watu katika viwanda,
Zana waliounda,
Jumlaye ilipanda,
Si kama ilipungua.”

878

“Tangu saba milioni,
Idadi yao mwanzoni,
Wakazidi hesabuni,
Watu kumi milioni jua.”

879

“Na mia tano elfu,
Wakaja tena halafu,
Kuunda na kusarifu,
Zana za kupigania.”

880

“Katika mwaka ujao,
Watu jumla yao,
Itazidi mbio mbio,
Kwa milioni tano sikia.”

881

“Jumla yote gharama,
Katika mwaka mzima,
Ya zana zote za chuma,
Pauni tawatajia.”

882

“Idadi yake pauni,
Kumi na tano milioni,
Gharama ya viwandani,
Zana kutengenezea.”

883

“Haya ni matayarisho,
Msiseme ndiyo mwisho,
Tutafanya mazidisho,
Ya zana kuziandaa.”

884

“Tutakazana zaidi,
Kukutanisha idadi,
Ya zana zinazobidi,
Mungu akitujalia.”

885

“Tutafanya kila hali,
Kukusanya zana kali,
Kushindwa iwe muhali,
Dhihaka au ruia.”

886

“Kama tulivyoungana,
Tutakutanisha zana,
Ili kusaidiana,”
Roosevelt akatua.

887

Hitler hotuba yake,
Kawambia watu wake,
Kuwa ajali yake,
Sasa inakaribia.

888

“Mwaka huu ukipita,
Tusipovishinda vita,
Lazima tutajuta,
Majuto ya kulemea.”

889

“Fungu letu litakuwa,
Majuto na kulaniwa,
Hayo tutayachukua,
Hata mwisho wa dunia.”

890

“Dalili ninazona,
Mbele yetu yaja laana,
Kama tusipokazana,
Kuwashinda Wahuria.”

891

“Usiku naota njozi,
Zionyazo waziwazi,
Kuwa yako majonzi,
Mbele yanatungojea.”

892

“Ninaelewa sahihi,
Kuwa watafurahi,
Kama tusipowawahi,
Watu wa Britania.”

893

“Sikufikiri vizuri,
Mwanzo wa hizi shari,
Kuwa hawa Wahuri,
Waweza kuvumilia.”

894

“Madege ya Waingereza,
Kuhesabu yatatiza,
Yakija hufunga kiza,
Japo likiwako jua.”

895

“Usiku katika anga,
Yakimulika mwanga,
Chembe ndogo za mchanga,
Huweza kuhesabiwa.”

896

“Madege ya Roosevelt,
Hewa yameidhibiti,
Huioni samawati,
Madege yakizagaa.”

897

“Mchana huwa usiku,
Madege yakija huku,
Moyoni mwangu nashuku,
Tutashindwa vibaya.”

898

“Usiku huwa mchana,
Pa kujificha hapana,
Mwanga mwingi sana,
Madege hayo hutoa.”

899

“Ningejua haya kwanza,
Vita nisingefanyiza,
Kuwaudhi Waingereza,
Kwa tamaa ya dunia.”

900

“Walishinda Kaizari,
Ninaelewa vizuri,
Lakini sikufikiri,
Na mimi nitazidiwa.”

901
"Maskini Chamberlain,
Waziri wa Britani,
Alinionya zamani,
Lakini sikusikia."

902
"Alinitaka radhi,
Kuwa nisiwaudhi,
Ikanizuzua hadhi,
Ya kutawala dunia."

903
"Najuta kufanya payo,
Kuchokoza watu hao,
Ningejua mwendo wao,
Vita visingetokea."

904
"Waingereza wakishinda,
Ninajua la kutenda,
Ugenini sitakwenda,
Udachi sitakimbia."

905
"Nashika tama kuwaza,
Hila ya kufanyiza,
Goering nakuuliza,
Njia ya kujiokoa."

906
"Kama unayo shaka,
Moyo wetu kuvunjika,
Wajibu ni kutamka,
Usifiche neno moja."

907
"Kama unayo tuhuma,
Ukinambia mapema,
Kwetu ingekuwa vyema,
Kuliko ukinyamaa."

908
"Dhihaka sasa iache,
Sema usinifiche,
Vita vinatoa cheche,
Kwa nguvu vinatujia."

909
"Mtangazaji habari,
Goebbels toa shauri,
La kuokoka hatari,
Na kushinda Wahuria."

910
"Kama unayo siri,
Tafadhali nihubiri,
Ili nipate fikiri,
Njia ya kutumia."

911
"Sema unavyofikiri,
Mabaya hata mazuri,
Nataka uyakariri,
Sitaki kuchaguliwa."

912
"Mambo yote ukisema,
Mimi nitayapima,
Na kutafuta hekima,
Ya kulizuia baa."

913
"Mkuu wa majasusi,
Himmler nakudadisi,
Moyo una wasiwasi,
Nimeota kuviziwa."

914
"Ninapolala naota,
Watu panga wamefuta,
Wanataka kunikata,
Usiku wanitishia."

915
"Watu hao si wageni,
Wajao usingizini,
Hizi ni ishara gani,
Himmler unazijua?"

916
"Ndoto ya pili fahamu,
Naota kutoka damu,
Tena nimeshika simu,
Nini inatabiria?"

917
"Hizi si ishara nzuri,
Naona hazina heri,
Uasi zinatabiri,
Hapa kwetu kutokea."

918
"Mkuu wa admeli,
Reader ninakusaili,
Mbona hufanyi akili,
Baharini twazidiwa?"

919
"Laiti wafanya ari,
Ya kumiliki bahari,
Tungewashinda Wahuri,
Kwa kuwafisha kwa njia."

920
"Wangepata upungufu,
Wa zana na masarufu,
Kama wangetiwa hofu,
Baharini Wahuria."

921
"Italia na Japani,
Wana tumaini gani,
Waziri wa nchi ngeni,
Ribentrop nambia."

922
"Nasikia Taliani,
Anatamani amani,
Habari hii yakini,
Kweli au hadaa?"

923
"Nilipendezwa na Tojo,
Alipoanzisha fujo,
Nikapiga kifijo,
Kuwa ataendelea."

924
"Habari imenifika,
Kuwa sasa Amerika,
Tojo inamtandika,
Pigo la kurudufia."

925

Goering alimjibu,
"Hatutapata aibu,
Ninao utaratibu,
Wa kushinda watu hawa."

926

"Moyo wetu kuvunjika,
Hilo halitatendeka,
Bwana ondoa shaka,
Usijitie fadhaa."

927

"Moyo wetu mgumu,
Na wote tumeazimu,
Kupigana kwa hamu,
Tangu vita kutokea."

928

"Moyo wetu na maungo,
Vigumu kama komango,
Kuvunjika ni uongo,
Hilo halitatokea."

929

"Tulifukuza kusudi,
Hapa kwetu Wayahudi,
Wasifanye uhasidi,
Uasi ukatokea."

930

"Tangu walipoondoka,
Udachi hapana shaka,
Nchi imesalimika,
Nadhani unaelewa."

931

"Katika vita vya bara,
Sisi ni watesi bora,
Usifanyize hasira,
Bwana zidi kungojea."

932

"Waingereza wakishuka,
Nchi tulizozishika,
Hapo yatafanyika,
Mambo ninayonua."

933

Goebbels alihubiri,
"Bwana zidi kusaburi,
Itaondoka hatari,
Jambo hili nalijua."

934

"Wahuri walihimili,
Mapigo yetu makali,
Na sisi tunayo hali,
Ya kuweza vumilia."

935

"Sisi tutanakili,
Kama walivyohimili,
Itabadilika hali,
Heri itatujia."

936

Himmler alisema,
"Bwana ondoa tuhuma,
Hatatokea daima,
Mtu wa kukuvizia."

937

"Mambo ya usingizini,
Usiyatie moyoni,
Hapana Mjermani,
Mwenye dhamiri mbaya."

938

"Naweza apa kiapo,
Mtu huyo hayupo,
Na ikiwa hapa yupo,
Mimi nitamgundua."

939

Reader kajibu maneno,
"Ninajitahidi mno,
Kufanyiza mapigano,
Baharini sijatua."

940

"Ninafanya ujasiri,
Njia zote za hatari,
Kuimiliki bahari,
Bado sijafanikiwa."

941

"Pengine twapigwa mno,
Lakini hilo si neno,
Ni mwendo wa mapigano,
Pande zote hutokea."

942

"Waingereza kwa kweli,
Baharini ni wakali,
Na mabwana wa awali,
Hapana asiyejua."

943

"Hii kwao ni asili,
Bado hawajabadili,
Bwana ukitaka kweli,
Wajibu hili kujua."

944

"Hila nyingi nafanyiza,
Sisi tuwe wa kwanza,
Hilo litatokeza,
Wakati ukiwadia."

945

Ribentrop kanena,
"Dalili sasa hapana,
Lakini mimi naona,
Ulegevu Italia."

946

"Laiti ingejikaza,
Kuzuia Waingereza,
Sisi tungekwisha weza,
Kuwashinda Warussia."

947

"Nguvu zetu twazigawa,
Russia na Italia,
Kisa cha kuzidiwa,
Ni hawa Waitalia."

948

"Kwetu hawafai sana,
Nawaona wana laana,
Tangu tulipoungana,
Heri ilitukimbia."

949

“Japani imeungana,
Kwetu sisi kupigana,
Lakini tamaa sina,
Kuwa watafanikiwa.”

950

“Kwa wakati mwingi sana,
Amepigana na China,
Ingawa anazo zana,
China hakuichukua.”

951

“Itakuwa miujiza,
Kama Japani aweza,
Kushinda Uingereza,
Na Amerika pamoja.”

952

“Watu waliozoea,
Vita na kushambulia,
Ajabu ingekuwa,
Kupigwa na Japania.”

953

“Lakini sisi Wadachi,
Tulio katika nchi,
Naapa hatukuachi,
Kwa heri wala kwa baa.”

954

Sasa imetukabili,
Habari ya admeli,
Darlan mwenye akili,
Na moyo wa ushujaa.

955

Wakati ulipojiri,
Wa Ufaransa kukiri,
Kutoka katika shari,
Darlan hakuridhia.

956

Alipeleka kwa siri,
Habari kwa manowari,
Kuwa hana amri,
Ya kusema kujitolea.

957

Alisema admeli,
Habari kwa signali,
Kuwa hana kauli,
Kusema na kutiwa.

958

Hili linatafsiri,
Alitaka manowari,
Zijiunge na Wahuri,
Kwao zipate tetea.

959

Kwa tafsiri nzuri,
Alionyesha dhahiri,
Kuwa hakuhiari,
Wanamaji kujitolea.

960

Bali kwa bahati mbaya,
Ishara aliyotoa,
Watu hawakuelewa,
Akatunga mpya njia.

961

Alimeza yake ari,
Kushindwa akakukiri,
Kwa kutaka manowari,
Zirudi kwa Wahuria.

962

Alikwenda kwa Petain,
Akajiweka Darlan,
Chini ya Wajermani,
Kutii na kuridhia.

963

Mtu waliyemcha,
Akayaficha makucha,
Kama kwamba ameacha,
Uhuru kuuwania.

964

Simba katika kuwinda,
Ndivyo anavyokwenda,
Makucha yake hupenda,
Kwanza kuyazuia.

965

Tunis yalipofika,
Majeshi ya ushirika,
Darlan hakufugika,
Ari ilimrudia.

966

Ilimrudia ari,
Na kiu ya uhuri,
Akatamka shauri,
Giraud la kumwambia.

967

Alimwambia Giraud,
“Nataka ujitahidi,
Kutekeleza mradi,
Wahuri kusaidia.”

968

“Adui anaitea,
Nchi ya Ufaransa,
Giraud fanya siasa,
Jiunge na Wahuria.”

969

“Kichwa sitakiinua,
Kama nitavumilia,
Nchi niliyozaliwa,
Adui kuionea.”

970

“Aibu tuliyopata,
Natamani kuifuta,
Kwa kujiunga kwa vita,
Uhuru kuutetea.”

971

Hili liliwapendeza,
Watu wa Uingereza,
Mara wakajihimiza,
Kumpokea shujaa.

972

Habari ya uhaini,
Ilitangazwa hewani,
Kwa kuepuka Darlan,
Sana akalaumiwa.

973

Lawama alilopewa,
Darlan halina njia,
Bure alilaumiwa,
Kusingiziwa hatia.

974

Huyu ni Mfaransa,
Kwa Wadachi ilipasa,
Kuwakimbia kabisa,
Kwao apate tetea.

975

Ingalikuwa makosa,
Admeli Mfaransa,
Uhuru wa Ufaransa,
Kuacha kuutetea.

976

Baada ya siku haba,
Ikatokea ghiliba,
Iliyoleta msiba,
Darlan akauawa.

977

Aliviziwa kwa hila,
Akapigwa bastola,
Risasi tatu ghafila,
Akaanguka shujaa.

978

Yalitokea afisi,
Mauti haya meusi,
Hapana aliyekisi,
Kuwa aliviziwa.

979

Mwaka wake wa ajali,
Kumi na tisa awali,
Arobaini na mbili,
Tarakimu hutiwa.

980

Ishirini na nne Desemba,
Ya mwaka nilioimba,
Ndipo yalipofumba,
Maisha yake shujaa.

981

Mtendaji jambo hili,
La kuua admeli,
Mtu wa kabila mbili,
Kwa mama Muitalia.

982

Baba yake Mfaransa,
Akafanywa ana hisa,
Kutetea Ufaransa,
Kumbe ana nia mbaya!

983

Mtu huyu mhalifu,
Hakuishi kujisifu,
Baada muda hafifu,
Na yeye aliuawa.

984

Aliua Alhamisi,
Hukumu ya Algiers,
Ikakata Jumamosi,
Muuaji kuuawa.

985

Mtu wa nia mbili,
Baada ya siku mbili,
Za majuto makali,
Hakuona tena jua.

986

Kwa desturi hasidi,
Maisha hayafaidi,
Adhabu kali hubidi,
Mara akigunduliwa.

987

Mambo aliyowaza,
Darlan kuyafanyiza,
Yote aliyatimiza,
Kabla ya kuuawa.

988

Katika matendo bora,
Yenye sifa kila mara,
Moja ni kwenda ahera,
Ukisha kufanikiwa.

989

Hayo ndiyo majaliwa,
Wapatayo mashujaa,
Hufa yakisha kuwa,
Mambo waliyonuia.

990

Pengo hili lilibidi,
Kuliziba Giraud,
Mwenye moyo wa juhudi,
Vita vikaendelea.

991

Jemadari Giraud,
Ni mvunjaji ukaidi,
Yumo katika idadi,
Ya Wahuri mashujaa.

992

Moyoni hana kinyume,
Ana sifa za kiume,
Tena mvunjaji ngome,
Kufungwa hakuzoea.

993

Wadachi walimshika,
Ngomeni wakamweka,
Mara akawaponyoka,
Kifungo hakuridhia.

994

Giraud alitaja,
"Tuna adui mmoja,
Afungaye bila hoja,
Watu wasio hatia."

995

"Kwanza tunataka,
Afukuzwe Afrika,
Hapa akiondoka,
Nyuma tutamwandamia."

996

"Halafu itatupasa,
Ulaya kuitakasa,
Tuutoe Ufaransa,
Udhalimu wa dunia."

997

“Tuufukuze utoke,
Udhalimu wende zake,
Ufaransa na dola yake,
Irudie uhuria.”

998

“Kama dhalimu hatoki,
Ikarudi tena haki,
Vita haviamuliki,
Hii ndiyo yangu nia.”

999

“Hatutaki atupunje,
Tutapiga tumvunje,
Adui atoke nje,
Ya Ufaransa huria.”

1000

“Nchi ya nuru kwanza,
Ya watu kuwaongoza,
Sasa imefunga kiza,
Nikikumbuka nalia!”

1001

“Moyo hauhimili,
Kuliona jambo hili,
Hii ni idhilali,
Nzito kuvumilia.”

1002

“Idhilali hii nzito,
Inatia moyo joto,
Tutamlipa majuto,
Adui wa dunia.”

1003

“Hukumu imelazimu,
Kwa mmwagaji wa damu,
Mkuu wa udhalimu,
Kufukuzwa ni sheria.”

1004

“Waingereza na Waamerika,
Na wengine washirika,
Ndivyo wanavyotaka,
Adui kumtendea.”

1005

“Na sisi Wafaransa,
Imetupasa kabisa,
Kuonyesha Ufaransa,
Kuwa itajikomboa.”

1006

“Tutaonyesha heshima,
Ya Ufaransa daima,
Kuanguka si kukoma,
Hatuwezi tawaliwa.”

1007

“Mbegu iliyoanguka,
Ndiyo inayochipuka,
Kwa hivi nina hakika,
Baraka itatujia.”

1008

“Ufaransa ilinguruma,
Adui akatetema,
Sasa haina heshima,
Fahari imepotea!”

1009

“Nchi iliyosema,
Adui akainama,
Itatetea heshima,
Yake ya asilia.”

1010

“Nchi iliyopiga,
Ikatia moyo woga,
Si yamkini kuaga,
Kabla kujikomboa.”

1011

“Kama ameghafilika,
Hitler atakumbuka,
Ufaransa kufugika,
Taabu sana kuridhia.”

1012

“Nchi ya uaskari,
Na fahari ya uhuri,
Utumwa haitakiri,
Lazima kujikomboa.”

1013

“Moto aliouzima,
Adui bado mzima,
Tena utamchoma,
Tumwonye ushujaa.”

1014

“Lazima tutasimama,
Tupiganiye heshima,
Na fahari ya daima,
Mungu atatumalia.”

1015

“Siwezi kuutabiri,
Mwisho wa hizi shari,
Ila najua vizuri,
Kuwa tutafanikiwa.”

1016

“Jambo lililo muhimu,
Ambalo nalifahamu,
Itatoka nyingi damu,
Kurudisha uhuria.”

1017

“Mmea wa damu hiyo,
Yatakuwa matokeo,
Ya ushindi tutakao,
Hapa katika dunia.”

1018

Zaidi tena habari,
Viongozi wa uhuri,
Walifanyiza safari,
Wakakutana pamoja.

1019

Kwanza ni Churchill,
Roosevelt ni wa pili,
Mtu wa tatu De Gaulli,
Na Giraud pamoja.

1020

Watu hawa mbali mbali,
Wote walitoka mbali,
Wakakutana mahali,
Jina wajibu kujua.

1021

Hawa walikutanika,
Kwa baraza Casablanca,
Bandari ya Afrika,
Wote wakahudhuria.

1022

Kumradhini tamko,
Mahali hasa iliko,
Bandari hiyo Morocco,
Yafaa sana kujua.

1023

Baraza ya maamiri,
Ilikuwa Januari,
Mwaka wa nne wa shari,
Tarehe yake sikia.

1024

Tarehe kumi na nne,
Hata ishirini na nne,
Viongozi wote wanne,
Walibarizi pamoja.

1025

Viongozi hawa wanne,
Walikuja wakutane,
Waliyo nayo wanene,
Wajue la kutumia.

1026

Kusonga kwa Warussi,
Hakukumpa nafasi,
Stalin kujilisi,
Udhuru wake katoa.

1027

Kawambia wateule,
"Sasa tunasonga mbele,
Siwahi baraza ile,
Mimi kuhudhuria."

1028

"Nataka kwenu nafasi,
Niwaongoze Warussi,
Msifanye wasiwasi,
Mimi kutohudhuria."

1029

"Nyinyi mliokutana,
Kila mtakalonena
Mimi ni radhi sana,
Yote nimewaridhia."

1030

Walibarizi kusema,
Na kutafuta hekima,
Wakamaliza salama,
Baraza waliyojia.

1031

Baraza ilipatana,
Wadachi washindwe sana,
Waone hapana maana,
Wanyonge kuwaonea.

1032

Iitaka Jermani,
Tena asitamani,
Kudhulumu maskini,
Bure kuwashambulia.

1033

Baraza ya viongozi,
Wakati wa kubarizi,
Iliwatia simanzi,
Maadui kusikia.

1034

Baraza ya siku kumi,
Ilifanyiza uvumi,
Hakutuliza ulimi,
Adui alipojua.

1035

Baraza ya Afrika,
Iliwatia mashaka,
Wadachi wakazuzuka,
Kusema yasiyokuwa.

1036

Habari walitamka,
Amekwenda Amerika,
Kumbe yuko Afrika,
Churchill aongea.

1037

Uvumi walikariri,
Yuko London Waziri,
Kumbe amesafiri,
Uturuki kukagua.

1038

Wakati wa marejeo,
Viongozi kwenda kwao,
Churchill mwenye cheo,
Uturuki kapitia.

1039

Kafika hata Adana,
Akapata kumwona,
Mtu maarufu sana,
Inonu mteuliwa.

1040

Alikuwa kama tunu,
Churchill kwa Inonu,
Alipopata fununu,
Hitler alichukia.

1041

Inonu na Churchill,
Walihadithi wawili,
Mashauri mbalimbali,
Kwa heshima na murua.

1042

Mkutano siku mbili,
Ulifanyizwa mahali,
Juu ya njia ya reli,
Baraza yake behewa.

1043

Walikaa behewani,
Wakasema ya moyoni,
Juu ya Jermani,
Uturuki ikirukiwa.

1044

Walisema biashara,
Na mambo mengine bora,
Ya mapato na tijara,
Mkataba ukatiwa.

1045
Balozi Von Papen,
Alipopata yakini,
Ya Inonu na mgeni,
Hakupata kutulia.

1046
Hili lilipokwisha,
Papen lilimuwasha,
Kwa Hitler kajibisha,
Mambo yaliyotokea.

1047
Baraza juu ya reli,
Ilikuwa pilipili,
Kwa Hitler jambo hili,
Kinywani isiyopoa.

1048
Churchill alisifu,
Wingi wa uaminifu,
Wa Inonu maarufu,
Kwao aliporejea.

1049
Sifa ya uaminifu,
Furaha na ukunjufu,
Ilimtia hofu,
Hitler kuisikia.

1050
Alihofu Uturuki,
Kwake itafanya dhiki,
Ikifanya urafiki,
Na Waingereza pamoja.

1051
Hitler alifikiri,
Kikombe cha shubiri,
Alichowapa fakiri,
Kwake kinakaribia.

1052
Hitler alizoea,
Mwenyewe kujitogoa,
Kila ilipotokea,
Siku aliyotawazwa.

1053
Alifanya sikukuu,
Kwa fahari na makuu,
Akajidai ukuu,
Na dola kuzibeua.

1054
Sikukuuye ya kumi,
Hakunyanyua ulimi,
Wala hotuba ya kemi,
Hakuweza kuitoa.

1055
Hakuweza kujisifu,
Na dola kuzikashifu,
Kwa sababu alihofu,
Fedheha na kuzidiwa.

1056
Hotuba ya utukufu,
Kudai umaarufu,
Nguvu na ukamilifu,
Watu hawakuambiwa.

1057
Kwa desturi mti,
Chini ya samawati,
Jua likiwa kati,
Kivuli kinapungua.

1058
Na Hitler kadhalika,
Hotuba hakutamka,
Kwa sababu iliwaka,
Nguvu ya uhuria.

1059
Nguvu ilimwinamia,
Kwanza aliyobeua,
Usemi ukapotea,
Udhuru ukatolewa.

1060
Udhuru usio njia,
Wadachi waliutoa,
Hitler hana wasaa,
Hotuba yake kutoa.

1061
Hiyo siyo sababu,
Ya kuacha kuhutubu,
Alichelea aibu,
Kushindwa na Warussia.

1062
Alikuwa na majonzi,
Huyu mkuu wa Nazi,
Alipoona hawezi,
Kuwashinda watu hawa.

1063
Warussia na Wafini,
Walipokuwa vitani,
Aliwadunisha chini,
Hitler Warussia.

1064
Aliwatoa thamani,
Hawahimili vitani,
Kumbe ni wapigani,
Wasio shaka na doa.

1065
Huzuni ilimjia,
Kuona amepotea,
Kuwapima sawasawa,
Kama walivyokuwa.

1066
Hakupima sawasawa,
Kuwa Warussia shujaa,
Tena wana udhia,
Kuwachokoza ni baa.

1067
Aliwaona wapuuzi,
Kumpiga hawawezi,
Kumbe watamuhizi,
Ajute na kushangaa.

1068
Watu aliodynamisha,
Sasa walimtisha,
Udhuru wa kuzuzusha,
Goering akautoa.

1069

“Sasa tunatiwa fora,
Kwenda nyuma kila mara,
Kwa sababu ya kudura,
Si nguvu ya Warussia.”

1070

“Wakati utafika,
Wa Russia kuanguka,
Hapo itatendeka,
Adhabu kwa Wahuria.”

1071

“Mtu asifikiri,
Nchi yetu itakiri,
Ushindi wa uhuri,
Hilo shida kutokea.”

1072

“Mtu anayekubali,
Litakuja jambo hili,
Huyo hana akili,
Hafai kuaminiwa,”

1073

“Ndege za Wajermani,
Nyingi haziko mijini,
Ndiyo sababu nadhani,
Miji yetu kuvunjiwa.”

1074

“Ndege zimo hamayani,
Magharibi na kusini,
Mashariki na kasikazini,
Nyingi tumezigawa.”

1075

“Ninawapa ahadi,
Ndege hizo zikirudi,
Kuwa hapana budi,
Wahuria watatujua.”

1076

Dharura hizi pungufu,
Shabaha yake upofu,
Kuwapa udanganyifu,
Watu wasioelewa.

1077

Watu wasioelewa,
Hasa wao maraia,
Siri walizuiwa,
Kweli hawakuambiwa.

1078

Habari zile na hizi,
Zilizosema na Nazi,
Hazikutowa uwazi,
Wa mambo yalivyokuwa.

1079

Walipochukua nyara,
Walidai kuwa bora,
Hawakujua kudura,
Mungu wala majaliwa.

1080

Iliota kwa haraka,
Nguvu yao kama chaka,
Wala hawakukumbuka,
Kukatwa na kung'olewa.

1081

Russia kila kukicha,
Sasa iliwafikicha,
Ikakata makucha,
Ya wenye kujitogoa.

1082

Mussolini kusikia,
Baraza ilivyokuwa,
Maneno ya kubeua,
Mengi sana alitoa.

1083

Alisema maneno,
Mengi yasiyo mfano,
Kwa kushindwa mapigano,
Na koloni kutwaliwa.

1084

Labda alibeua,
Kwa sababu Italia,
Yeye ilimchagua,
Hasarani kuitia.

1085

Kama alichaguliwa,
Faida kuiletea,
Kinywa asingefunua,
Kuona amepotea.

1086

Neno asingetamka,
Wala kufanya dhihaka,
Machozi yangemtoka,
Dharau ingekimbia.

1087

Huzuni ingemshika,
Kwa sababu Afrika,
Koloni walizoshika,
Zote ziliwakimbia.

1088

Ingemliza hasara,
Ya koloni zao bora,
Kuwapotea mara,
Kama kuzimika taa.

1089

Nchi ya Abyssinia,
Fahari ya Italia,
Mwaka haikuchukua,
Mara iliwakimbia.

1090

Katika Somaliland,
Waliodai ufundi,
Kuwa nyuma hawendi,
Mbio walikimbia.

1091

Wahuri waliingia,
Nchi ya Eritrea,
Bendera ya Italia,
Ikakoma kupepea.

1092

Majeshi ya Axis,
Yalipoteza watesi,
Wengi wasio kiasi,
Yakatolewa Libya.

1093

Bendera ya Italia,
Katika Tripolitania,
Wahuri waliitua,
Nchi ikachukuliwa.

1094

Hasara za kulemea,
Hizi zilizotokea,
Ajabu kuzibeua,
Mkuu wa Italia.

1095

Habari hii si kweli,
Msingi wake dhalili,
Wala mtu hakubali,
Dharau ya Italia.

1096

Labda Mussolini,
Jambo alilotamani,
Ni kufutwa duniani,
Taifa la Italia.

1097

Labda aliliona,
Si taifa la maana,
Lilipompa ubwana,
Juu ya Waitalia.

1098

Ngazi aliyopanda,
Atakavyo akatenda,
Kuanguka alipenda,
Kabla ya kuchelea.

1099

Hili lilimpendeza,
Ndiyo kisa cha kuweza,
Kudharau baraza,
Ya viongozi shujaa.

1100

Watu aliosimanga,
Vita wakivipanga,
Adui hutangatanga,
Akakosa pa kukaa.

1101

Wasemapo neno lao,
Kuamru shambulio,
Adui huenda mbio,
Akajuta kuzaliwa.

1102

Wafanyapo shambulio,
Adui harudi kwao,
Ila hurudi kilio,
Na matanga kufanyiwa.

1103

Salama waipatayo,
Watu waokokao,
Ni kuwa mateka yao,
Jingine shida kuwa.

1104

Wasemalo halirudi,
Kwa wingi wa jitihadi,
Tena huwajia sudi,
Kwa haki kuitetea.

1105

Ndlyo wahesabiwao,
Woledi wa maandao,
Kudharau watu hao,
Ni kama kujiponzea.

1106

Bure alijigamba,
Munsolini na kugomba,
Fini si sawa na simba,
Kwa nguvu na ushujaa.

1107

Hawalingani sawa,
Wanyama wawili hawa,
Fisi hana wasaa,
Simba akikaribia.

1108

Mahali akikijilisi,
Simba pana wasiwasi,
Fisi hapati nafasi,
Hofu humkulia.

1109

Kurudi kwa wasafiri,
Safari ya mashauri,
Maneno walihubiri,
Watu kuwatangazia.

1110

London alipofika,
Kutoka Casablanca,
Churchill katamka,
Nia waliyonuia.

1111

Alieleza habari,
Akataja mashauri,
Ya kuzimisha shari,
Maneno yake sikia:

1112

“Lazima vita tushike,
Kwa nguvu visitutoke,
Hata adui achoke,
Hili tumekusudia.”

1113

“Adui sharti awake,
Damu imchuruzike,
Kama majeshi yake,
Yalivyofanywa Russia.”

1114

“Apigwe bara na pwani,
Hewani na baharini,
Hata aombe amani,
Hima bila kuchelewa.”

1115

“Imetupasa mwanzoni,
Kupiga sabmarini,
Za adui baharini,
Ama zitatusumbua.”

1116

“Hizo tusipozidhili,
Tukazishinda awali,
Nguvu yetu kamili,
Kutumwa itachelewa.”

1117

“Nguvu ikikawia,
Adui kumwelelea,
Vita vitaendelea,
Kuichafua dunia.”

1118

“Na huo siyo mradi,
Lazima tujitahidi,
Kukomesha uhasidi,
Watu wapate tulia.”

1119

“Watu hawana raha,
Imekimbia furaha,
Kwa vifo na majeraha,
Huzuni imeenea.”

1120

“Watu hawana pumzi,
Kwa vilio na machozi,
Wanataka ukombozi,
Upesi kuwafikia.”

1121

“Lazima Jermani,
Taliani na Japani,
Walazimishwe amani,
Bila sharti kutia.”

1122

“Hatutaki maadui,
Kufanya tena kisozi,
Wala sharti kudai,
Wakati wa kujitolea.”

1123

“Amani ya masharti,
Ya adui penye hati,
Itasaliti umati,
Tena izuke baa.”

1124

“Hatutaki kuliona,
Jambo hilo kuja tena,
Kwa hivi tutapigana,
Kusudi kulitangua.”

1125

“Lazima maadui,
Amri yetu watii,
Jingine haturidhii,
Amani ikitokea.”

1126

“Hatutaki ikirahi,
Jeuri na usafihi,
Kuuu na kujeruhi,
Kila mara kutokea.”

1127

“Si kusudi la umbile,
Dhuluma kujaa tele,
Na vita kuwa milele,
Hapa katika dunia.”

1128

“Kama tutatangulia,
Kushinda vita Ulaya,
Japani ikibakia,
Tutakwenda saidia.”

1129

Kurudi kwa Roosevelt,
Kwao katoa sauti,
Akawambia umati,
Baraza ilivyokuwa.

1130

“Baraza niliyokwenda,
Imenuia kutenda,
Kila njia ya kushinda,
Adui kumfanyia.”

1131

“Lazima kila upande,
Apigwe mengi makonde,
Asijue wapi ende,
Kushoto au kulia.”

1132

“Afanyiwe shambulizi,
Mpaka awe hawezi,
Kujua omo na tezi,
Kwa hali ya kuzidiwa.”

1133

“Apigwe mbele na nyuma,
Asiweze kusimama,
Kimbilio la salama,
Limshinde kulijua.”

1134

“Asijue atokako,
Wala mahali endako,
Mkuu wa machafuko,
Kwa kupigwa kila njia.”

1135

“Japani tukimwendea,
Kisiwa hata kisiwa,
Miaka mingi itakuwa,
Bure tutakawia.”

1136

“Kila njia iliyoko,
Bora ya kufika huko,
Pasipo mzunguko,
Wajibu kuitumia.”

1137

“Tutafanya barabara,
Moja isiyo duara,
Ya kutufikisha mara,
Nchi ya Japania.”

1138

“Lazima twende Tokyo,
Kwa mfalme wao,
Tukafanye shambulio,
Kwa njia moja kwa moja.”

1139

“Tukamwonye Mikado,
Asiyoyaona bado,
Mpaka wamake do!
Watu wa Japania.”

1140

“Zitakwenda mzmomzo,
Ndege zetu mfulizo,
Zikakomeshe mzozi,
China hata Japania.”

1141

“Nia tuliyo nayo,
Ni kufanya shambulio,
Hata siku yashindayo,
Majeshi ya uhuria.”

1142

“Mpaka majeshi hayo,
Yapite na shangwe lao,
Berlin na Tokyo,
Na Rumi kwa Italia.”

1143

“Kama havikukatika,
Ulaya vita haraka,
Japani ikianguka,
Tutakwenda Ulaya.”

1144

“Hitler anaelewa,
Hatari yake Ulaya,
Kama itampotea,
Nchi ya Tunisia.”

1145

“Hiyo ndiyo maana,
Ya adui kupindana,
Kwa sadaka kubwa sana,
Ya watu kuangamia.”

1146

“Adui ajitahidi,
Kufanyiza ukaidi,
Nia yake na mradi,
Tuchelewe Tunisia.”

1147

“Tunisia nafikiri,
Vita tena vikijiri,
Hasara bila urari,
Lazima zitatokea.”

1148

“Hasara bila kipimo,
Kubwa zisizo kikomo,
Watapata waliyomo,
Nasi tumejiandaa.”

1149

“Tumeviandaa vita,
Karibu tutaviteta,
Ambavyo havijapata,
Duniani kutokea.”

1150

“Nawataka wasikizi,
Masikio yawe wazi,
Kuwa siku zizi hizi,
Sisi tutashambulia.”

1151

“Siri tunafunua,
Kuwa tunakusudia,
Kushambulia Ulaya,
Kwa njia ya Tunisia.”

1152

“Hiyo ndiyo dhamiri,
Waliyo nayo Wahuri,
Na siku ya kudhihiri,
Sasa inakaribia.”

1153

Roosevelt na Churchill,
Nia hawakubadili,
Wote watu wawili,
Walisema sawasawa.

1154

Maneno waliyotaja,
Nia ilikuwa moja,
Iluikutokea hoja,
Iliyobadili nia.

1155

Wakati wa kusemeka,
Hayo niliyoandika,
Vita vya Afrika,
Vilikuwa Tunisia.

1156

Wingi wa maadui,
Walioshika nchi hii,
Jumla haipungui,
Robo milioni moja.

1157

Hiyo robo milioni,
Ilikuwa mtegoni,
Kama ulimi kinywani,
Jinsi ilivyozingwa.

1158

Na kila siku mtego,
Ulijibana kidogo,
Liweze kila pigo,
Adui kumwangukia.

1159

Wahuri waliazimu,
Kila kombora na bomu,
Liangukiye hasimu,
Wakati wa kutolewa.

1160

Waliibana duara,
Kila bomu na kombora,
Lipate tia hasara,
Wakati wa kutumiwa.

1161

Ikiwa hakuuawa,
Adui hakutakiwa,
Aweze kujiokoa,
Ila mateka kuwa.

1162

Hakutakiwa tena,
Arudiye kupigana,
Adui aliyeona,
Vita vya Tunisia.

1163

Basi Jeshi la Nane,
Likenda kama mashine,
Makusudi lipigane,
Na Rommel Tunisia.

1164

Hakutaka akutane,
Tena na Jeshi la Nane,
Tangu Rommel aone,
Nguvuye na ushujaa.

1165

Vita vya jeshi hili,
Vilikuwa vikali,
Akahofu Rommel,
Tena kumfikia.

1166

Ndilo lililomuhizi,
Wakati wa shambulizi,
Likamwonyesha kazi,
Misiri akatolewa.

1167

Misiri alipohama,
Jeshi halikusimama,
Lilimfuata nyuma,
Wala halikumwachia.

1168

Montgomery na Alexander,
Vyeo vyao vilipanda,
Kwa kazi iliyotendwa,
Na jeshi hili sikia.

1169

Mara lilipoingia,
Jeshi hili Tunisia,
Eisenhower kapewa,
Mamlaka kuongoa.

1170

Huyo ni Mwamerika,
Shujaa alisifika,
Sasa aliyeshika,
Uongozi Tunisia.

1171

Alexander akawa,
Chini ya Eisenhower,
Amiri wao wa hewa,
Arthur Tedder alikuwa.

1172

Arthur Tedder mashuhuri,
Na mwanahewa hodari,
Alielewa vizuri,
Vita katika hewa.

1173

Mtu huyu maarufu,
Shujaa asiye hofu,
Akawa mdhaminifu,
Juu ya Tunisia.

1174

Wilson alipanda,
Mahali pa Alexander,
Akahimiza kushinda,
Badili yake akawa.

1175

Jeshi la askari,
La Wafaransa Wahuri,
Lilipewa jemadari,
Anderson Tunisia.

1176

Jemadari Wilson,
Pamoja na Anderson,
Walikuwa wapigani,
Hodari na mashujaa.

1177

Andrew Cunningham,
Admeli maalum,
Yeye alishika zamu,
Huko Mediterranea.

1178

Admeli Harwood,
Yeye ilimbidi,
Kuangalia zaidi,
Buhari Sham sikia.

1179

Macho ya dunia nzima,
Yalivutwa kutazama,
Siku ya vita kuvuma,
Juu ya Tunisia.

1180

Wakati huo sikia,
Tunisia ilijaa,
Matope mengi ya mvua,
Majeshi yakangojea.

1181

Majeshi yalingojea,
Mabadiliko ya hewa,
Ikabakia doria,
Kutazama kila njia.

1182

Doria huko na huku,
Zilifanyiza viteku,
Mchana na usiku,
Njia ziliangaliwa.

1183

Masika yalipokoma,
Majeshi mbele na nyuma,
Yalianza kusimama,
Adui kumwelekea.

1184

Walisonga wanaume,
Makusudi wamwegeme,
Adui katika ngome,
Za Mareth Tunisia.

1185

Mareth ni malindo,
Yenye ngome nyingi kando,
Wakaonyeshana kondo,
Axis na huria.

1186

Majengo ya ngome hizo,
Yalikuwa ya mkazo,
Yakamtia mawazo,
Adui kutozidiwa.

1187

Zilijengwa kwa maki,
Adui akasadiki,
Kuwa hazipenyeki,
Ngome kwa kusakifiwa.

1188

Mbele yake pana mto,
Hapo ukawaka moto,
Wa mizinga mizito,
Juu ya Wahuria.

1189
Waliwahi Axis,
Kusonga mbele upesi,
Ili wapige risasi,
Wahuri wakisogea.

1190
Waliileta mizinga,
Axis ya kuinga,
Mara katika anga,
Wahuri wakachachawa.

1191
Watu wa New Zealand,
Walionyesha ufundi,
Wakaliziua kundi,
La Wadachi kukimbia.

1192
Hao walikuja hima,
Kutokea El Hamma,
Wakazuia kwa nyuma,
Njia ya kukimbilia.

1193
Walikuja autani,
Maili arobaini,
Kuzuia Jermani,
Kama hatua moja.

1194
Hilo ndilo tendo,
Lililotia mshindo,
Pale penye malindo,
Ngome zikaingwiwa.

1195
Elfu nane watesi,
Watu wa Axis,
Walishikwa mahabusi,
Mareth ikatwaliwa.

1196
Rommel alikazana,
Kwa hila kila namna,
Hata akakutana,
Na Arnim, Tunisia.

1197
Alikuwa na migando,
Von Arnim ya kondo,
Akasifiwa vitendo,
Hodari kuvumilia.

1198
Tena ni jemadari,
Stadi katika shari,
Rommel akafikiri,
Auni imemjia.

1199
Waliongea wawili,
Rommel akasaili,
"Waionaje shughuli,
Ya vita vya Tunisia?"

1200
"Tangu nitoke Misri,
Wamenandama Wahuri,
Wingi wa askari,
Wangu wamenipotea."

1201
"Nisingetoka Misri,
Buli nguvu ya Wahuri,
Ilipita kadiri,
Ya kuweza vumilia."

1202
"Uzito ulinizidi,
Ikawa hapana budi,
Nifanyize jitihadi,
Niweze kujiokoa."

1203
"Uzito ninaosema,
Umeniandama nyuma,
Hapa tuliposimama,
Nadhani tumezingiwa."

1204
Von Arnim kanena,
"Kila nilipokutana,
Na Wahuri kupigana,
Hasara wamenitia."

1205
"Sisi watu wawili,
Yatupasa kila hali,
Kufanyiza vita kali,
Tusije kulaumiwa."

1206
"Ingawa tuna kusudi,
Ina kutimiza ahadi,
Jambo moja limebidi,
Rommel kukwambia."

1207
"Watu wa Italia,
Ambao twasaidia,
Kila siku wajitolea,
Hawapigani kwa nia."

1208
"Nikifanyiza juhudi,
Kufikiri zaidi,
Naona kama kusudi,
Mtegoni tumetiwa."

1209
"Ninajua kwa hakika,
Kuwa hapa Afrika,
Sisi tutashindika,
Na taabu kutufikia."

1210
"Naona Waingereza,
Lazima watatusoza,
Rommel peleleza,
Haya ninayokwambia."

1211
"Lakini hapana budi,
Tufanyize jitihadi,
Ya kutimiza ahadi,
Tuliypata kutoa."

1212
"Hitler tulimwambia,
Sadaka tutajitoea,
Basi imepasa kuwa,
Ahadi tuliyofoa."

1213

“Na watu wanaoasi,
Katika vyetu vikosi,
Wajibu wao risasi,
Wapigwe wakijitolea.”

1214

Arnim na Rommel,
Walizingiwa mahali,
Urefu maili mbili,
Ndipo walipokuwa.

1215

Na maili arobaini,
Mpaka sabiini,
Ndiyo upana yakini,
Mahali palivyokuwa.

1216

Panafanana na kitu,
Sanduku la pembe tatu,
Watu hao watukutu,
Ndipo walipokuwa.

1217

Ukuta wa chuma pua,
Mgumu kutobolewa,
Ndani yake yalikuwa,
Majeshi ya watu hawa.

1218

Kwa pwani mahali hapo,
Vita vilipokuwapo,
Bandari zilikuwapo,
Za kutoka Tunisia.

1219

Bandari hizo huitwa,
Tunis na Bizerta,
Ikawazwa atapata,
Adui kwenda Ulaya.

1220

Ni bandari mashuhuri,
Za meli na manowari,
Watu wakafikiri,
Adui atakimbia.

1221

Laiti angaliweza,
Baharini kueleza,
Vyombo kama Mwingereza,
Hilo lingalitokea.

1222

Angetawala bahari,
Kwa nguvu ya manowari,
Angefanya ujasiri,
Kuvusha majeshi haya.

1223

Angeiga Waingereza,
Mambo waliyoyaweza,
Dunkirk kufanyiza,
Kuokoa mashujaa.

1224

Hilo lilikuwa shida,
Kwa sababu kila muda,
Ilifanywa kawaida,
Vyombo vyake kuzuiwa.

1225

Hitler hakujaribu,
Kuzileta merikebu,
Kali alizohesabu,
Kwa bahari kuzuiwa.

1226

Wala hakuthubutu,
Kufanyiza utukutu,
Wa kuokoa watu,
Kwa bahari wala hewa.

1227

Tunis na Bizerta,
Wahuri walipopata,
Nguvu ya kuteta vita,
Adui ilimwishia.

1228

Mwanzo wake msiba,
Kusema ole na toba,
Ulikuwa Mei saba,
Mwaka mtasikia.

1229

Mwaka huo hugutiwa,
Kumi na tisa mia,
Arobaini hutiwa,
Tatu ikaishilia.

1230

Tena wajibu ninene,
Wasomaji waone,
Mei tarehe nane,
Ilitua Tunisia.

1231

Tarehe hii hakika,
Ndipo waliposhindika,
Maadui Afrika,
Mateka mengi yakawa.

1232

Ambrosio na Rommel,
Jumla watu wawili,
Waliokoka ajali,
Ya kutekwa Tunisia.

1233

Watu wawili hawa,
Mdachi na Mwitalia,
Ndiyo waliojaliwa,
Kuponyoka Italia.

1234

Jemadari wa hasimu,
Von Arnim fahamu,
Ikawa kwake adimu,
Nafasi ya kukimbia.

1235

Von Arnim alikiri,
Masharti na amri,
Ambayo Jemadari,
Eisenhower katoa.

1236

Kwanza alitamka,
Eisenhower kutaka,
Wajitolee kwa haraka
Bila neno zaidia.

1237

Neno la pili kasema,
Mapatano ni lazima,
Yakubaliwe hima,
Bila ya kuchelewa.

1238

Neno la tatu *lazima,*
Uharibifu kukoma,
Wa zana zilizo nzima,
Na amri kutiwa.

1239

Jumla majemadari,
Waliotii amri,
Wanapata kwa kadiri,
Kumi na moja sikia.

1240

Mtu wa kumi na mbili,
Alifanya ufedhuli,
Akasema hakubali,
Bunduki kuiachia.

1241

Jina lake Spennech,
Kasema kuwa haachi,
Kupigania Udachi,
Wala hatajitolea.

1242

Alifanyiza hamaki,
Kuwambia Marafiki,
Kujitolea hataki,
Kwa maneno kama haya:

1243

“Mimi na wangu watesi,
Tutapigana utesi,
Hata ya mwisho risasi,
Iwe imetuishia.”

1244

Baada muda kidogo,
Wa vishindo na mapigo,
Spennech mwenye togo,
Mikononi alitiwa.

1245

Alikamatwa upesi,
Yeye na chake kikosi,
Kabla hizo risasi,
Kuanza kumwishia.

1246

Alishindwa kupigana,
Akakamatwa na zana,
Nzima kila namna,
Bado hazijapungua.

1247

Mia na hamsini,
Elfu Wajermani,
Pamoja na Taliani,
Mwisho walijitolea.

1248

Hao ni askari,
Wateule na hodari,
Ambao hakufikiri,
Hitler watajitolea.

1249

Walikamatwa na zana,
Nyingi kila aina,
Nu chakula kingi sana,
Vitani kutumia.

1250

Watu kama hawa,
Nu zana zilivyokuwa,
Ajabu kubwa ikawa,
Kukamatwa mara moja.

1251

Watu walitumai,
Watashindwa maadui,
Bali si namna hii,
Ghafa kujitolea.

1252

Ushindi wa nguvu,
Kwa mapigano makavu,
Na kutoana mapovu,
Watu walitazamia.

1253

Hili wasingelitenda,
Lakini Alexander,
Arnim alimshinda,
Kwa vita kuviandaa.

1254

Kadhani Jeshi la Nane,
Litasonga apigane,
Na majeshi mengine,
Yatakaa kungojea.

1255

Watu aliodhania,
Kuwa watangojea,
Mara walishambulia,
Pakawa hapana njia.

1256

Hili lilipotendeka,
Vita vya Afrika,
Mwisho wake ukafika,
Kwa kushinda Wahuria.

1257

Ushindi wa Marafiki,
Ulifuta zote dhiki,
Walizopata Dunkirk,
Watu wa Britania.

1258

Mwaka wa elfu moja,
Tisa mia ikija,
Thelathini na tatu pamoja,
Tarehe hii sikia.

1259

Hitler alitokea,
Akajidai Ulaya,
Kuwa atapindua,
Watawala wa dunia.

1260

Ndipo kilipoanza,
Chama chake kutokeza,
Akafanya miujiza,
Ya kuchafua dunia.

1261

Alidai kuwa bora,
Nguvu nyingi na busara,
Akaudhi kila mara,
Mataifa ya Ulaya.

1262

Alijidai kipawa,
Mambo yote kuelewa,
Hakuwaza patakuwa,
Mtu wa kumzidia.

1263

Alianza utukutu,
Akajisifu kwa watu,
Kuwa hapana kitu,
Ambacho chamtishia.

1264

Alijidai uungwana,
Kuwa hapana tena,
Taifa la kulingana,
Na Wadachi Ulaya.

1265

Alijisuifu werevu,
Akili na welekevu,
Akawaita wabovu,
Watu waliobakia.

1266

Alijisuifu mizungu,
Kushinda wote Wazungu,
Na mambo chunguchungu,
Wenziwe wasiyojua.

1267

Muda wa miaka tisa,
Alifanyiza mikasa,
Ambayo haikupasa,
Watu kuwatendea.

1268

Ghururi ilimshika,
Asiweze kukumbuka,
Kuwa ataanguka,
Na kuchekwa na dunia.

1269

Mwaka wa elfu moja,
Tisa mia ukitaja,
Arobaini na tatu pamoja,
Akashindwa Tunisia.

1270

Wakati wa kufanyika,
Ushindi wa Afrika,
Alikuwa Amerika,
Waziri wa Britania.

1271

Alifanyiwa aliko,
Yeye kufika huko,
Mastadi walioko,
Walihudhuria pia.

1272

Ushindi ulipotimu,
Wa Afrika fahamu,
Alipata salamu,
Huko alikokuwa.

1273

Salamu hizo wajibu,
Ziwe katika kitabu,
Na mimi nitajaribu,
Wasomaji kuwambia.

1274

Mfalme Mtukufu,
Kwa wingi ukinaifu,
Waziri kamwarifu,
Kama hivi sikia:

1275

"Kwa kushinda kwa fahari,
Katika nchi ya hari,
Nimefurahi waziri,
Tena nakushangilia."

1276

"Ninaelewa jinsi,
Tulivyoshinda upesi,
Kuwa ni wewe halisi,
Ambaye uliandaa."

1277

"Nafahamu kwa dhati,
Tena nina ithibati,
Yalivyo madhubuti,
Mawazo yako na nia."

1278

"Moyo wako na nia,
Shida sana kulegea,
Nami nimefurahiwa,
Hili kukutangazia."

1279

"Tangu mashaka ya kwanza,
Hukushindwa kuongoza,
Ninapenda kutangaza,
Kuwa tumefadhiliwa."

1280

"Majeshi ya Afrika,
Yote yaliyoungika,
Kila tulilotaka,
Yamekwisha tutendea."

1281

"Imepata fadhili,
Nchi yetu kamili,
Na wewe wastahili,
Sana kushukuriwa."

1282

"Mataifa ya ona,
Yote yaliyoungana,
Kuwa umepatikana,
Ushindi kwa yako nia."

1283

Hapa sasa ni mahali,
Pa kufanya kila hali,
Majibu ya Churchill,
Nijaribu kuyatia.

1284

"Mfalme Mtukufu,
Naomba kukuarifu,
Salamu zako nadhifu,
Kuwa zimenifikia."

1285

“Mfalme wa heshima,
Nakuarifu ya kama,
Kwako nimepata wema,
Kuliko wenzangu pia.”

1286

“Katika mawaziri,
Mimi najifikiri,
Uwezo bila kadiri,
Kwako nimepokea.”

1287

“Nafikiri hapana,
Waziri mwingine tena,
Ambaye wake bwana,
Mno alimridhia.”

1288

“Katika miaka mitatu,
Ya hatari kubwa kwetu,
Na usumbufu kwa watu,
Sana niliaminiwa.”

1289

“Siku uliyokubali,
Nifanyize serikali,
Ya mataifa ya mbali,
Moyo ulipendezewa.”

1290

“Niliona ni faraja,
Katika siku za haja,
Kuridhiwa mara moja,
Jambo lililotufaa.”

1291

“Sifa uliyosema,
Mfalme wangu mwema,
Imezidi nikipima,
Ustahili wa sawa.”

1292

“Na maneno ya heshima,
Ambayo umeyasema,
Nitakumbuka daima,
Kuishi nikijaliwa.”

1293

Hapa sasa nataka,
Niendeleo kuandika,
Baraza ya America,
Namna ilivyokuwa.

1294

Msemaji wa baraza,
Maneno alitangaza,
Watu kuwaeleza,
Mfano wake sikia.

1295

“Nimejaliwa nafasi,
Kubwa isiyo kiasi,
Mtu mkubwa halisi,
Mbele kuwawekea.”

1296

“Huyu ndiye Winston,
Waziri wa Britani,
Amefika barazani,
Kutoka Britania.”

1297

“Huyu ni mtu mmoja,
Katika wanaotajwa,
Kuwa watu wa haja,
Na muhimu wa dunia.”

1298

“Kuja kwetu Waziri,
Ni dalili mashuhuri,
Ya maungano mazuri,
Sisi na Britania.”

1299

Wasikizi barazani,
Walimwamkia mgeni,
Kwa furaha moyoni,
Shangwe likaendelea.

1300

Shangwe liliendelea,
La mgeni kupokewa,
Dakika zikatimia,
Kadha wa kadha sikia.

1301

Halafu alianza,
Waziri wa Kiingereza,
Kusema na baraza,
Hotuba akaitoa.

1302

“Mkuu wa taadhima,
Msemaji wa heshima,
Na wote wanachama,
Wa baraza nawambia.”

1303

“Kumi na saba yapata,
Miezi iliyopita,
Tangu nilipopata,
Mbele yenu kutokea.”

1304

“Siku kwa mfano,
Zaidi ya mia tano,
Tumejitahidi mno,
Taabu kuzishirikia.”

1305

“Mbele ya ukatili,
Na uadui mkali,
Tumefanya kila hali,
Mateso kuvumilia.”

1306

“Mateso na maumivu,
Ya adui mwenye nguvu,
Tumetatamua mbavu,
Kila bega kuchukua.”

1307

“Tumefanya maungano,
Kukabili mapigano,
Sehemu nyingi mno,
Mbalimbali za dunia.”

1308

“Tumepigana shari,
Nyingi bila kadiri,
Za bara na za bahari,
Hata katika hewa.”

1309

“Tangu mliponitaka,
Nije tena Amerika,
Hali kazi yatendeka,
Naona kuheshimiwa.”

1310

“Ni dalili mashuhuri,
Katika wangu umri,
Kuwa hatukuhasiri,
Tulipofanya ubia.”

1311

“Waonapo halaiki,
Tumekuwa marafiki,
Wema katika dhiki,
Fahari inanijia.”

1312

“Fahari inanijia,
Kuona tumeingia,
Kazi tuliyonua,
Kutimiza kila njia.

1313

“Ninasema waziwazi,
Mbele yenu wasikizi,
Kwanza sikumaizi,
Kwamba tutakuwa bia.”

1314

“Sikutumai kabisa,
Kuwa hii mikasa,
Mwisho itatupasa,
Kwa umoja kuzuia.”

1315

“Sikuwaza jambo hili,
Kama hizi nchi mbili,
Zitaungana kamili,
Adui kumwelelea.”

1316

“Wakati ule wa kite,
Wa majonzi nchi zote,
Utakumbukwa na wote,
Watu katika dunia.”

1317

“Ndiyo wakati adhimu,
Wa kujua mwanadamu,
Kuwa jambo muhimu,
Ni kuungana pamoja”

1318

“Hapana jambo kamili,
Kuliko watu wawili,
Waunganapo kweli,
Kwa vita na kutulia.”

1319

“Waunganapo kwa haki,
Kwa amani na dhiki,
Huwa haikadiriki,
Heri inayowajia.”

1320

“Basi nilijiandaa,
Kwa roho kunikua,
Mapigo kuvumilia,
Yote yaliyotujia.”

1321

“Mapigo mengi makali,
Ya Mashariki ya Mbali,
Yalilazimu kudhili,
Waingereza sikia.”

1322

“Mapigo yalituja,
Mengi kutuangukia,
Ambayo yalitokea,
Nchi ya Japania.”

1323

“Wakati ule hakika,
Uingereza na Amerika,
Bahari ziliwatoka,
Pasific na India.”

1324

“Hasara moja kwa moja,
Kama kushuka daraja,
Mara moja zilikuja,
Kwetu na wenzetu pia.”

1325

“East Indies na Singapore,
Phillipines na Malaya,
Orodha nawatajia,
Hasara za Britania.”

1326

“Hasara za Waingereza,
Kama nilivyoeleza,
Hizi zapita za kwanza,
Katika historia.”

1327

“Mkuu wa taadhima,
Msemaji wa heshima,
Hasara hizi lazima,
Zinataka kufidiwa.”

1328

“Niamruni kunena,
Nionyeshe kwa bayana,
Mtu asiseme tena,
Waingereza watalegea.”

1329

“Kusema hatudhuriwi,
Na matendo ya adui,
Atendayo nchi hii,
Hilo si kweli sikia.”

1330

“Sisi na Waamerika,
Vita tutavishika,
Kwa nguvu pasipo shaka,
Mpaka tupate dia.”

1331

“Nimekuja kuwambia,
Kuwa tunakusudia,
Kupigana vita bia,
Tumshinde Japania.”

1332

“Tutatumia busara,
Za majeshi yetu bora,
Hata tutie fora,
Sisi na nyinyi pamoja.”

1333

“Hatutakoma kuteta,
Pumzi tunapopata,
Na damu ikipita,
Mishipani sikia.”

1334

“Sehemu kuu ya vita,
Kwa Wajapani kuteta,
Itapasa kuleta,
Majeshi yaliyokua.”

1335

“Majeshi mengi ya hewa,
Na ya baharini pia,
Ambayo yasimamiwa,
Sasa na Britania.”

1336

“Majeshi yakitumiwa,
Mipakani mwa India,
Ndiyo njia nadhania,
Ya China kusaidiwa.”

1337

“China imeteseka,
Kisha imesumbuka,
Ndipo mimi nikataka,
Upesi kusaidiwa.”

1338

“Msaada wa haraka,
China tukipeleka,
Ni jambo la kutukuka,
Katika mambo ya bia.”

1339

“Tena nataka kunena,
Msikose kuona,
Kuwa nimefuatana,
Na Wavell pamoja.”

1340

“Amekuja Amiri,
Yeye na majemadari,
Wawili mashuhuri,
Waliotoka India.”

1341

“Safari ya watu hawa,
Hawakuja mwombea,
Mikado wa Japania,
Furaha wala uzima.”

1342

“Mimi nilifikiri,
Lingekuwa jambo zuri,
Walio na mashauri,
Wakutane pamoja.”

1343

“Wakutane wanene,
Kirafiki wapatane,
Kusudi wote waone,
Lipasalo kutumiwa.”

1344

“Habari ninawapasha,
Ili kuwahakikisha,
Mwaweza kuamrisha,
Majeshi ya India.”

1345

“Yaweza majeshi hayo,
Kufanya mashambulio,
Upande wa matokeo,
Ya jua mkiridhia.”

1346

“Yaweza kuandama,
Majeshi njia ya Burma,
Hili mkilisema,
Amri itatolewa.”

1347

“Mkitaka mwendo huo,
Hii alasiri leo,
Yaweza amri hiyo,
Mara moja kutolewa.”

1348

“Kwa sababu ya milima,
Na misitu kusimama,
Mwendo ninaosema,
Mno una udhia.”

1349

“Mwendo huo wataka,
Kama mnavyotamka,
Nyinyi Waamerika,
Elimu ya kuelewa.”

1350

“Nakana kila tuhuma,
Mkuu wa taadhima,
Kwa ajili ya wema,
Wako nitaaminiwa.”

1351

“Tusifanye tuhuma,
Tukaficha macho nyuma,
Kila shauri jema,
Yafaa kulitumia.”

1352

“Mimi na Serikali,
Ambaye ni wakili,
Twanuia kila hali,
Kila mtu kutumia.”

1353

“Kila bunduki na zana,
Vyombo kila namna,
Na kila neno la maana,
Twanuia kutumia.”

1354

“Hilo tutakamilisha,
Kama tulivyokwisha,
Zamani kuonyesha,
Kila tulipoingia.”

1355

“Wakati wa kufanyika,
Baraza Casablanca,
Ushahidi ulitoka,
Wenye nguvu maridhawa.”

1356

“Kushindwa kwa Japani,
Si kushindwa Jermani,
Na kushindwa Jermani,
Ni kushindwa Japania.”

1357

“Ujuzi wa jambo hili,
Si kama unabadili,
Kuwa nchi hizi mbili,
Haziendi njia moja.”

1358

“Ndipo ikapasa,
Nguvu nyingi hasa,
Za Amerika sasa,
Pasific kutumiwa.”

1359

“Amerika ilidhamini,
Kupigana na Japani,
Makusudi kuauni,
New Zealand na Australia.”

1360

“Tulishika Atlantiki,
Tukazikabili dhiki,
Kuu zilizo na maki,
Zote tukazichukua.”

1361

“Laiti hii bahari,
Iungayo kuabiri,
Isingeshikwa hodari,
Hasara ingetujia.”

1362

“Kwa nguvu na jitihadi,
Tumetimiza mradi,
Ambao ulitubidi,
Arctic na Mediterranea.”

1363

“Mapato ya merikebu,
Kusema ni wajibu,
Yenu yashinda hesabu,
Za hasara zetu bia.”

1364

“Kama tusipolegea,
Twaweza kutazamia,
Siku zote kuzidia,
Vyombo vya kupigania.”

1365

“Jumla ya sabmarini,
Tulizozivunja chini,
Katibu wa baharini,
Akiri imezidia.”

1366

“Wakati ninapodhani,
Hatari ya sabmarini,
Kuwa kubwa vitani,
Tumaini hunijia.”

1367

“Tumaini hunijia,
Kuwa zitakazaniwa,
Sana kushambuliwa,
Mpaka zishindwe pia.”

1368

“Shambulio laongozwa,
Udachi kulieneza,
Kwa ndege za Kiingereza,
Na Amerika pamoja.”

1369

“Madege ya Amerika,
Mchana vita hushika,
Usiku kadhalika,
Yetu yanashambulia.”

1370

“Kwa vita tuliyo nayo,
Wingi ndiyo utakwao,
Kutimiza tutakayo,
Mchana na usiku pia.”

1371

“Marafiki kwa hewa,
Wamekwisha jiteua,
Kuliko Italia,
Udachi na Japania.”

1372

“Hivyo vita vya hewa,
Udachi na Japania,
Zilipenda kudhania,
Vitatisha dunia.”

1373

“Mapigano yaya haya,
Yaonya bila udhia,
Kuwa wenye hatia,
Kwanza wataangamia.”

1374

“Mkuu wa taadhima,
Watu wengine husema,
Maadui lazima,
Washindwe katika hewa.”

1375

“Wako watu wasemao,
Kuwa mwendo huo siyo,
Inapasa tegemeo,
Sana kuangaliwa.”

1376

“Lakini hapana shaka,
Wote mtakumbuka,
Udachi tumepeleka,
Hasara nyingi kwa hewa.”

1377

“Hili litaendelea,
Wadachi na Waitalia,
Watake kuchagua,
Wakatili kuondoa.”

1378

“Vita vyetu vya hewani,
Humfanya Jermani,
Kuhamisha ufichoni,
Viwanda vya kuundia.”

1379

“Tumekwisha kupatana,
Kuwa upesi sana,
Nguvu iliyoungana,
Tupeleke Japania.”

1380

“Tumepata ushahidi,
Japani kwa uhasidi,
Ameua makusudi,
Waamerika wa hewa.”

1381

“Watu wa vita wajibu,
Wafanye utaratibu,
Japani waiharibu,
Iwe jivu na makaa.”

1382

“Ishambuliwe kwa nguvu,
Miji iwe majivu,
Kabla ya utulivu,
Na amani kurejea.”

1383

“Katika mkutano,
Tufanyao mapatano,
Imelazimu mno,
Japani kufikiriwa.”

1384

“Taabu iliyotukuka,
Mbele ya Amerika,
Na Uingereza pulika,
Si majeshi kuandaa.”

1385

“Si mapato ya risasi,
Na eropleni za kasi,
Tunavyo bila kiasi,
Vitu hivi sikia.”

1386

“Shida inayotupasa,
Ni matumizi hasa,
Ya majeshi haya sasa,
Adui kumfanyia.”

1387

“Kufanyiza matumizi,
Ya watu na zana hizi,
Mbele ya pingamizi,
Ya sabmarini udhia.”

1388

“Majeshi kuyavusha,
Na bara kuyapitisha,
Habari ninawapasha,
Kuwa zina dhiki njia.”

1389

“Mashauri yetu yote,
Ya kuandaa tutete,
Vita vya pande zote,
Yafaa kuangaliwa.”

1390

“Wajibu kuangaliwa,
Jinsi yanavyokuwa,
Wakati wa kutumiwa,
Lazima kuchaguliwa.”

1391

“Yanapasa mambo hayo,
Yafanywe mbio mbio,
Ili mashambulio,
Yasizidi kuchelewa.”

1392

“Ni lazima kutendewa,
Ulaya na Asia,
Adui kutumia,
Nguvu zote mara moja.”

1393

“Basi mnapoolewa,
Taabu ninazowambia,
Njia za kutumia,
Heri kuchaguliwa.”

1394

“Mahali mwa kutumiwa,
Mwapasa kuchaguliwa,
Ili yapate tujia,
Mazao maridhawa.”

1395

“Kazi hii hutaka,
Maangalizi pulika,
Ya watu kukutanika,
Wakuu wa kuteua.”

1396

“Wakuu wa serikali,
Wa nchi hizi mbili,
Kukutana afadhali,
Wapate kuangalia.”

1397

“Watu wengi huweza,
Mashauri kufanyiza,
Lakini kuyatimiza,
Kwao ndiyo udhia.”

1398

“Laiti nisingetiwa,
Katika kazi sikia,
Ya cheo nilichopewa,
Mashauri ningetoea.”

1399

“Ningetoea mengi sana,
Mashauri ya maana,
Kisha ningekazana,
Mpaka yakatumia.”

1400

“Lakini hivi sasa,
Hoja ni ngumu hasa,
Kufua na kutakasa,
Hadharani si wasia.”

1401

“Hoja tutazitakasa,
Zilingane na visa,
Kadiri inavyopasa,
Faraghani tukitua.”

1402

“Si vizuri hasimu,
Siri zetu kufahamu,
Kwa hivi yatulazimu,
Hadhari kutumia.”

1403

“Mkuu wa taadhima,
Fahamu sitakimwa,
Kuja na wanachama,
Tena nikiamriwa.”

1404

“Naweza kuja nao,
Watu waelewao,
Na wako ulio nao,
Wakapatana pamoja.”

1405

“Zamani nilitamani,
Tukutane barazani,
Pamoja na Stalin,
Chiang Kai-Shek pia.”

1406

“Sikupata jambo hili,
Wala sijui mahali,
Ambapo pastahili,
Wao kuhudhuria.”

1407

“Mfano wenye imara,
Ulioleta tijara,
Kwa mashauri bora,
Umekwisha kutokea.”

1408

“Ushindi wa Afrika,
Kama tulivyotaka,
Sasa umekamilika,
Vizuri na sawasawa.”

1409

“Mwaka jana mwezi Juni,
Nipo hapa ugenini,
Karatasi ya huzuni,
Mimi ilinifikia.”

1410

“Ilikuwa na habari,
Mbaya isiyo kadiri,
Majeshi yetu kukiri,
Tobruk kujitolea.”

1411

“Wala haikuarifu,
Ishirini na tano elfu,
Watu katika safu,
Kisa cha kujitolea.”

1412

“Mara mliamru,
Kuyapeleka mafaru,
Kwa njia inayoduru,
Misri yakaingia.”

1413

“Sikizeni wasikizi,
Niwambie wazi wazi,
Mafaru yalifanya kazi,
Kubwa hata Tunisia.”

1414

“Hitler na Mussolini,
Hasara zao vitani,
Afrika kwa yakini,
Si ndogo mkiambiwa.”

1415

“Elfu tisa na hamsini,
Idadi ya wapigani,
Waliokufa vitani,
Na mateka wakawa.”

1416

“Tena toni za meli,
Ni milioni mbili,
Na mia nne kamili,
Elfu zilipotewa.”

1417

“Vyombo katika hewa,
Elfu nane sikia,
Mizinga ikatimia,
Sitini na tano mia.”

1418

“Ishirini na tano mia,
Hamsini ikitiwa,
Ni mafaru sikia,
Yao yaliyopotea.”

1419

“Na sabiini elfu,
Isiyo na upungufu,
Ni malori nadhifu,
Yaliyopotea pia.”

1420

“Jamii ya maamiri,
Wa bara na bahari,
Katika hii shari,
Sifa nitawatolea.”

1421

“Nawaarifu ya kuwa,
Amerika haikutoa,
Mtu wa kuteua,
Kuliko Eisenhower.”

1422

“Labda moyo dhaifu,
Ulio na upungufu,
Huwa si mkunjufu,
Furaha ikitokea.”

1423

“Wajibu kushukuru,
Kwa mambo yalivyoduru,
Ingawa yanayodhuru,
Mbele yanatungojea.”

1424

“Tushukuru wastani,
Tunayoona machoni,
Kisha tujiandaeni,
Kupinga yanayokuja.”

1425

“Tuandae taratibu,
Ili tuzuie taabu,
Nyingi zisizo hesabu,
Za bahari zote pia.”

1426

“Hitler amejaribu,
Russia kuiharibu,
Lakini kapata taabu,
Mwisho ataangamia.”

1427

“Tufanye yanayopasa,
Kwa haraka hivi sasa,
Ili tuweze hasa,
Kusaidia Russia.”

1428

“Nataka tusingahau,
Yatupasa mwaka huu,
Kufanya bidii kuu,
Tugawe shida Russia.”

1429

“Tuzigawe shida hizo,
Nzito wachukuazo,
Tuyavunje matatizo,
Mengi yaliyowendea.”

1430

“Tutachukua sehemu,
Shida zilizo ngumu,
Mungu atatukirimu,
Kuiokoa Russia.”

1431

“Wadachi na Japania,
Hasa walitazamia,
Vita vikikawia,
Wahuri watalegea.”

1432

“Yatupasa kukazana,
Kuivunja yao dhana,
Kama dhana nyingi sana,
Ambazo tumetangua.”

1433

Hotuba hii sikia,
Kila alipotulia,
Churchill kupumua,
Watu walishangilia.

1434

Watu walioweza,
Maadui kufukuza,
Mfalme kapendezwa,
Kwenda kuwaangalia.

1435

Mfalme mahashumu,
Hakuridhika kwa simu,
Mwenyewe aliazimu,
Safarini kujitia.

1436

Hakutoshwa na barua,
Safarini kajitia,
Kwenda kushangilia,
Watu wake mashujaa.

1437

Hakuagiza wakili,
Kulifanya jambo hili,
Hili lilstahili,
Mwenyewe kuhudhuria.

1438

Alikwenda akague,
Watu wake awajue,
Awape yeye mwenyewe,
Zawadi za ushujaa.

1439

Alifika Afrika,
Nishani akawavika,
Bora zilizotukuka,
Askari mashujaa.

1440

Eisenhower kapewa,
Nishani ya kuteua,
Yenye cheo na ulua,
Heshima ya ushujaa.

1441

Marejeo ya London,
Waziri wa Britani,
Mwezi thelathini Juni,
Watu kawahotubia.

1442

Hotubaye Churchill,
Alisema Guildhall,
Akashukuru fadhili,
Ambazo ametendewa.

1443

“Nafurahi kuungama,
Ninavyotendewa wema,
Katika zote huduma,
Msaada sikuhiniwa.”

1444

“Nashukuru msaada,
Nipatao kila muda,
Nyakati hizi za shida,
Kwa watu wa Britania.”

1445

“Kwa kazi niliyo nayo,
Niwapo mambo hayo,
Huja katika moyo,
Nia ya kuendelea.”

1446

“Tulitaka kwa hiari,
Kuwa katika shari,
Ili kukinga hatari,
Kubla ya kurukiwa.”

1447

“Bila ya kuwa tayari,
Tukawa katika shari,
Pasipo silaha nzuri,
Wala gharama kujua.”

1448

“Bila kujua gharama,
Tuliitikia hima,
Wito wa heshima,
Mara ulipotujia.”

1449

“Hatukupenda kuona,
Dhuluma wala hiana,
Bure pasipo maana,
Poland kutendewa.”

1450

“Tangu tulipoahidi,
Kuzuia uhasidi,
Nyuma hatukurudi,
Wala hatukulegea.”

1451

“Nyuma hatukutazama,
Kuvunja yetu heshima,
Wala hatukusimama,
Kwa woga na kutushiwa.”

1452

“Hatukutaka tijara,
Zawadi zilizo bora,
Nchi wala ujira,
Wala pato kuridhiwa.”

1453
"Miaka iliyopita,
Mitatu katika vita,
Hitler alipata,
Fahari kujitogoa."

1454
"Fahari alipata,
Kinywani ikatokota,
Kuwa aweza kufuta,
Miji katika dunia."

1455
"Hasara kuu za vitu,
Na maisha ya watu,
Zilikuwa fungu letu,
Bali tulivumilia."

1456
"Tulikabili makonde,
Kupigwa kila upande,
Makusudi tutende,
Ahadi tuliyotoa."

1457
"Tangu kuunganika,
Sisi na Amerika,
Tumepata kwa haraka,
Nguvu ya kutegemea."

1458
"Canada na Australia,
Na New Zealand pia,
Mara ziliposikia,
Wito zilitikia."

1459
"Afrika ya Kusini,
Pamoja na makoloni,
Zilijitia vitani,
Ili kutusaidia."

1460
"Kisha tulipata shime,
Ya vikosi vya waume,
Wenye nguvu na tume,
Mashujaa wa India."

1461
"Kwa radhi waliridhia,
Wito kuitikia,
Ili kuzuia baa,
Lililotisha dunia."

1462
"Hapajakuwa daima,
Katika dunia nzima,
Kiwashacho na kuuma,
Nacho kuumwa pia."

1463
"Dunia yatazamia,
Jambo hilo kutokea,
Katika historia,
Adui akizidiwa."

1464
"Katika mambo ya vita,
Hakika ina matata,
Afadhali kuyakata,
Mawazo yenye tamaa."

1465
"Kabla hayajakoma,
Maneno ninayosema,
Jambo moja lazima,
Watu kuwatangazia."

1466
"Kabla ya kuanguka,
Majani ya masika,
Mapigano yatawaka,
Makali Mediterranea."

1467
Vita vya Afrika,
Mara vilipoanuka,
Waingereza walishika,
Njia ya Italia.

1468
Walishika mitambo,
Eropleni na vyombo,
Kuisafirisha ng'ambo,
Kupita Mediterranea.

1469
Alitamka zamani,
Kujisifu Mussolini,
Kuwa haiwezekani,
Kupita Mediterranea.

1470
Muda ulipowadia,
Kushambulia Ulaya,
Ikawa Mediterranea.
Njia ya kupitia.

1471
Wahuri walisafiri,
Kwa ndege na manowari,
Wakashuka askari,
Kisiwa Pantellaria.

1472
Lampedusa na Sardinia,
Na vinginevyo visiwa,
Mara vilijitolea,
Shindo lilipoingia.

1473
Lilizidi shindo hili,
Bila kufanya zohali,
Likafika Sicily,
Karibu ya Italia.

1474
Meli thelathini mia,
Zilipata kutumiwa,
Kuchukua Wahuria,
Sicily kushambulia.

1475
Idadi ya wapigani,
Walioshuka kisiwani,
Mia moja na sitini,
Elfu mashujaa.

1476
Elfu kumi na nne,
Ni magari ya mashine,
Zaidi zana nyingine,
Ni mafaru sita mia.

1477

Mizinga ya askari,
Katika hii safari,
Iipata kwa kadiri,
Kumi na nane mia.

1478

Upesi bila kusita,
Nyuma zilifuata,
Zana nyingine za vita,
Kwa bahari na hewa.

1479

Majemadari hodari,
Eisenhower mashuhuri,
Alexander na Montgomery,
Mbele walitangulia.

1480

Kufika kwa watu hawa,
Na wengine mashujaa,
Vita vikali vikawa,
Katika hiki kisiwa.

1481

Upande wa Waingereza,
Nguvu ilitokeza,
Nyingi ya kushangaza,
Adui akalemewa.

1482

Yalipotokea haya,
Mambo niliyowambia,
Wahuri walichagua,
Kuonya Waitalia.

1483

Churchill na Roosevelt,
Waliandikisha hati,
Kuwaarifu umati,
Hatari ya Italia.

1484

Hati ya watu hao,
Ilisomwa kwa radio,
Ikaonya matokeo,
Watu wa Italia.

1485

Hati iliwachaguza,
Kutaka au kuiza,
Kwa maneno kutangaza,
Hivi wakaarifiwa:

1486

"Mkuu wa Amerika,
Na Churchill shirika,
Wawaarifu waraka,
Watu wa Italia."

1487

"Baada ya salamu,
Yawapasa kufahamu,
Kuwa tumeazimu,
Vita kuwaletea."

1488

"Majeshi ya Washirika,
Waingereza na Waamerika,
Silaha yameshika,
Chini ya Eisenhower."

1489

"Na makamo jemadari,
Alexander tayari,
Kuongoza hii shari,
Ndani ya Italia."

1490

"Haya yasingetokea,
Kwa watu wa Italia,
Kuma wasingeridhia,
Mussolini kuongoa."

1491

"Haya ni matokeo,
Hawa yafuatayo,
Ambayo mtu huyo,
Nduni yake kawatia."

1492

"Maongozi ya aibu,
Ndiyo yaliyoharibu,
Hutu ikawa wajibu,
Sisi kuwashambulia."

1493

"Mussolini kwa bilisi,
Kuwasanya wafuasi,
Wa kuharibu nafsi,
Na uhuru wa dunia."

1494

"Mussolini kawatia,
Vitani kushirikia,
Hababu alidhania,
Hitler kafanikiwa."

1495

"Juu ya kupotea,
Nguvu nyingi Italia,
Ya bahari na hewa,
Hiana mmefanyiwa."

1496

"Mmetendewa hiana,
Kutwaliwa wenu wana,
Na meli nyingi sana,
Hata majeshi ya hewa."

1497

"Msaada ilipewa,
Udachi kutumia,
Ili ishinde Russia,
Misri hata dunia."

1498

"Umoja wa ubazazi,
Walioubuni Nazi,
Makusudi kuwahizi,
Haufai Italia."

1499

"Watu wa maendeleo,
Elimu na mapokeo,
Ya kale tuheshimuyo,
Ajabu kughilibiwa."

1500

"Askari Taliani,
Wamepigana vitani,
Kwa bidii moyoni,
Lakini wamehiniwa."

1501

“Wadachi waliwahini,
Kwa kuacha Taliani,
Peke yao mipakani,
Afrika na Russia.”

1502

“Tamaa ya Jermani,
Ya kushinda duniani,
Imepeperushwa chini,
Sasa katika dunia.”

1503

“Hewa ya Italia,
Imekwisha tawaliwa,
Na majeshi ya hewa,
Ya mataifa huria.”

1504

“Na pwani ya Taliani,
Imekuwa hatarini,
Kwa nguvu ya Britani,
Na Amerika pamoja.”

1505

“Mbele yamewakabili,
Majeshi yetu makali,
Yaliyoahidi kweli,
Kuivunja enzi mbaya.”

1506

“Enzi bure iuayo,
Watu waichukiayo,
Majeshi hayo yajayo,
Yanua kutangua.”

1507

“Enzi isiyo maana,
Inayodai ubwana,
Twanuia kupigana,
Mpaka kuuzuliwa.”

1508

“Hatutaki kuiona,
Enzi isiyo maana,
Ya viongozi fitina,
Kuwa katika dunia.”

1509

“Mkitaka pumziko,
Tumaini bado liko,
Majeshi yaliyo huko,
Kwetu yakijitolea.”

1510

“Mtakapo masalia,
Ya nchi ya Italia,
Kwetu mkijitolea,
Heshima mtapewa.”

1511

“Kama mkiendelea,
Wadachi kusaidia,
Mateso yatawajia,
Yawapasa kuchagua.”

1512

“Kama mtafanya hamu,
Kusaidia hasimu,
Vita vitalazimu,
Nchi ya Italia.”

1513

“Hatupendi kuwaudhi,
Wala sisi haturidhi,
Katika yenu ardhi,
Vita kuwaletea.”

1514

“Kuleta uharibifu,
Katika nchi nadhifu,
Twaona ni takilifu,
Nchi yenu kutokea.”

1515

“Lakini tumeazimu,
Kuangamiza hasimu,
Wuo na yao elimu,
Yetu msiporidhia.”

1516

“Juani kila dakika,
Vita hivi mkishika,
Kuzuia Washirika,
Hasara yaendelea.”

1517

“Kila tone la sadaka,
La damu inayotoka,
Yuwapasa kukumbuka,
Jambo moja huandaa.”

1518

“Huandaa ukimbizi,
Wa wakuu wa Nazi,
Wasipate maamuzi,
Yu dhuluma na hatia.”

1519

“Mambo mtazamiayo,
Pamoja na mapokeo,
Yote mliyo nayo,
Nazi wameyabukua.”

1520

“Waongozi wanafiki,
Waovu wasio haki,
Wameliletea dhiki,
Taifa la Italia.”

1521

“Salama ya Italia,
Mkitaka kutokea,
Lazima kukataliwa,
Waongozi wabaya.”

1522

“Hilo likitokea,
Italia itapewa,
Cheo cha kuheshimiwa,
Cha mataifa huria.”

1523

“Wakati umewadia,
Kwa watu wa Italia,
Mpate jirudishia,
Heshima ya mazoea.”

1524

“Kama mkichagua,
Kuishi kwa Italia,
Na amani ya dunia,
Twapenda kuarifiwa.”

1525
"Au kama mwatamani,
Kufa kwa Mussolini,
Na Hitler Jermani,
Wakatabahu barua."

1526
Hayo yaliposemwa,
Kabla kupita juma,
Kuongoza alikoma,
Mussolini Italia.

1527
Mussolini alikuja,
Enzini kama kioja,
Ishirini na moja,
Miaka akatumia.

1528
Alifanywa kiongozi,
Akawa katika enzi,
Ambaye wake wazazi,
Kwanza hawakutumia.

1529
Mfalme wa Italia
Huyo alimridhia
Kuongoza kila njia,
Pasipo kushauriwa.

1530
Hadhi ya usultani,
Alipata Mussolini,
Akashika sukani,
Zote za Italia.

1531
Watu aliwaongoza,
Katika njia za kiza,
Akajidai kuweza,
Kupigana na dunia.

1532
Alitumia makamo,
Ovyo pasipo kipimo,
Hata yakapita kimo,
Cha hadhi aliyopewa.

1533
Ngazi aliyopanda,
Kushuka ilimshinda,
Kwa mambo aliyotenda,
Ya kuchukiza dunia.

1534
Ngazini aliponyoka,
Asipate pa kushika,
Ghafla akaanguka,
Jina likapotea.

1535
Angeishi kiungwana,
Angalitukuka jina,
La watu kupokezana,
Italia na dunia.

1536
Hayo kuwa matokeo,
Na mwisho wa mtu huyo,
Pietro Badoglio,
Uongozi alipewa.

1537
Pietro Badoglio,
Maarufu mtu huyo,
Ajulikana kwa cheo,
Amiri Jeshi shujaa.

1538
Mfalme wa enzi,
Halafu alibarizi,
Kuwambia mageuzi,
Watu wake Italia.

1539
"Watu wa Italia,
Nawaarifu ya kuwa,
Leo nimejitwalia,
Mamlaka Italia."

1540
"Amri ya askari,
Wenye silaha za shari,
Leo nawapa habari,
Mwenyewe nimechukua."

1541
"Saa hii ya majonzi,
Nimeshika uongozi,
Raia wote wa enzi,
Wajibu kuvumilia."

1542
"Kila mtu ajiweke,
Imara mahali pake,
Ahadi yake ashike,
Kutetea Italia."

1543
"Mambo ya upotofu,
Kuitia nchi hofu,
Habari nawaarifu,
Samaha hayatapewa."

1544
"Mambo ya kugombana,
Kutia nchi fitina,
Yatapatilizwa sana,
Mara yakigunduliwa."

1545
"Yapasa kuvumilia,
Majeraha kuchukua,
Ambayo yanapasua,
Nchi ya Italia."

1546
"Kwa majeshi hodari,
Ya silaha za shari,
Na nia ya ujasiri,
Itapona Italia."

1547
"Watu wa Italia,
Ahadi ninawambia,
Najiunga na raia,
Kuokoa Italia."

1548
Mfalme wa cheo,
Kwisha kutamka hayo,
Waziri Badoglio,
Akasema na raia.

1549

“Mfalme kakubali,
Niongoze Serikali,
Mamlaka kamili,
Nimekwisha kabidhiwa.”

1550

“Vita yaendelea,
Nchi ya Italia,
Ambayo zake wilaya,
Mno zimejaribiwa.”

1551

“Neno tulilotamka,
La ahadi tutashika,
Japo miji yavunjika,
Hatutabadili nia.”

1552

“Hayo ndiyo mapokeo,
Ya kale tufuatayo,
Kuacha njia hiyo,
Sawa na kupotea.”

1553

“Jipangeni kiume,
Kando ya Mfalme,
Tena fanyeni shime,
Kuokoa Italia.”

1554

“Amri zimetolewa,
Mtu akizipotoa,
Afahamu ya kuwa,
Lazima kuadhibiwa.”

1555

Hayo yalipodhihiri,
Jemadari wa Wahuri,
Akatangaza habari,
Ya amani Italia.”

1556

Jemadari Eisenhower,
Amani aliyotoa,
Kwa watu wa Italia,
Maneno yake ni haya:

1557

“Watu wa Italia,
Sisi twawashangilia,
Tangu mlipochagua,
Mussolini kumwondoa.”

1558

“Mtu huyo alivuta,
Nchi katika vita,
Hitler akapata,
Kiti cha kukalia.”

1559

“Zuio lililotenga,
Sisi nanyi kujiunga,
Urafiki tukajenga,
Wenyewe mmeondoa.”

1560

“Jambo lililobakia,
Ni Wadachi kutolewa,
Ili isafike njia,
Ya amani Italia.”

1561

“Kama amani mwataka,
Mtapata kwa haraka,
Bora yenye kutukuka,
Ya serikali huria.”

1562

“Twaja kama wakombozi,
Sehemu yenu ya kazi,
Komeni masaidizi,
Wadachi kuwafanyia.”

1563

“Hili likisha kuwa,
Wadachi tutawatoa,
Na vita hivi vibaya,
Vitakoma Italia.”

1564

“Kama katika Sicily,
Haitakuwa kali,
Yetu sisi serikali,
Nanyi mtakirimiwa.”

1565

“Watu watarudia,
Maisha ya mazoea,
Mahabusi Wahuria,
Kama tutarudishiwa.”

1566

“Maelfu na mamia,
Mahabusi wa Italia,
Wa Sicily na Tunisia,
Kwao watarejea.”

1567

“Uhuru wenu wa kale,
Na mapokeo teule,
Yaliyo bora milele,
Yote mtarudishiwa.”

1568

“Msifanye ghaidhi,
Zaidi mkajiudhi,
Mtarudishiwa hadhi,
Kamili ya asilia.”

1569

Halafu yake sikiza,
Barazani Uingereza,
Churchill kaeleza,
Mambo yaliyotokea.

1570

“Baraza itasikia,
Kwa uradhi nadhanja,
Kuwa amevunjikiwa,
Mussolini Italia.”

1571

“Katika wahalifu,
Mussolini maarufu,
Wa vita hivi vichafu,
Vilivyoleta ukiwa.”

1572

“Imevunjika msingi,
Enziye ya muda mwingi,
Iliyomwaga rangi,
Ya damu ya Italia.”

1573

“Mambo yatatokea,
Lakini hatujajua,
Nini litaangukia,
Wadachi Italia.”

1574

“Ujinga na manza,
Ambayo amefanyiza,
Mussolini yametoza,
Ghali Waitalia.”

1575

“Sasa yamekwisha fika,
Majeshi ya Washirika,
Waingereza na Waamerika,
Milango ya Italia.”

1576

“Majeshi kila namna,
Tayari kwa kupigana,
Yamesimama na zana,
Sasa zinazotumiwa.”

1577

“Ni majeshi yaya haya,
Ambayo yataokoa,
Nchi ya Italia,
Amani ikichagua.”

1578

“Majeshi yanayokuja,
Yataipa faraja,
Na uhuru mara moja,
Nchi ya Italia.”

1579

“Na baadaye kitambo,
Tukisha tengeza mambo,
Itashirikia umbo,
La heshima ya Ulaya.”

1580

“Naona hapana shaka,
Waitalia wataka,
Watolewe kwa haraka,
Wadachi Italia.”

1581

“Waitalia naona,
Kuwa wataka sana,
Watengane na mabwana,
Ambao wawasumbua.”

1582

“Wanataka uokofu,
Katika uharibifu,
Uhuru na utukufu,
Wapate jirudishia.”

1583

“Watakapo mambo hayo,
Wanaweza kuwa nayo,
Hiari wanayo wao,
Mikononi wamepewa.”

1584

“Serikali ya Italia,
Wadachi ikiwachia,
Hatuna la kuchagua,
Ila kuishambulia.”

1585

“Nchi ya Taliani,
Itakuwa vitani,
Kasikazini na kusini,
Baharini na kwa hewa.”

1586

“Tena tutajitahidi,
Kufanya yanayobidi,
Nguvu ya vita izidi,
Juu ya Italia.”

1587

“Amri ya mambo hayo,
Hivi sasa nisemayo,
Majemadari wanayo,
Imekwisha kutolewa.”

1588

“Italia ikisema,
Kuwa yataka utumwa,
Wa Wadachi lazima,
Halidhuru Wahuria.”

1589

“Halitabadili mwendo,
Wala kupunguza kondo,
Ila litazidi shindo,
La vita Italia.”

1590

“Miezi haba ijayo,
Itachomwa nchi hiyo,
Hata yaje matokeo,
Ya kiza na fadhaa.”

1591

“Mabadiliko ya mambo,
Yatachukua kitambo,
Ndipo yapate umbo,
La nia ya Italia.”

1592

“Na njia ifaayo,
Kuhimiza nia hiyo,
Ni kufanya shambulio,
La nguvu kuendelea.”

1593

“Shambulio likidumu,
Labda watafahamu,
Kuwa imewalazimu,
Wadachi kuwakataa.”

1594

“Wakipigwa kila siku,
Kwa chuma na simaku,
Hamu yao na shauku,
Ya vita itakimbia.”

1595

“Neno moja la hadhari,
Kuambia ni vizuri,
Mambo yaliyodhihiri,
Kwanza hatukuyajua.”

1596

“Hatukuwa na habari,
Wala hatukufikiri,
Italia itakiri,
Mussolini kumwondoa.”

1597
"Tangu ulipovunjika,
Uwezo alioshika,
Tusijinyime baraka,
Kupatana na Italia."

1598
"Sisi hatukutafuta,
Kuisaliti na vita,
Hata iweze kupata,
Italia kupotea."

1599
"Hatukutaka kuona,
Mtu hakubaki tena,
Awezaye kupatana,
Na sisi Italia."

1600
"Faida ya Italia,
Na watu wa uhuria,
Kama ingejitolea,
Bila neno zaidia."

1601
"Hilo kuwezekana,
Ama kutowezekana,
Sasa ni mapema sana,
Siri hiyo kuijua."

1602
"Lo lote likitokea,
Wajibu kukumbukia,
Adui wa uhuria,
Mkubwa si Italia."

1603
"Udachi ndiyo adui,
Wala vita havitui,
Kila tukiwa hai,
Mpaka ishindwe pia."

1604
"Mambo yanayotendeka,
Twayafanya kwa shirika,
Uingereza na Amerika,
Zote hushirikia."

1605
"Na marafiki Russia,
Daima huarifiwa,
Kila linalotokea,
Hawakosi kuambiwa."

1606
"Serikali Uingereza,
Na Amerika sikiza,
Shauri likifanyizwa,
Daima hushauriwa."

1607
"Na ruhusa nimepewa,
Ya kuandika barua,
Kwa Roosevelt sikia,
Kila siku nawambia."

1608
"Katika kumi sehemu,
Za nguvu ya hasimu,
Italia ni sehemu,
Moja tu ilikuwa."

1609
"Tumaini la Wadachi,
Kuchafuka haliachi,
Kwa matokeo mabichi,
Yaliyomo Italia."

1610
"Tamaa ya Jermani,
Juu ya sabmarini,
Kushindia vitani,
Chini inadidimia."

1611
"Inadidimia chini,
Kama sabmarini,
Tuvunjazo baharini,
Kila dakika na saa."

1612
"Na mapigano ya kasi,
Mipakani mwa Urussi,
Huangamiza watesi,
Wa Wadachi vibaya."

1613
"Mavunjiko ya miji,
Yanakwenda kama maji,
Wala hayawafariji,
Wadachi Ulaya."

1614
"Na nia ya uasi,
Inakua kwa upesi,
Na kutia wasi wasi,
Nchi walizochukua."

1615
"Bali tujihadharishe,
Tena tujikumbushe,
Kazi tusiidunishe,
Ambayo tumeingia."

1616
"Nguvu ya Jermani,
Bado kushuka chini,
Na majeshi hesabuni,
Bado sana kupungua."

1617
"Maisha ya Serikali,
Ya Wadachi ni kamili,
Kisha wana mahali,
Na nchi za kutumia."

1618
"Na zana za shambulizi,
Zilizobaki kwa Nazi,
Sikilizeni wasikizi,
Nzito juu ya Ulaya."

1619
"Nia tuliyo nayo,
Ni kuvunja nguvu hiyo,
Adui aliyo nayo,
Itoweke Ulaya."

1620
Roosevelt sikiliza,
Halafu alitangaza,
Mambo yaliyotokeza,
Sicily kama haya:

1621

"Zuio la ushupavu,
Lilionyesha nguvu,
Mbele ya Jeshi kavu,
La Nane la Wahuria."

1622

"Jambo hili halikuwa,
Jipya kwa mashujaa,
Kwa sababu ya tabia,
Ya vita kuizoea."

1623

"Kwa vita kuvizoea,
Jeshi hili lilitia,
Hasara kwa kuchelewa,
Wadachi kujitolea."

1624

"Jeshi la Amerika,
La saba lilipofika,
Kisiwani likashuka,
Palermo likachukua."

1625

"Sicily na Tunisia,
Uongo zimetangua,
Kusema haziwi bia,
Amerika na Britania."

1626

"Habari ya kuzuliwa,
Imekwisha gunduliwa,
Dunia sasa yajua,
Tunaweza kuwa bia."

1627

"Na katika matokeo,
Ya wakati ujao,
Ndani tutakwenda nao,
Waingereza pamoja."

1628

"Kama katika Sicily,
Tulivyoonyesha kweli,
Pamoja tutakabili,
Kila linalotokea."

1629

"Vita vitaendelea,
Juu ya Waitalia,
Hata waweze elewa,
Bure wanajizuzua."

1630

"Vita vitawashukia,
Hata wawe waelewa,
Batili ya kugombea,
Upande wenye hatia."

1631

"Ufa wa kwanza,
Umekwisha jitokeza,
Tangu alipoteleza,
Mussolini Italia."

1632

"Hitler alimuhini,
Msaada Mussolini,
Ndipo alipobaini,
Kuwa amevunjikiwa."

1633

"Kwa watu kuwadhiki,
Mussolini haokoki,
Yeye na marafiki,
Zake wataadhibiwa."

1634

"Hapana mhalifu,
Apataye uokofu,
Wala adhabu hafifu,
Kwa kazini kujitoa."

1635

Heri tufuate nyayo,
Za mambo na matokeo,
Makusudi tusemayo,
Yazidi kutuelea.

1636

Wajibu wetu kujua,
Muda uliotumiwa,
Sicily kupiganiwa,
Na hasara za kisiwa.

1637

Yalidumu mapambano,
Ya makali mapigano,
Muda majuma matano,
Na siku tatu pamoja.

1638

Mapigano yalidumu,
Mazito tena magumu,
Wengi wakenda kuzimu,
Wengi wakajeruhiwa.

1639

Adui alizidiwa,
Na nguvu ya Wahuria,
Kila siku kisiwa,
Kikawa chachukuliwa.

1640

Mwisho alijaribu,
Kuvuka kwa merikebu,
Mia tatu hesabu,
Vyombo vikaharibiwa.

1641

Vyombo thelathini mia,
Ghafla vilipotea,
Pamoja na abiria,
Ndani waliokuwa.

1642

Adui hakuungama,
Watu waliozama,
Lakini ukitazama,
Salama haikuwa.

1643

Watu wengi walizama,
Wakati wa kuhama,
Hata kama alisema,
Kuwa alifanikiwa.

1644

Inaelewa bahari,
Wingi wa askari,
Ambayo yao makaburi,
Majini yalitokea.

1645

Hasara za wanafiki,
Katika kisiwa hiki,
Ni watu moja laki,
Na elfu zaidia.

1646

Sitini na saba elfu,
Hufanya ukamilifu,
Wa watu katika safu,
Wao waliopotea.

1647

Mizinga mia tano,
Katika msukumano,
Haikufaulu neno,
Ila iliwapotea.

1648

Mia mbili na sitini,
Mafaru ya Jermani,
Yaliyokuwa vitani,
Yaliangamia pia.

1649

Madege yake adui,
Yaliyokosa uhai,
Jumla haipungui,
Kumi na saba mia.

1650

Maelfu ya magari,
Na akiba za tayari,
Walishika Wahuri,
Katika hiki kisiwa.

1651

Jeshi la Waitalia,
Katika hiki kisiwa,
Zima liliangamia,
Bila mtu kubakia.

1652

Jumla ya wapigani,
Waliokuwa jeshini,
Ni mia na thelathini,
Elfu Waitalia.

1653

Tangu kuwa mapigano,
Jeshi hili ni la tano,
Ambalo kwa mfano,
Kabisa lilipotea.

1654

Kumi na saba mia,
Mizinga ilipotea,
Mafaru yakatimia,
Hamsini na mia.

1655

Ishirini na sita elfu,
Ni Wahuri wapungufu,
Katika zao safu,
Zaidi ni tisa mia.

1656

Wakati iliposhikwa,
Sicily na Washirika,
Aliandika waraka,
Mfalme wa Britania.

1657

Burua ya Mfalme,
Nakariri muisome,
Waelewe wanaume,
Na wanawake pamoja.

1658

"Nakuarifu barua,
Jemadari Eisenhower,
Kuwa nimependezewa,
Slcily kufanikiwa."

1659

"Wewe na askari,
Chini yako Jemadari,
Moyo waona fahari,
Wote kuwashangilia."

1660

"Katika milki nzima,
Tulipenda kutazama,
Maendeleo mema,
Namna yalivyokuwa."

1661

"Wote tumefurahiwa,
Kwa kuona ya kuwa,
Mwendo uliotumiwa,
Umefaulu njia."

1662

"Tena ningependezwa,
Watu wangu ukiweza,
Wakanada na Waingereza,
Wote kunisalimia."

1663

"Wote wape habari,
Kuwa naona fahari,
Ya shirika yao nzuri,
Hata ushindi ukawa."

1664

Sicily ilipotekwa,
Wahuri walivuka,
Majeshi yakashuka,
Bara ya Italia.

1665

Yalivuka Messina,
Kwenda ng'ambo kupigana,
Shindo kubwa sana,
Likavuma Italia.

1666

Italia ilitaka,
Katika vita kutoka,
Wajumbe ikapeleka,
Amani kutaradhia.

1667

Ilipeleka wajumbe,
Kwa siri wakaombe,
Kuwa tena wasigombe,
Na mataifa huria.

1668

Wajumbe wa mashauri,
Hawakuwa na hiari,
Ila amani kukiri,
Bila neno zaidia.

1669

Mwezi tatu Septemba,
Mwaka wa tano kugomba,
Amani waliyoomba,
Mikono ilitiwa.

1670

Amani hii ya siri,
Iilitiwa muhuri,
Mbele ya majemadari,
Alexander na Eisenhower.

1671

Sicily ilijiteua,
Kuwa ndicho kisiwa,
Amani ya Italia,
Mikono ilipotiwa.

1672

Mwezi nane Septemba,
Eisenhower simba,
Akatangaza ya kwamba,
Amani ameitoa.

1673

Admeli mahashumu,
Andrew Cunningham,
Alitangaza salamu,
Kuonya Waitalia.

1674

Aliwaonya shauri,
La kutaka manowari,
Zende katika bandari,
Za nchi za uhuria.

1675

Meli na manowari,
Ambazo zilisafiri,
Kwenda nchi za uhuri,
Zinapata mja moja.

1676

Vyombo hivi vya kuteta,
Viliwasili Malta,
Ambako aliviita,
Cunningham shujaa.

1677

Wadachi walitaka,
Vyombo hivi kuvishika,
Lakini viliponyoka,
Kitanzi walichotia.

1678

Badoglio katoa,
Kwa watu wa Italia,
Tangazo la kuwambia,
Amani ilivyokuwa.

1679

“Serikali ya Italia,
Yamkini yaelewa,
Ni dhiki kuendelea,
Kupigana na huria.”

1680

“Kwa kuepuka madhara,
Na zaidi ya hasara,
Imeona kuwa bora,
Amani kutaradhia.”

1681

“Haja iliyotakiwa,
Eisenhower katoa,
Na nchi ya Italia,
Amani imepewa.”

1682

“Vita kati ya huria,
Na watu wa Italia,
Wajibu sasa kutua,
Amri imetolewa.”

1683

“Watu wa Italia,
Wajibu kujitetea,
Kama watashambuliwa,
Na adui wa huria.”

1684

Wakati wa jambo hili,
Roosevelt na Churchill,
Walikuwa mahali,
Pamoja wamekaa.

1685

Walikuwa Amerika,
Hili lilipofanyika,
Habari ilipofika,
Wote wakafurahiwa.

1686

Amani waliyopewa,
Watu wa Italia,
Ukitaka kuelewa,
Masharti yake haya:-

1687

*Corsica na Italia,
Lazima kujitolea,
Kwa mataifa huria,
Kwa vita kuendeshea.*

1688

*Bandari za Italia,
Na viwanja vya hewa,
Lazima kudhaminiwa,
Kwa Wahuri kutumia.*

1689

*Mahabusi Wahuria,
Lazima kurudishiwa,
Bila mtu kupungua,
Udachi kuchukuliwa.*

1690

*Manowari za Italia,
Na majeshi ya hewa,
Yende yalikoambiwa,
Na Admeli huria.*

1691

*Serikali za shari,
Jemadari mhuri,
Atachagua pazuri,
Pa kukaa Italia.*

1692

*Italia yaahidi,
Amani inavyobidi,
Kufanya jitihadi,
Wahuri kuwaridhia.*

1693

*Serikali ya Italia,
Lazima kuridhia,
Majeshiye kutumia,
Kutimiza mambo haya.*

1694

Halafu Badoglio,
Alifanya mafunuo,
Ya serikali yao,
Akasema kama haya:

1695

"Mara wakiondolewa,
Wadachi Italia,
Italia itakuwa,
Nchi ya uhuria."

1696

"Majeshi yaliyo hapa,
Kiapo yameapa,
Mfalme kumpa,
Msaada na himaya."

1697

"Amani ya Italia,
Wadachi waichukia,
Na hili linapanua,
Hasama kuendelea."

1698

"Hasama kuendelea,
Ndivyo itakavyokuwa,
Baina ya Italia,
Na Wadachi kwa haya."

1699

"Amani tumekubali,
Tuepuke idhilali,
Wala hatutajali,
Lawama kulaumiwa."

1700

"Siku zote Jermani,
Walilidunisha chini,
Taifa la Taliani,
Mateso likatendewa."

1701

"Mateso lilitendewa,
Makubwa kuvumilia,
Likahe sabiwa kuwa,
Duni katika dunia."

1702

"Italia yakumbuka,
Kuwa ilipeleka,
Majeshi vita kushika,
Ufaransa na Russia."

1703

"Iipeleka vikosi,
Nchi za Balkans,
Na kila penye utesi,
Wadachi kupiganiwa."

1704

"Hayo yalipofanyika,
Wadachi walizunguka,
Mali zetu wakashika,
Heshima tukavunjiwa."

1705

"Tulivunjiwa heshima,
Tukawa kama wanyama,
Tusile chakula chema,
Ila haba na kibaya".

1706

"Walitupa mashaka,
Mazito kuchukulika,
Ambayo yatakumbukwa,
Milele Italia."

1707

"Wadachi waliyotenda,
Yatia moyo kidonda,
Watu tuliowapenda,
Kutubadilia nia!"

1708

"Kuungama si haramu,
Masharti ni magumu,
Lakini ililazimu,
Kuokoa Italia."

1709

"Ingawaje ni magumu,
Ni kizuio cha damu,
Ya Italia fahamu,
Bure kujimwagikia."

1710

"Mwombaji hana haba,
Wala hana takiriba,
Japo kidogo hushiba,
Hayavuti maridhawa."

1711

"Mwombaji hachagui,
Hataki ile na hii,
Apewacho hukinai,
Si haba tuliyo pewa."

1712

"Haja yetu mashuhuri,
Kutoka katika shari,
Tusitete na Wahuri,
Jambo hili limekuwa."

1713

"Tena wajibu kujua,
Imeshindwa Italia,
Basi afadhali haya,
Kuliko kuangamia."

1714

"Mungu apendalo kuwa,
Hapana wa kuzuia,
Wala halina dawa,
Ngao ya kukingia."

1715

"Na dhiki wameumbiwa,
Watu kuvumilia,
Na haya yaliyokuwa,
Ndiyo yetu majaliwa."

1716

"Siku zote dhiki ngumu,
Apatapo mwanadamu,
Huwa kama mwalimu,
Wa kumwongoza njia."

1717

"Mshindwa anapotii,
Hutoweka uadui,
Kwa hivi amani hii,
Yaokoa Italia."

1718

"Thamani yake amani,
Hivi sasa hamwoni,
Lakini natumaini,
Mwisho mtapendezewa."

1719

"Kwa kutoka shirikani,
Sisi na Jermani,
Ninayo matumaini,
Nafuu itatujia."

1720

"Itatujia nafuu,
Dhiki yetu tusahau,
Jipeni moyo mkuu,
Hapana lisilokuwa."

1721

"Hapana lisilokuwa,
Itapona Italia,
Na watu watarudia,
Maisha ya mazoea."

1722

"Wajibu ni kusimama,
Tupigane na hasama,
Tumekuwa wanachama,
Wa mataifa huria."

1723

Roosevelt alitoa,
Maneno kama haya,
"Amani ya Italia,
Ni ushindi wa huria."

1724

"Sasa hatutaweza,
Amani kuitukuza,
Mpaka kuwafukuza,
Wadachi Italia."

1725

"Kwanza imetupasa,
Kuwatoa Ufaransa,
Tena tuwapige hasa,
Udachi wanakokaa."

1726

Smuts alieleza,
"Ushindi wa Waingereza,
Italia umegeuza,
Hali ya vita Ulaya."

1727

"Ushindi wetu Russia,
Na juu ya Italia,
Waonyesha yakuwa,
Twendako twakaribia."

1728

"Mbele tunasogea,
Na karibu tutakuwa,
Twapigana na mdawa,
Katika ngome Ulaya."

1729

"Mwisho haujakuwa,
Lakini twakaribia,
Kituoni kuingia,
Yukiwapo majaliwa."

1730

Amani ilipokuja,
Watu walijipambaja,
Kwa furaha na faraja,
Katika Italia."

1731

Mukanisa yalijaa,
Watu kuomba madua,
Shukurani wakatoa,
Kwa amani kuwajia."

1732

Furaha iliwajaa,
Watu wengi wakalia,
Kuona wamejitoa,
Shimoni walimokuwa."

1733

Machози yaliwatoka,
Kwa furaha na kucheka,
Kuona wameepuka,
Urafiki wa hadaa."

1734

Wafaransa kadhalika,
Nao walifurahika,
Habari ilipofika,
Kwao walishangilia."

1735

Habari ilipofika,
Italia imetoka,
Kwa Wadachi ushirika,
Mikado alishangaa."

1736

Alishangaa sana,
Asipate la kunena,
Meno akayatafuna,
Kwa hasira kumjaa."

1737

Yeye na Waziri Tojo,
Waliona kuwa fujo,
Kubwa sana la machinjo,
Japani lakaribia."

1738

Waliona ya kuwa,
Vyombo vya Waitalia,
Lazima vitatumiwa,
Japani kushambulia."

1739

Waliona majilio,
Ya mapigano Tokio,
Yamo katika mbio,
Karibu kuwafikia."

1740

Waliona ya kama,
Wahuri wamesimama,
Sasa juu ya mlima,
Japani imenamiwa."

1741

Walifanyiza baraza,
Faraghani ya kuwaza,
Wajue la kufanyiza,
Wakati ukiwadia.

1742

Wadachi walichukiwa,
Kwa amani hii kuwa,
Wakalaumu ya kuwa,
Hiana wametendewa.

1743

Serikali ya Badoglio,
Ilisemwa kuwa ndiyo,
Iliyoyatenda hayo,
Sana ikalaumiwa.

1744

Amani ilipotoa,
Vitani Waitalia,
Nchi yao ilikuwa,
Mikononi mwa mdawa.

1745

Wadachi hawakupenda,
Kuonyesha wameshindwa,
Kwa hivi walijipinda,
Kupigana Italia.

1746

Waitalia walipewa,
Habari ya kuwa,
Majeshi ya uhuria,
Yanashuka Italia.

1747

Jemadari Eisenhower,
Aliahidi ya kuwa,
Kama watasaidia,
Msaada watapewa.

1748

Majeshi ya watesi,
Yasiyo na wasiwasi,
Yalishuka Naples,
Nchi ya Italia.

1749

Walishuka askari,
Saa za alfajiri,
Mizinga ya manowari,
Ikawapa hamaya.

1750

Majeshi ya uhuria,
Kati ya Italia,
Viongozi walikuwa,
Watu wa kuteuliwa.

1751

Mbele alitangulia,
Alexander shujaa,
Mtu wa pili akawa,
Mark Clark sikia.

1752

Wa tatu Montgomery,
Jemadari mashuhuri,
Aliye shujaa tayari,
Kusini mwa Italia.

1753

Clark Mwamerika,
Shujaa alisifika,
Si mtu wa kustuka,
Vitani akitokea.

1754

Montgomery na Alexander,
Nyuma kidogo tukenda,
Ni watu walioshinda,
Sicily na Tunisia.

1755

Kuwasili nchi kavu,
Majeshi yao ya nguvu,
Wahuri na washupavu,
Katika vita wakawa.

1756

Wadachi walisaki,
Ndani ya mahandaki,
Kuwangoja Marafiki,
Nchi wasiyojua.

1757

Wahuri hawakusita,
Walivikabili vita,
Njia yao wakakata,
Kati ya matata haya.

1758

Wahuri Jeshi la Tano,
Walipofika Salerno,
Watu wa mapigano,
Damu waliogelea.

1759

Waliogelea damu,
Kwa mapigano magumu,
Kila upande fahamu,
Hodari ulizua.

1760

Mark Clark alifika,
Hata katika mpaka,
Kuwambia Washirika,
Wazidi kushikilia.

1761

Vikosi vyenye ngao,
Vilishuka mwambao,
Kuyapa tegemeo,
Majeshi ya uhuria.

1762

Manowari madhubuti,
Warspite na Valiant,
Zilisukuma kati,
Mizinga kusaidia.

1763

Ilipigwa baharini,
Mizinga hiyo jueni,
Ikafika shabahani,
Kama ilivyonuiwa.

1764

Tena katika hewa,
Adui hakuachiwa,
Mapigano kila saa,
Yakawa yaendelea.

1765

Aliporudi Kwebeki,
Baraza ya Marafiki,
Kasema na halaiki,
Churchill kama haya:-

1766

“Ndege tuzitakazo,
Sasa tunazo kwa mzo,
Kuliko walizonazo,
Wadachi na Japania.”

1767

“Wingi ukiendelea,
Wakati utatokea,
Wa kuvunja sawasawa,
Kila nyumba ya mdawa.”

1768

“Miezi iliyopita,
Minne hazikupata,
Hasara wala matata,
Meli tunazotumia.”

1769

“Hasara za Japania,
Za habari na hewa,
Kubwa sana zimekuwa,
Vigumu kubadiliwa.”

1770

“Louis Mountbatten,
Atafanya masikani,
Makubwa ya wapigani,
New Delhi India.”

1771

“Huko yeye atakuwa,
Vita anaviandaa,
Juu ya Japania,
Kama Eisenhower.”

1772

“Vita Mediterraneo,
Msidhani kuwa ndiyo,
Badala ya shambulio,
La Wahuri Ulaya.”

1773

“Hivi vilikusudiwa,
Kwanza kutangulia,
Mpaka Italia,
Vingine vyaandaliwa.”

1774

“Vikosi vya Amerika,
Kwa hewa vingalishuka,
Kama visingalishikwa,
Rumi viwanja vya hewa.”

1775

“Adui alitangulia,
Viwanja kuvizujia,
Ndipo ukashindwa kuwa,
Mwendo ulionuiwa.”

1776

“Stalin alitoa,
Ahadi ya kuzuia,
Wadachi huko Russia,
Hili limekwisha kuwa.”

1777

“Muda wa mwaka mzima,
Tumepata sudi njema,
Sisi na wanachama,
Wote wa uhuria.”

1778

“Hapana aliyejua,
Wala kutazamia,
Kushindwa kwa Italia,
Mara moja kutokea.”

1779

“Bomu tulizobwaga,
Udachi kuivuruga,
Zapita tulizopiga,
Mwaka uliotangulia.”

1780

“Bomu zetu zilipata,
Shabaha nyingi za vita,
Kuliko walizoleta,
Wadachi Britania.”

1781

“Hasara zetu za hewa,
Kidogo zilikuwa,
Bado tunatazamia,
Zitazidi kupungua.”

1782

“Tena kwa maendeleo,
Mwaka huo ujao,
Wadachi nguvu yao,
Hewani itazidiwa.”

1783

“Walakini tujikaze,
Bidii tusilegeze,
Hatari tusiibeze,
Mbele inayotujia.”

1784

“Tusisadiki ya kuwa,
Vita vinakaribia,
Kituoni kuingia,
Hilo halitafaa.”

1785

“Mzigo huwa na taabu,
Kama wendako karibu,
Kwa hivi tusihesabu,
Mwisho unakaribia.”

1786

“Kabla ya kutuliwa,
Mzigo huwalemea,
Watu wanaochukua,
Pengine wakazidiwa.”

1787

“Wajibu kutazamia,
Adui wetu mbaya,
Hakosi kujaribia,
Kisasi kutufanyia.”

1788

“Adui wetu mlafi,
Tuliyepiga makofi,
Atafanya ukorofi,
Hakosi kutukamia.”

1789
"Manahodha wa sabmarini,
Bora wa Kijermani,
Wengi wamo gerezani,
Wengine wameuawa."

1790
"Kwa hali waliyo nayo,
Hili haliwapi moyo,
Kutimiza watakayo,
Wadachi mabaharia."

1791
"Hili haliwafariji,
Halikidhi mahitaji,
Kwa sababu wanamaji,
Wengi wamewapotea."

1792
"Majeshi ya Marafiki,
Katika Pasifiki,
Yamewaonjesha dhiki,
Kubwa Wajapania."

1793
"Lae na Salamaua,
Walipigwa Wajapania,
Kwa bahari na kwa hewa,
Nguvu yetu wakajua."

1794
"Walipigwa Wajapani,
Kama vile Wajermani,
Katika El Alamein,
Vita vilivyotangulia."

1795
"Visiwa vya Aleutians,
Wajapani watesi,
Walikimbia upesi,
Kiza kilipoingia."

1796
"Wajapani kukimbia,
Bila kujipigania,
Wa mwisho akauawa,
Ni ajabu kusikia."

1797
"Hili hawakuzoea,
Kisha laonyesha kuwa,
Jambo geni watumia,
Kwa moyo kuwalegea."

1798
"Kuokoka kwa Mussolini,
Kwenda kwa Wajermani,
Hakutii asilani,
Badoglio hatia."

1799
"Walenzi waliambiwa,
Kama akikimbia,
Lazima kumuua,
Lakini walipumbaa."

1800
"Naples na Salerno,
Tumefanya mapigano,
Yaliyo magumu mno,
Bali tumefanikiwa."

1801
"Na sasa mpaka wetu,
Italia ni wa tatu,
Tumekwisha weka watu,
Wa pili kufunguliwa."

1802
"Vita vya kumwaga damu,
Mbele vitatulazimu,
Lakini tumeazimu,
Heshima kupigania."

1803
"Ndani yake tutakwenda,
Hata tuwe tumeshinda,
Na hilo tatalitenda,
Sababu tumenuia."

1804
"Vita tutaviingia,
Mpaka kuzikomboa,
Nchi walizochukua,
Zote Wadachi Ulaya."

1805
"Kukomboa Ufaransa,
Ni jambo linalopasa,
Tena ni heshima hasa,
Kwa watu wa Britania."

1806
"Kupeleka uokofu,
Ni kazi takatifu,
Wala hatuna hofu,
Sadaka kubwa kutoa."

1807
"Hatuna hofu na shaka,
Hili litatendeka,"
Kwisha hayo kutamka,
Churchill alitua."

1808
Staghafiru maneno,
Turudie mapigano,
Ya Naples na Salerno,
Tujue yalivyokuwa."

1809
Turudie tuelewe,
Tuyasome tuyajue,
Mioyoni tuyatie,
Tuzidi kukumbukia."

1810
Walikakamua kano,
Wadachi hapo Salerno,
Kusudi Jeshi la Tano,
La Wahuri kuzuiwa."

1811
Wadachi walishitadi,
Kupigana kikaidi,
Na Wahuri wakazidi,
Vita kuvishikilia."

1812
Shindo kubwa lilivuma,
La silaha za chuma,
Ardhi ikatitima,
Kama tufani la mvua."

1813
Ardhi ilititima,
Hapana aliyesema,
Kila mtu kasimama,
Kupigana kishujaa.

1814
Hapana aliyesema,
Ila sauti ya vyuma,
Ndizo zilizovuma,
Kwa Wadachi na huria.

1815
Vita vilistawi,
Vya Wahuri na adui,
Sadaka za uhai,
Kila upande zikawa.

1816
Vita vilishika kasi,
Pande zote za watesi,
Kama upepo wa kusi,
Uvumavyo kwa ghasia.

1817
Vita vilipozidi,
Wadachi iliwabidi,
Nyuma wenyewe kurudi,
Wahuri wawape njia.

1818
Mara Wadachi watesi,
Walipotoa nafasi,
Jeshi la Tano upesi,
Naples lilingia.

1819
Lilipofika mjini,
Lilikuta Wajermani,
Wameiacha motoni,
Naples kuteketea.

1820
Ulikuwa ukiwaka,
Mji wote kakakaka,
Na majengo kuyeyuka,
Kama barafu kwa jua.

1821
Watu waliochoma,
Naples bila huruma,
Walikuwa wanachama,
Wapenzi wa Italia.

1822
Na watu waliozima,
Moto uliochomwa,
Walidhaniwa si wema,
Kwanza na Italia.

1823
Hiyo ndiyo miujiza,
Ambayo huwapoteza,
Wanaochagua kiza,
Nuru wakaikataa.

1824
Huo ndiyo utelezi,
Wengi unaowahizi,
Wanaofanya wapenzi,
Watu wenye mbili nia.

1825
Watu wenye nia mbili,
Si marafiki wa kweli,
Wala hawana muhali,
Ahadi kuibeua.

1826
Walijifanya Wadachi,
Ahadi hawaiachi,
Kumbe walitaka nchi,
Mwisho moto kuitia.

1827
Kumi na tatu Oktoba,
Mwaka wa tano dhoruba,
Alitangaza hotuba,
Waziri wa Italia.

1828
"Ukali wa kisasi,
Iliofanywa Naples,
Umepita kiasi,
Katika historia."

1829
"Watu wa mji huo,
Wamefanya wawezayo,
Kutetea roho zao,
Kwa nguvu na ushujaa."

1830
"Kila aina ya feli,
Yenye sifa ya ukali,
Na wingi wa ukatili,
Wadachi wametumia."

1831
"Dhuluma iliyotimu,
Hapana mwanadamu,
Awezaye kufahamu,
Zamani ilitokea."

1832
"Majuma kadha wa kadha,
Watu wamepata adha,
Majuma kadha wa kadha,
Watu wamevumilia."

1833
"Wamevumilia taabu,
Nyingi zisizo hesabu,
Kwa kutimiza wajibu,
Kujunga na huria."

1834
"Hapatakuwa amani,
Wala shwari mijini,
Akibaki Jermani,
Mmoja Italia."

1835
"Tusonge bega kwa bega,
Na marafiki kupiga,
Watu wanaovuruga,
Nchi ya Italia."

1836
"Twende vitani shirika,
Katika kila mpaka,
Italia na Amerika,
Pamoja na Britania."

1837

"Twende vitani bia,
Pamoja na Warussia,
Na mataifa huria,
Shirika yaliyongia."

1838

"Po pote wanapokuwa,
Raia wa Italia,
Wapigane na mdawa,
Bila mtu kubakia."

1839

"Balozi wa Taliani,
Anayekaa Spain,
Nimempa idhini,
Wadachi kuarifiwa."

1840

"Nimempa idhini,
Kuarifu Jermani,
Italia i vitani,
Upande wa uhuria."

1841

"Tena nimemwarifu,
Eisenhower tarafu,
Kuwa nia badilifu,
Zimehama Italia."

1842

"Mashaka na matata,
Wahuri walivyopata,
Ni mapito yamepita,
Wala hayatarejea."

1843

"Kwa hiari tunapenda,
Vitani tena kwenda,
Tusaidiye kushinda,
Mataifa huria."

1844

"Ushindi wa Wahuria,
Bila shaka utakuwa,
Kwa fahari Italia,
Yapenda kusaidia."

1845

"Twapenda kusaidia,
Twende na Wahuria,
Vitani kushambulia,
Adui wa dunia."

1846

"Na mara vikisha vita,
Bila shaka watapata,
Uhuru wa kutakata,
Watu wa Italia."

1847

"Italia itakuwa,
Na serikali huria,
Na hili litakuwa,
Vita mara vikitua."

1848

Walitakwa waongozi,
Waandaye shambulizi,
Akaitwa kubarizi,
Smuts Britania.

1849

Kuwasili kwa mgeni,
Liwali wa London,
Alisema barazani,
Hotuba kumpokea.

1850

"Imekutana baraza,
Makusudi kusikiza,
Mweledi wa kuwaza,
Na stadi wa kujua."

1851

"Karibisho la London,
Namkirimu mgeni,
Wa pili kwa kifani,
Katika wateuliwa."

1852

"Huyu ni askari,
Shujaa na mashuhuri,
Kisha ni waziri,
Bora anayesifiwa."

1853

"Rafiki wetu mpenzi,
Mheshimiwa na enzi,
Wote tuliobarizi,
Karibisho tunatoa."

1854

Liwali alipokoma,
Usemi wake kusema,
Smuts alisimama,
Shukurani akatoa.

1855

Alipokwisha eleza,
Jinsi alivyopendezwa,
Kwa kuitwa Uingereza,
Hotuba hii kutoa:-

1856

"London ina fahari,
Leo isiyo kadiri,
Wala isiyo urari,
Katika historia."

1857

"Licha watuwe mjini,
Hata wa ulimwenguni,
Wajivunia London,
Mji usiolemewa."

1858

"London hailemewi,
Na mapigo ya adui,
Wala hofu haijui,
Saa ya kujaribiwa."

1859

"Haitishwi na mashaka,
Tena shida kuvunjika,
Ukumbusho imeweka,
Bora katika dunia."

1860

"London imesimama,
Mfano kama alama,
Ya uhuru wa daima,
Hapa chini ya jua."

1861

"Kama ilivyo London,
Taifa la Britani,
Lilijiunga yakini,
Dola yake kutetea."

1862

"Liliungana kiume,
Likafanya nyingi shime,
Kando ya Mfalme,
Pamoja na Malkia."

1863

"Lilifanyiza umoja,
Wa kusimama pamoja,
Ambao haujakuja,
Katika historia."

1864

"Safari hii naona,
Imenipendeza sana,
Kuliko ya mwaka jana,
Ya kuja Britania."

1865

"Kusini ya Afrika,
Kiongozi ilitaka,
Nafurahi kutamka,
Kuwa nimechaguliwa."

1866

"Na wenzangu wawili,
Wa milki mbali mbali,
Nao iliwakabili,
Heri ya kuteuliwa."

1867

"Mambo haya nadhania,
Yanadhihirisha nia,
Ya vita kushikiliwa,
Hata mwisho kuujua."

1868

"Na haya ni madhubuti,
Ya kuungana umati,
Kwa urafiki thabiti,
Na watu wa Britania."

1869

"Mashimo yenye hadaa,
Ya dola peke kukaa,
Dola zitayakimbia,
Yasiharibu dunia."

1870

"Zitakimbia mashimo,
Duniani yaliyomo,
Pasiwe kusema simo,
Hatari ikitokea."

1871

"Sihitaji kuonyesha,
Nini ninafananisha,
Ila nitadhihirisha,
Moyo wangu umetua."

1872

"Hufurahi wangu moyo,
Ninapowaza yajayo,
Wakati huo ujao,
Kuliko nilivyokuwa."

1873

"Kama huu uchaguzi,
Ukisemwa waziwazi,
Wuonya bila ajizi,
Dulili ya kushindia."

1874

"Watu wa Uingereza,
Hawataki kuteuzwa,
Kuonyesha wanaweza,
Kujiunga mara moja."

1875

"Wameungana kwa kweli,
Nyuma ya Churchill,
Ambaye astahili,
Heshima ya dunia."

1876

"Yeye atawaongoza,
Hata iwe mmeweza,
Ushindi kuutumiza,
Na faida kuwajia."

1877

"Atawaletea sudi,
Nyingi zisizo idadi,
Walimwengu wafaidi,
Katika hii dunia."

1878

"Yeye atafanyiza,
Ambayo hawakuweza,
Wengine kuyatimiza,
Vita iliyotangulia."

1879

"Hawakuwa na hakika,
Watu waliozuzuka,
Kutabiri kuanguka,
Dola ya Britania."

1880

"Waliodai kujua,
Ushindi utatokea,
Juu ya Britania,
Kabisa walipotea."

1881

"Watu waliotabiri,
Kushindwa kwa Wahuri,
Sasa waona dhahiri,
Hilo shida kutokea."

1882

"Jawabu limetokea,
La kuonyesha ya kuwa,
Waliotabiri haya,
Sasa wanawayawaya."

1883

"Vita vilipozuka,
Badala ya kuvunjika,
Dola iliunganika,
Kama imesakifiwa."

1884

"Mwaka jana na huu,
Mabadiliko makuu,
Yaliyoleta nafuu,
Yamepata kutokea."

1885

"Nakumbuka nilisema,
Mwaka jana ya kama,
Kujikinga kutakoma,
Iwe tunashambulia."

1886

"Wakati nilipotoa,
Maneno hayo sikia,
Mimi sikutazamia,
Kuwa yatakuwa haya."

1887

"Na mabadiliko haya,
Tangu yalipotokea,
Imani inanijia,
Kuwa tutafanikiwa."

1888

"Kila yakijibadili,
Hatari inakabili,
Lakini ndiyo dalili,
Ya ushindi kutokea."

1889

"Mwaka jana Oktoba,
Tulikabili misiba,
Mikali kama dhoruba,
Kwa hatari kuzidia."

1890

"Nguvu yetu maalumu,
Ambayo naifahamu,
Ilikuwa ya mabomu,
Na ndege katika hewa."

1891

"Hilo ndilo tegemeo,
Letu sisi mwezi huo,
Lakini mengineyo,
Tamaa hayakutia."

1892

"Hatari ya sabmarini,
Za adui baharini,
Naikumbuka moyoni,
Kuwa hofu ilitia."

1893

"Tisho la Caucasus,
Lilitupa wasiwasi,
Mwingi usio kiasi,
Alipopenya mdawa."

1894

"Adui alichaga,
Akatisha kuvuruga,
Caspian na Volga,
Katika nchi Russia."

1895

"Halafu ikaja dhiki,
Upande wa mashariki,
Ikawa tulidiriki,
Kurudi hata India."

1896

"Na katika Pasifiki,
Vikosi vya Marafiki,
Vilijikinga kwa dhiki,
Katika kila kisiwa."

1897

"Kusikazini Afrika,
Mapigano yaliwaka,
Akatisha kuteka,
Adui Alexandria."

1898

"Tangu mwanzo wa msimu,
Huta vuli kutimu,
Wingi wa bahati ngumu,
Mwaka jana tulipewa."

1899

"Mapigano mawili
Ndiyo yaliyobadili,
Hali yetu ya awali,
Ushindi ukatujia."

1900

"Kwanza Stalingrad,
Walishindwa wakaidi,
Na pili kwa idadi,
El Alamein sikia."

1901

"Hayo ndiyo mapigano,
Yaliyoacha mfano,
Mkubwa kwa mlingano,
Na mengine ya dunia."

1902

"Maumivu na majonzi,
Ya utawala wa Nazi,
Kufanya maenezi,
Ulaya yamepungua."

1903

"Jeshi la sabmarini,
Lilipigwa taabani,
Visiwa vya Solomon,
Vikatoka kwa mdawa."

1904

"Tena zaidi ya haya,
Mwendo uliendelea,
Wa adui kutolewa,
Katika New Guinea."

1905

"Hili linatazamisha,
Tena linaajabisha,
Mtu akipambanisha,
Mambo yaliyotokea."

1906

"Karibu huyu mdawa,
Ushindi kuufikia,
Ghafla yakatokea,
Mageuzo kama haya."

1907

"Mambo yalijibadili,
Yakaleta na ajali,
Ya kushindwa wakatili,
Stalingrad Russia."

1908

"Pili Waingereza,
Kadhhalika waliweza,
Adui kumfukuza,
El Alamein, Misria."

1909

"Hapana kinachoweza,
Kunyang'anya Waingereza,
Wala Warussia sikiza,
Sifa ya matendo haya."

1910

"Basi hizi mara mbili,
Za kushindwa wakatili,
Zilionyesha dalili,
Mwisho utakavyokuwa."

1911

"Hizi ni ishara mbili,
Ambazo zilibadili,
Ushindi wa wakatili,
Usiweze kutimia."

1912

"Na sasa Waamerika,
Vita wamevishika,
Kisha yanaongezeka,
Majeshi yao kukua."

1913

"Kwa msaada wa Amerika,
Tulishinda Afrika,
Mediterraneo tukavuka,
Kutiisha Italia."

1914

"Mambo yaliyofanyika,
Yanapasa kukumbukwa,
Na mioyoni kuwekwa,
Hata kusimuliwa."

1915

"Tena si kama nazua,
Nguvu yetu ya hewa,
Imempa mdawa,
Uzito wa kulemea."

1916

"Imempa uzito,
Wa kuwaka miji moto,
Na mawazo na majuto,
Ambayo hakudhania."

1917

"Tukitazama nyuma,
Ili mambo kuyapima,
Tutaona ya kama,
Mengi tumejitendea."

1918

"Tumepanda toka chini,
Tena tumo safarini,
Ushindi si yamkini,
Kuwa utatukimbia."

1919

"Tunapanda polepole,
Kisha tunasonga mbele,
Tufike kwenye kilele,
Cha kumshinda mdawa."

1920

"Huko twendako si mbali,
Mungu akitujali,
Karibu tutakabili,
Vita vikubwa Ulaya."

1921

"Masika hayo yajayo,
Yatakuwa nisemayo,
Kwa kufanya shambulio,
Kubwa tunalonuia."

1922

"Wakati huo wa mwaka,
Tutakuwa tumefika,
Hitler alikoweka,
Ngome kubwa Ulaya."

1923

"Ngomeni tukisha fika,
Mapigano yatawaka,
Kwa zana zilizoshikwa,
Zote na Wahuria."

1924

"Na shambulio la pili,
La Mashariki ya Mbali,
Litafanywa liwe kali,
Juu ya Japania."

1925

"Hitler anguko lake,
Magharibi mkumbuke,
Litahimiza makeke,
Mikado kumfikia."

1926

"Anguko la Jermani,
Ni alama ya mwanzoni,
Ya kushindwa Japani,
Na vita kutulia."

1927

"Sehemu ya Amerika,
Kwa kweli imetukuka,
Kwa kuwapa Washirika,
Zana za kupigania."

1928

"Na labda itakuwa,
Mbele inatangulia,
Vita vikiwadia,
Katika ngome Ulaya."

1929

"Nataka nisifiche,
Wala mengine niache,
Wakati huwa mchache,
Vitani mtu akiwa."

1930

"Yapasa kila dakika,
Tufanye jambo haraka,
Nchi zilizoshikwa,
Zipate kuokolewa."

1931

"Kama tunakusudia,
Ulaya kuiokoa,
Itapasa kuandaa,
Vita vishe mara moja."

1932

"Kama tukichelewa,
Dhiki kubwa itakuwa,
Ya kurudisha Ulaya,
Hali ilivyokuwa."

1933

“Kila mashaka magumu,
Wamepata wanadamu,
Tangu walipoazimu,
Wadachi kufanya baa.”

1934

“Uovu wa Jermani,
Karne ya ishirini,
Kabisa haulingani,
Na mwingine wa dunia.”

1935

“Hata siku za ushenzi,
Hapakutokea enzi,
Ilinganayo na Nazi,
Kwa dhuluma na ubaya.”

1936

“Yatupasa kila hali,
Tufanyize tasihili,
Kukomesha ukatili,
Unaodhuru Ulaya.”

1937

“Na Hitler hivi sasa,
Hana tumaini hasa,
Kuwa itampasa,
Kuishinda dunia.”

1938

“Hapiganii kushinda,
Kama alivyopenda,
Lakini amejipinda,
Muda mwingi kutumia.”

1939

“Hapigani kwenda mbele,
Makusudi atawale,
Nchi hii na ile,
Kama alivyonua.”

1940

“Amekuwa si muwinda,
Wa dunia kuishinda,
Ila bidii atenda,
Tuzidi kuchelewa.”

1941

“Anazohalisha shari,
Na kuwatisha Wahuri,
Ana silaha ya siri,
Labda atatumia.”

1942

“Sasa hapigani vita,
Kwa tamaa ya kupata,
Lakini anatafuta,
Bahati kumtokea.”

1943

“Bahati anaitaka,
Ya kugomba Washirika,
Lakini shida kuzuka,
Jambo analongojea.”

1944

“Kama angoja kura,
Ya kumpa tijara,
Atazamiye hasara,
Kuwa itamfikia.”

1945

“Kuma angoja nasibu,
Daada ya kuharibu,
Atazamiye adhabu,
Ndilo lililolekea.”

1946

“Kila akingoja sana,
Mutokeo ya fitina,
Jibu letu ataona,
Twezidi kushambulia.”

1947

“Wuhuri wamejiunga,
Wala hapana uganga,
Uwezao kuwatenga,
Mbulimbali wakawa.”

1948

“Wamejiunga kuteta,
Mpaka mwisho wa vita,
Hitler shida kupata,
Hila ya kuwafumua.”

1949

“Hila hiyo atakosa,
Hata iwe yampasa,
Amani kwetu kuposa,
Atubu kila hatia.”

1950

“Sababu kusudi letu,
Ni kutenda kila kitu,
Juu ya adui wetu,
Kiwe kinamlelea.”

1951

“Tutafanya shambulio,
Juu ya metegemeo,
Adaiyo kuwa ngao,
Yapate kumwangukia.”

1952

“Mwaka huo ujao,
Tutatenda tuwezayo,
Tuhimize matokeo,
Ya amani ya dunia.”

1953

“Lazima tupige kumbo,
La kuyahimiza mambo,
Yasichukue kitambo,
Kikubwa yakakawia.”

1954

“Lazima tufanye shindo,
Kubwa sana la matendo,
Makusudi hii kondo,
Ikome kuendelea.”

1955

“Busara yetu ya vita,
Sifa imekwisha leta,
Na nguvu tuliyoipata,
Yatosha kutegemea.”

1956

“Tena si kama hatuna,
Kiongozi wa maana,
Tumepata bora sana,
Mtu anayeelewa.”

1957

"Kiongozi wetu sisi,
Stadi nambari mosi,
Ajua nyingi jinsi,
Za vita kuviandaa."

1958

"Mwisho utakavyokuwa,
Hata adui ajua,
Neno lililobakia,
Ni kuuhimiza kuwa."

1959

"Lazima tuuhimiza,
Kuchelewa usiweze,
Kila jambo tufanyize,
Ambalo tutajaliwa."

1960

Smuts alipokoma,
Hotuba yake kusema,
Baraza ilinguruma,
Kwa shangwe alilopewa.

1961

Alipewa shangwe kuu,
Mwisho wa usemi huu,
Sauti zikenda juu,
Za waliousikia.

1962

Tarudi kusimulia,
Namna yalivyokuwa,
Mapigano Italia,
Ya adui na huria.

1963

Tarudi ili ninene,
Mwendo wa Jeshi la Nane,
Na la Tano mwone,
Mzidi kuelewa.

1964

Majeshi haya mawili,
Yaliposhuka ni mbali,
Kwa wingi wa maili,
Hata Rumi kufikiwa.

1965

Mji huo wa Rumi,
Ndiyo kinywa na ulimi,
Ukishikwa haisemi,
Nchi ya Italia.

1966

Ndiyo fahari ya dola,
Na kiti cha utawala,
Kuliko kila mahala,
Katika Italia.

1967

Na mkono wa adui,
Ulikuwa hautui,
Kwa kuharibu uhai,
Huko Rumi wa raia.

1968

Italia haihemi,
Mpaka mji wa Rumi,
Utolewe kwa magumi,
Mkononi mwa mdawa.

1969

Illi ya kuondolewa,
Katika Rumi mdawa,
Malama ya Italia,
Kuwa haijatimia.

1970

Ndipo yalipowania,
Majeshi mawili haya,
Kumfuata mdawa,
Rumi aliyezuia.

1971

Majeshi haya mawili,
Katika kila maili,
Yulikuta wakatili,
Vita wanavingojea.

1972

Walivingoja watete,
Wahuri wasipite,
Au wauawe wote,
Wadachi Italia.

1973

Adui kila mahali,
Alifanya vita kali,
Kuzuia mahali,
Pawezapo kuwa njia.

1974

Nchi yenyewe ya mito,
Wakati wa mvua nzito,
Usumbufu wa mapito,
Mkubwa ulitokea.

1975

Usumbufu wa kupita,
Ulifanyiza matata,
Wahuri wakateta,
Katika kila hatua.

1976

Katika safari ndefu,
Wingi wa usumbufu,
Ujengao utukufu,
Mara nyingi hutokea.

1977

Walipanda milima,
Wakiteta njia nzima,
Bila ya kusimama,
Adui na huria.

1978

Walipayita mabonde,
Wakipigana makonde,
Watu wa kila upande,
Hasirani walikuwa.

1979

Hasira iliwashika,
Nyuso zikakunjika,
Mishipa ikawatoka,
Kwa hali ya kuchukia.

1980

Mishipa ya wapigani,
Wahuri na Wajermani,
Iiinuka nyusoni,
Wakatisha kuangalia.

1981

Jasho liliwatoka,
Wadachi na Washirika,
Kila upande ulitaka,
Kuonyesha ushujaa.

1982

Wadachi walihofia,
Wakitoka Italia,
Italazimu dunia,
Kusifu Britania.

1983

Hiyo kwao ni chuki,
Kusikia hawataki,
Kuwa dola yenye maki,
Ni Waingereza Ulaya.

1984

Wadachi walijisifu,
Kuwa watu watukufu,
Wengine wote dhaifu,
Si watu wa kusifiwa.

1985

Kama yangeamriwa,
Tutakayo yote kuwa,
Kwa Mungu tungechukua,
Ungu tukatumia.

1986

Lakini hilo Mwenyezi,
Hakutuwekea wazi,
Kuchukua hatuwezi,
Ila kwa majaliwa.

1987

Walimwengu watakavyo,
Sivyo Mungu atendavyo,
Hutenda apendavyo,
Wala hana hatia.

1988

Cha chini hukipandisha,
Cha juu akakishusha,
Jambo akiamrisha,
Lazima litakuwa.

1989

Mungu kabisa hafunzwi,
Wala hawi mwanafunzi,
Njia zake haziwazi,
Siyo kama za dunia.

1990

Mungu hana tatizi,
Hatatizwi Mwenyezi,
Hufanya kiwe azizi,
Cho chote akichagua.

1991

Mungu haambiwi sivyo,
Hakatazwi atendavyo,
Kutamani kuwa hivyo,
Mwanadamu si sheria.

1992

Mungu kikimpendeza,
Cho chote kukitukuza,
Mwanadamu kukiviza,
Atakuwa hana njia.

1993

Basi majeshi yale,
Kila siku polepole,
Yalizidi kwenda mbele,
Mateka yakachukua.

1994

Yalikamata miji,
Pamoja na vitongoji,
Wingi wa wapiganaji,
Mahabusi wakawa.

1995

Wadachi walipigana,
Kwa nguvu nyingi sana,
Hila kila aina,
Walipata kutumia.

1996

Hila za kuzuia,
Wadachi walizojua,
Nyingi walitumia,
Hata mpya wakatia.

1997

Hila mpya walitia,
Miji wakaibomoa,
Majeshi ya uhuria,
Yasipate pa kukaa.

1998

Miji mingi ya thamani,
Iliyovuta uoni,
Iltiwa motoni,
Uzuri ukapotea.

1999

Wadachi kurudi kwao,
Kama bahari ipwayo,
Wahuri kusonga kwao,
Kama bahari kujaa.

2000

Ukitaka kuelewa,
Vita vilivyokuwa,
Mfano wake bamvua,
Kupwa na kujaa.

2001

Vita vilifanya wimbi,
Wakaonyana ujimbi,
Na wingi wa vitimbi,
Wadachi na Wahuria.

2002

Vitimbi vya ushujaa,
Na silaha za Ulaya,
Mpya katika dunia,
Uamuzi zilipewa.

2003

Ziliachwa ziamue,
Hata dunia ijue,
Aliyeshinda mwenziwe,
Adui au huria.

2004

Zana za chuma kigumu,
Zitishazo wanadamu,
Ambazo walifahamu,
Wadachi walitumia.

2005
Wahuri walitumia,
Zana za chuma pua,
Ambazo zilifuliwa,
Vita kuamulia.

2006
Zana hizo zikivuma,
Kwa mashujaa ni ngoma,
Fahari na heshima,
Moyoni tele hujaa.

2007
Mizinga ilipoonda,
Mashujaa walipenda,
Mfano kama kinanda,
Ngurumo walisikia.

2008
Wote mbele walisonga,
Silaha zilipogonga,
Japo kama mchanga,
Mauti yalienea.

2009
Kila mtu alisonga,
Pasipo moyo kugonga,
Bunduki na mizinga,
Zikawa kama bandia.

2010
Silaha za kutishia,
Wote walizotumia,
Zilikuwa kama pia,
Za watoto kuchezea.

2011
Walipigana wagomvi,
Marafiki na wajuvi,
Ukakawia ugomvi,
Siku nyingi Italia.

2012
Vita vilistawi,
Vya Wahuri na adui,
Kugombea nchi hii,
Jasho jingi wakatoa.

2013
Wadachi wenye fahari,
Na Wahuri wenye ari,
Pande zote askari,
Wasema shime shujaa!

2014
Palikuwa na Mdachi,
Ambaye kitu hafichi,
Wala kweli haichi,
Wenziwe kuwambia.

2015
Alikuwa na shabaha,
Ya kifo au jeraha,
Hidaya ya ufasaha,
Wa usemi alipewa.

2016
Alikuwa na heshima,
Katika jeshi zima,
Neno akilisema,
Halikosi kutokea.

2017
Aliwambia wenziwe,
"Nataka wote mjue,
Vita hivi mwishowe,
Naona kuwa mbaya."

2018
"Hitler haelewi,
Dhiki ya vita hii,
Lakini sisi tu hoi,
Twatamani kupumua."

2019
"Kila siku adui,
Aja mbele hatui,
Mimi sioni rai,
Ya kushinda watu hawa."

2020
"Niamruni niseme,
Kuwashinda ni kinyume,
Nawataka mtazame,
Haya ninayowambia."

2021
"Mlima tunaopanda,
Kwa kusudi la kushinda,
Juu hatuwezi kwenda,
Buki kuning'inia."

2022
"Twashuka mtelemko,
Mbio hatuna kishiko,
Katika maanguko,
Karibu tutaingia."

2023
"Kila tukiwa bondeni,
Au maangukoni,
Tusiweke tumaini,
La ushindi kutujia."

2024
"Bahati si uongo,
Imetupa mgongo,
Tumo katika ukingo,
Bado kutumbukia."

2025
"Kuchafua makabila,
Kwetu sisi ni mila,
Lakini kuyatawala,
Jambo gumu kutokea."

2026
"Kama wasingeingia,
Watu wa Britania,
Dola zilizobakia,
Zingeshindwa mara moja."

2027
"Lakini Waingereza,
Shida sana kuwaweza,
Kwa sababu miujiza,
Mingi wanaelewa."

2028
"Laini kama hariri,
Lakini katika shari,
Kushindwa hawakiri,
Ndivyo walivyojaliwa."

2029

“Ni wapenzi wa amani,
Saburi na makini,
Lakini nuksani,
Wakitendwa ni udhia.”

2030

“Katika wanadamu,
Waingereza wagumu,
Na baridi kama sumu,
Alaye hudhuriwa.”

2031

“Sumu haina mchezo,
Ikiliwa ni mzozo,
Tusifanye hatunazo,
Akili za kutambua.”

2032

“Sumu isipochokozwa,
Shida sana kuumiza,
Lakini ikimezwa,
Manza yatatokea.”

2033

“Kila silaha kali,
Tuliyoshika awali,
Wamepata mara mbili,
Na labda kuzidia.”

2034

“Baharini wana vyombo,
Na bara wana mitambo,
Ihimiliyo makumbo,
Na nguvu katika hewa.”

2035

“Badoglio mwerevu,
Msidhani mpumbavu,
Aliona ushupavu,
Wetu hauna njia.”

2036

“Asingefanya maasi,
Na kutwachia utesi,
Angaliona halisi,
Kuwa tutafanikiwa.”

2037

“Ubongo mkiukaza,
Kwa kusudi la kuwaza,
Picha ninayofanyiza,
Mtaona kuwa sawa.”

2038

“Vichwa mkivilegeza,
Mtaona Waingereza,
Mwaweza waangamiza,
Shida hilo kutokea.”

2039

“Kwanza haikutokea,
Udachi kushambuliwa,
Sasa moto inatiwa,
Kila pembe na mdawa.”

2040

“Mwanzo wa mapigano,
Tulipata mavuno,
Huu mwaka wa tano,
Mavuno yatapotea.”

2041

“Hapahitaji nahau,
Kuonyesha mwaka huu,
Kuwa mavuno makuu,
Watapata Wahuria.”

2042

“Ingawa mimi Mdachi,
Kusema kweli siachi,
Wala mawazo sifichi,
Wenzangu kuwambia.”

2043

“Kwa moyo ninapigana,
Hitler awe bwana,
Lakini ninayoona,
Kuficha siyo sawa.”

2044

Hapa nafanya mchovyoo,
Katika mambo yalivyo,
Kila jambo lilivyo,
Watu wapate elewa.

2045

Alifika Teheran,
Waziri wa Britani,
Roosevelt na mgeni,
Stalin wa Russia.

2046

Mtu mwingine wa maana,
Chiang Kai-Shek jina,
Kiongozi wa China,
Alihudhuria pia.

2047

Mkutano Teheran,
Wa watu hawa wageni,
Uliongea Japani,
Namna ya kutendewa.

2048

Walikuja wapatane,
Pato la nusu karne,
La nchi za wengine,
Irudishe Japania.

2049

Nchi walizochukua,
Kwa choyo kwa wakiwa,
Baraza iliamua,
Wenyewe kurudishiwa.

2050

Lazima kuondolewa,
Katika kila kisiwa,
Ambacho walichukua,
Kwa kudhulumu wakiwa.

2051

Katika visiwa vyote,
Walivyovitia pete,
Wataondolewa wote,
Bila mtu kubakia.

2052

Visiwa mbalimbali,
Karibu elfu mbili,
Si haki wala halali,
Japani kuachiwa.

2053

Kila walipoweka,
Bendera ya mamlaka,
Italazimu kushuka,
China hata India.

2054

Walidai Wajapani,
Ujapani kwa Japani,
Kadhaliika nchi ngeni,
Kuachiwa si sheria.

2055

Hawawataki wageni,
Kwayo haiwezekani,
Kuachiwa Japani,
Ushirika wa dunia.

2056

Muumba hutoa jua,
Tena hushusha mvua,
Akaeneza na hewa,
Watu wote kutumia.

2057

Kisha hutoa mwezi,
Na nyota za maongozi,
Dunia nzima hasazi,
Viumbe hukirimiwa.

2058

Vitu hivi muhimu,
Hugawa sawa Karimu,
Kwa wote wanadamu,
Bila ya kupendelea.

2059

Vitu hivi vya lazima,
Mungu mwenye rehema,
Wa mbele na wa nyuma,
Humpa fungu sawa.

2060

Haya huonyesha wazi,
Kusudi la Mwenyezi,
Kufanya maongozi,
Watu waishi bia.

2061

Japani haya hataki,
Lazima itendwe haki,
Wengine asiwadhiki,
Kwao kuwavurugia.

2062

Kama hataki kwake,
Watu wengine wafike,
Kwa hivi haki yake,
Ushirikani kutolewa.

2063

Asiyetaka ushirika,
Katika alichoshika,
Hana haki ya kutaka,
Kisicho chake kupewa.

2064

Nia ya baraza hii,
Kila nchi ya adui,
Shina lake na matawi,
Lazima kuharibiwa.

2065

Japani inatakiwa,
Matawi kuondolewa,
Na shina kung'olewa,
Kama mmea mbaya.

2066

Kwa sababu haiwezi,
Enzi wala maongozi,
Zaidi ya uchokozi,
Wanyonge kuwaonea.

2067

Haitaachiwa tena,
Igombane na China,
Wala kufanya fitina,
Na kuchafua dunia.

2068

Ikitokea amani,
Nchi ya Japani,
Itawekwa mkononi,
Mwa taifa huria.

2069

Itapewa Amerika,
Nchi hii kuishika,
Mpaka kuelimika,
Uhuru na sheria.

2070

Shindo la baraza hiyo,
Katika kila radio,
Ilioko Tokio,
Lilipata kusikiwa.

2071

Radio za Berlin,
Na pengine duniani,
Zilieleza kiini,
Cha baraza sawasawa.

2072

Zilisema waziwazi,
Kuwambia wasikizi,
Zawadi ya wachokozi,
Ambayo watapewa.

2073

Adui kila mahali,
Aliambiwa kweli,
Jambo la kustahili,
Ambalo atatendewa.

2074

Lakini wapotofu,
Shida kuwa waongofu,
Hawahofu kukashifu,
Wema wanalochelea.

2075

Hitler na Mikado,
Muda kidogo bado,
Watavuna mipando,
Ya dhuluma na ubaya.

2076

Mchovyoni niliotaka,
Sasa umekamilika,
Teheran tutatoka,
Tuandame tena njia.

2077
Zaidi nitaandika,
Watu wapate kumbuka,
Mambo yaliyotendeka,
Bila moja kubakia.

2078
Mwaka ulipotokea,
Elfu na tisa mia,
Arobaini pamoja,
Mwisho nne ikatiwa.

2079
Uingereza Mfalme,
Alitaka wanaume,
Wa kuzishukia ngome,
Za Hitler Ulaya.

2080
Jina la mpaka huu,
Watu wasisahau,
Kuwa Waziri Mkuu,
Alikwisha watajia.

2081
Alisema Churchill,
Kuwa mpaka wa pili,
Mwenye macho ya nili,
Uamiri akapewa.

2082
Hayo macho ya nili,
Ni ushahidi kamili,
Wa hekima na akili,
Mtu aliyejaliwa.

2083
Kwa mtu aliye nayo,
Macho hayo ni kioo,
Kionyeshacho upeo,
Wa fikira kujaa.

2084
Ndiyo macho yapenyayo,
Pasi na kizuio,
Katika ayawezayo,
Mwanadamu kuyajua.

2085
Yanaonyesha ubongo,
Wa akili mvingo,
Inayopanga mipango,
Mambo yakawa sawa.

2086
Jina lake nakariri,
Watu wajue vizuri,
Huyo ni Jemadari,
Dwight Eisenhower.

2087
Umri wa huyu mtu,
Aliyeongoza watu,
Ni hamsini na tatu,
Miaka yake ilikuwa.

2088
Mtu wa makamo haya,
Ni kijana maridhawa,
Kwa umri si sawa,
Na cheo alichopewa.

2089
Dhamana hii ni kuu,
Kuliko umri huu,
Yataka moyo wa juu,
Kama wa Eisenhower.

2090
Kazi ya shambulio,
Ulaya nzima mwambao,
Alipewa mtu huyo,
Bara na katika hewa.

2091
Alipewa kitara,
Atengeze barabara,
Mpaka kwa sogora,
Mdai enzi Ulaya.

2092
Uongozi wa majeshi,
Ya kukomesha ubishi,
Hesabu yake haishi,
Chini yake ulikuwa.

2093
Mwendo wa askari,
Kila aina magari,
Na zana zote za shari,
Ulimpasa kujua.

2094
Dhamana ya madege,
Makundi kama ya nzige,
Aliamru yabwage,
Bomu alipochagua.

2095
Historia hazina,
Mfano wa kulingana,
Na namna ya dhamana,
Yeye aliyopewa.

2096
Vita vyote vya zamani,
Hata vya Napoleon,
Hakuwapo mpigani,
Mdhaminifu wa haya.

2097
Yeye alichaguliwa,
Mbele ya watu kukaa,
Sababu alielewa,
Kumshawishi mdawa.

2098
Maarifa ya kuvuta,
Adui katika vita,
Na maamuzi kukata,
Mengi alielewa.

2099
Alikuwa ni turufu,
Wala kitu hakuhofu,
Mfalme Mtukufu,
Ndipo akamchagua.

2100
Alipewa uongozi,
Ufaransa abarizi,
Belgiji na Holanzi,
Na Udachi kwa mdawa.

2101

Chini yake jepadari,
Mtu wa kumshauri,
Alikuwa ni Amiri,
Arthur Tedder mwanahewa.

2102

Mtu wa tatu mgumu,
Katika hii kaumu,
Simba mkali fahamu,
Montgomery shujaa.

2103

Mfalme alitaka,
Montgomery kushika,
Waingereza wakishuka,
Kushambulia Ulaya.

2104

Vita Mediterraneo,
Na Afrika mwambao,
Vilikuza watu hao,
Ndipo wakenda Ulaya.

2105

Walitakwa watu hao,
Wakafanye shambulio,
Lihimize matokeo,
Ya ushindi kutokea.

2106

Alexander jabali,
Yeye hakwenda mahali,
Aliachiwa shughuli,
Ya vita Italia.

2107

Yeye aliachwa pale,
Ashike upande ule,
Tena asonge mbele,
Atiwe pete mdawa.

2108

Huyu aliamriwa,
Vita kuvishikilia,
Hata Italia,
Iwe imeokolewa.

2109

Kazi hii kuitenda,
Yataka bega kupinda,
Mfalme akapenda,
Alexander kupewa.

2110

Aliyepewa stadi,
Simba hahofu jihadi,
Ashikapo mkaidi,
Windo lake kutwaliwa.

2111

Adui akimshika,
Shida sana kuponyoka,
Kama hakuanguka,
Mateka atakuwa.

2112

Mbele ya huyu simba,
Kesselring alitamba,
Wakanuia kugomba,
Watu wawili hawa.

2113

Jepadari Kesselring,
Mdachi wa sifa nyingi,
Zivumazo kama mwangi,
Alishika Italia.

2114

Sifa kama kikorombe,
Zilivuma kila pembe,
Kuwa hana hata chembe,
Hofu ila ushujaa.

2115

Hitler alimwambia,
Kesselring kuzuia,
Rumi kutochukuliwa,
Na vita kuendelea.

2116

Tena apigane tu,
Atumie kila mtu,
Pasipo kusaza kitu,
Kiwezacho kutumiwa.

2117

Apigane sana Rumi,
Asichoshwe na magumi,
Hata avunje uvumi,
Wa Wadachi kuzidiwa.

2118

Na huku Alexander,
Aliamriwa kwenda,
Mpaka Rumi kushinda,
Hali itakavyokuwa.

2119

Aliamriwa ende,
Hata apate ushinde,
Asigeuke upande,
Wala nyuma kurejea.

2120

Apigane na adui,
Akaokoe uhai,
Kuvunja amri hii,
Siyo yake mazoea.

2121

Uhai wa raia,
Rumi uliharibiwa,
Naye hakuvumilia,
Hili kuendelea.

2122

Damu yake ilichoma,
Kwa kusikia dhuluma,
Akajihimiza hima,
Kupeleka hamaya.

2123

Ndipo aliposhuka,
Mwenyewe vita kushika,
Na kutanua mpaka,
Wa vita Italia.

2124

Baada ya askari,
Alishuka Jepadari,
Pwani yenye hori,
Ilipo mtatajiwa.

2125

Askari Marafiki,
Waliposhuka sadiki,
Ni kusini mashariki,
Rumi kuiielekea.

2126

Na hapo ilipo hori,
Juu ziko bandari,
Majina yake vizuri,
Wasomaji kutiliwa.

2127

Jina la kwanza Nettuno,
Wala si mbali mno,
Hapo na Rumi mfano,
Umbali wake sikia.

2128

Hapo na Rumi umbali,
Ni thelathini maili,
Takiriba saa mbili,
Gari likisafiriwa.

2129

Bali mwendo wa vita,
Hata karibu matata,
Sababu pa kupita,
Kwanza kuchaguliwa.

2130

Jina la pili Anzio,
Watu wa bandari hiyo,
Waliona majilio,
Ya wageni yawendea.

2131

Yaonekana ya kuwa,
Wadachi hawakujua,
Kuwa watashukiwa,
Horini kushambuliwa.

2132

Juu ya merikebu,
Nyingi sana kwa hesabu,
Zilizokuja karibu,
Kumbe hawakuelewa!

2133

Wadachi kutahamaki,
Askari marafiki,
Pwani wamefanya maki,
Ugeni umeenea.

2134

Hermann Goering,
Chini yake Kesselring,
Kwa mshangao mwingi,
Habari aliambiwa.

2135

Na katika wakaidi,
Wavumao kama radi,
Yumo katika idadi,
Hermann kwa kusifiwa.

2136

Alipewa habari,
Kuwa katika hori,
Wameshuka askari,
Bandari zimetwaliwa.

2137

Kushikwa hizo bandari,
Aliona ni hatari,
Akafanya ujasiri,
Kujaribu kuzuia.

2138

Aliamru mitambo,
Ipige mbele makumbo,
Walioshuka kwa vyombo,
Mbele wakaendelea.

2139

Alipoona mkazo,
Wa vita una mzozo,
Akapeleka tangazo,
Hermann kusaidiwa.

2140

Msaada alitaka,
Umwendee kwa haraka,
Watu katika mipaka,
Mingine wakatolewa.

2141

Watu walitolewa,
Mipakani mwa Russia,
Ili kwenda kuzuia,
Rumi kutochukuliwa.

2142

Shindo lilikuwa kubwa,
Ufa wataka kuzibwa,
Likaletwa jeshi kubwa,
Upesi kuziba njia.

2143

Kila Mdachi wa sifa,
Mtesi wa maarifa,
Aliarifiwa ufa,
Ule kwenda kuzuia.

2144

Wadachi walibana,
Ufa usiwe mpana,
Wahuri wakakazana,
Ufa kuupanua.

2145

Ufa ulitaka hasho,
Watu wakatoka jasho,
Vita vikafanya tisho,
Kila upande sikia.

2146

Kwenda nyuma ilihusu,
Maili moja na nusu,
Wadachi kama kisu,
Wakakata Wahuria.

2147

Walikata kwa pupa,
Hata katika mfupa,
Makali yakanepa,
Wasipate pa kunoa.

2148

Vile kupewa nafasi,
Ndiyo hila ya utesi,
Lakini hawakukisi,
Nini liliwangojewa.

2149

Walishika Wajermani,
Wahuri warudi pwani,
Ghaffa kama tufani,
Pigo liliwatokea.

2150

Liliwatokea pigo,
Zito kuliko mzigo,
Wakageuza visogo,
Nyuma wakakimbia.

2151

Pale walipochukua,
Wadachi walitolewa,
Kabla ya kuchwa jua,
Pato likawakimbia.

2152

Pato liliwakimbia,
Na jeshi lilipungua,
Ikawa kuwayawaya,
Watu waliobakia.

2153

Anzio na Nettuno,
Sitaki kukaa mno,
Nitageuza maneno,
Nipate kuendelea.

2154

Nitageuza maneno,
Ili nitie pigano,
Lililokuwa Cassino,
Katika kitabu pia.

2155

Mabomu maelfu,
Na makombora sufufu,
Juu ya wapotofu,
Cassino ilimwagiwa.

2156

Uzito wa mabomu,
Juu ya Cassino fahamu,
Kulinganisha vigumu,
Na pengine Italia.

2157

Mabomu ya baruti,
Kama matunda ya mti,
Yalimwagwa katikati,
Adui alipokuwa.

2158

Hayo mabomu mazito,
Na makombora ya moto,
Kulia na kushoto,
Yalishuka kama mvua.

2159

Mabomu na makombora,
Yalipotulia mara,
Ilipandishwa bendera,
Cassino na Wahuria.

2160

Watu walisadiki,
Zuio halikubaki,
Kumbe ndani ya handaki,
Wadachi walingojea.

2161

Wadachi kama mchwa,
Chini walijificha,
Bomu kutowafikicha,
Hata kulipotulia.

2162

Kimya kilipotokea,
Wadachi kuangalia,
Cassino inapepea,
Bendera ya uhuria.

2163

Walijiama vidole,
Wakatamani wajile,
Kwa kuona kuwa pale,
Bendera inapepea.

2164

Walitoka kwa pigano,
Pakawa masukumano,
Wao na Jeshi la Tano,
Makubwa sana elewa.

2165

Nataka hapa tulipo,
Hata hotuba iwepo,
Kwa simu ya upepo,
Ya Churchill kutiwa:

2166

"Natumaini ya kuwa,
Leo sitatazamiwa,
Usiku kuwambia,
Maajabu ya dunia."

2167

"Sitazamiwi kusema,
Shida zilizosimama,
Wala kutoa hekima,
Ya mafumbo kufumbua."

2168

"Mafumbo yote ya vita,
Na amani kupata,
Jibu la kutakata,
Bado halijatokea."

2169

"Mambo ya mwanadamu,
Kujua yote vigumu,
Lakini nina hamu,
Kidogo kuongea."

2170

"Leo nataka nionje,
Kusema japo punje,
Watu wa nchi za nje,
Waweze kunisikia."

2171

"Kama nyinyi mwapenda,
Kujua tunavyokwenda,
Kadhali napenda,
Hayo kuwasimulia."

2172

"Juu ya makosa yangu,
Nashukuru kwa Mungu,
Kuwa nyinyi wenzangu,
Wema mmenitendea."

2173

"Kwenu nimepata wema,
Nisioweza kupima,
Na msaada daima,
Ambao 'takumbukia."

2174

"Yapata mwaka mzima,
Tangu niliposimama,
Katika simu kusema,
Kwetu Britania."

2175

"Wakati uliopita,
Ni wakati wa matata,
Lakini tulipata,
Hata heri kutujia."

2176

"Heri yetu na mashaka,
Mizanini mkiweka,
Mtaona bila shaka,
Heri imezidia."

2177

"Mtaona kwa dhahiri,
Heri imepita shari,
Na mwendo wetu mzuri,
Twendako tunasogea."

2178

"Tunakwenda mbio mbio,
Mfulizo mwendo huo,
Tufike kwenye kituo,
Ambacho twakusudia."

2179

"Sasa safari ndefu,
Ya hatari na hofu,
Majeshi ya uokofu,
Yenda hatua hatua."

2180

"Mwisho wa safari yetu,
Utakamilika tu,
Na yaliyotisha watu,
Inshala hayatakuwa."

2181

"Tisho la ukatili,
Utumwa na ujahili,
Giza na ufedhuli,
Halitaziba dunia."

2182

"Na mtu wa haraka,
Kutabiri atataka,
Siku gani hakika,
Amani itatokea."

2183

"Atataka kutafiti,
Apate na madhubuti,
Namna ya masharti,
Mwisho yatakavyokuwa."

2184

"Hapana shaka na hoja,
Amani itakuja,
Hapahitaji kutaja,
Siku ya kutokea."

2185

"Umoja wa Marafiki,
Walio kisiwa hiki,
Na wa mbali sadiki,
Utavunja kila baa."

2186

"Umoja huu wa tendo,
Na nia katika kondo,
Sasa wahimiza undo,
La amani kutokea."

2187

"Jeshi la Nane mwajua,
Mwaka jana lilikuwa,
Limo katika njia,
Ndefu kuhadithia."

2188

"Maili kwa mfano,
Elfu na mia tano,
Za mwendo na mapigano,
Likenda bila kutua."

2189

"Lilisafiri jangwani,
Kutoka El Alamein,
Kupigana na Jermani,
Mpaka Mareth pia."

2190

"Halafu Jeshi la Kwanza,
Lililotoka Uingereza,
Safari liliongoza,
Na la Amerika pamoja."

2191

"Mwendo wa majeshi hayo,
Sasa niwambiayo,
Ulikwenda mbio mbio,
Yakafika Tunisia."

2192

"Wote tulitazamia,
Ushindi kutujia,
Bali hatukukisia,
Ghafa kutokea."

2193

"Hatukujua asili,
Kuwa miezi miwili,
Atapigwa katili,
Afrika na kutolewa."

2194

"Pigo dhoruba moja,
Lilitosha yetu haja,
Ushindi kwetu ukaja,
Mateka tukachukua."

2195

"Jumla mateka yetu,
Ilikuwa laki tatu,
Thelathini na tano watu,
Elfu walizidia."

2196

"Na Sicily tulipata,
Ushindi uliovuta,
Kiongozi wa matata,
Mussolini kutolewa."

2197

“Kaokoka Mussolini,
Ende akale mezani,
Mkate wa huzuni,
Na Hitler pamoja.”

2198

“Amemwua mkwewe,
Mume wa bintiye,
Kusudi akapewe,
Chakula cha kujilia.”

2199

“Italia kaitupa,
Na watu alioapa,
Mapenzi yake kuwapa,
Kisasi awatendea.”

2200

“Ajali na hukumu,
Alizopata dhalimu,
Mfano wake fahamu,
Heri kifo kutokea.”

2201

“Adhabu hizi ngumu,
Amezipata dhalimu,
Aliyekuwa na hamu,
Ya fahari ya dunia.”

2202

“Ampatwa na mkasa,
Kwa kuchoma Ufaransa,
Mgongoni bila kisa,
Kwa hamu ya kusifiwa.”

2203

“Jambo hili la hatia,
Yeye alitazamia,
Kuweza kumletea,
Enzi Mediterranea.”

2204

“Ushindi wetu sisi,
Wa Sicily na Naples,
Umetupa upesi,
Corsica na Sardinia.”

2205

“Visiwa hivi viwili,
Tuliviona awali,
Vitataka vita kali,
Lakini haikuwa.”

2206

“Sasa nawambia watu,
Katika sehemu tatu,
Sehemu moja ni yetu,
Ya bara ya Italia.”

2207

“Mwendo wetu haukuwa,
Kama tulivyodhania,
Lakini natazamia,
Rumi itaokolewa.”

2208

“Tena tumekwisha futa,
Vikosi vinavyopata,
Kama sitini na sita,
Vya nchi ya Italia.”

2209

“Na vikosi vya Jermani,
Ishirini na tano hesabuni,
Na sehemu ya hewani,
Vimebanwa Italia.”

2210

“Hivi vitatoka damu,
Na kuungua fahamu,
Katika nchi hasimu,
Aliyojiunga bia.”

2211

“Hapa akipata haya,
Mambo mengine mabaya,
Pengine yanangojea,
Adui kumtokea.”

2212

“Kutofanikiwa kwetu,
Aegean si kitu,
Ni hasara ndogo tu,
Bahari hii sikia.”

2213

“Hasara zetu kidogo,
Kuliko mvurugo,
Unaoandaa pigo,
Hungary na Rumania.”

2214

“Fujo linaandaliwa,
Adui kumwendea,
Ugiriki na Bulgaria,
Zimo katika njia.”

2215

“Tena Amiri Tito,
Anafanya pigo zito,
Linalowatia moto,
Wadachi Yugoslavia.”

2216

“Mashariki Karibu,
Na mbali mkihesabu,
Tumetimiza wajibu,
Wa kwenda bila kutua.”

2217

“Tangu siku zile,
Za huzuni na ole,
Upeke na makelele,
Hatukumwacha mdawa.”

2218

“Tangu siku za upeke,
Tulipinga yatanuke,
Adui matata yake,
Kama tulivyojaliwa.”

2219

“Siku zile za hatari,
Alituletea shari,
Mussolini Misri,
Usomali tukatolewa.”

2220

“Nchi ya Ethiopia,
Siku zile ilikuwa,
Mnyororo imetiwa,
Na watu wa Italia.”

2221

“Wakati ule sikia,
Mahali pa kuzuia,
Sisi hatukujua,
Ila tulikaza nia.”

2222

“Mashariki Mediterranea,
Na Balkans pia,
Kama hayo yatakuwa,
Lakini shaka ondoa.”

2223

“Watu wa Uingereza,
Kwa furaha watukuza,
Hatari ilivyovizwa,
Ya sabmarini Britania.”

2224

“Miezi hamsini na tano,
Mfulizo mapigano,
Ya ujinga mwingi mno,
Sabmarini zilitishia.”

2225

“Zilitisha kukata,
Riziki zetu kupata,
Lakini tumeteta,
Hata tumepata njia.”

2226

“Tisho tulivumilia,
Kubwa katika hewa,
Wakati tulipokuwa,
Hatuna silaha moja.”

2227

“Alituletea tisho,
Hitler na mtingisho,
Bali hakupata mwisho,
Sana alionuia.”

2228

“Hivi sasa wanajuta,
Watu waliotafuta,
Juu yetu kuleta,
Maangamizi kwa hewa.”

2229

“Chini wanagaagaa,
Kwa pigo la kutishia,
Linalokwenda kwa hewa,
Kutoka Britania.”

2230

“Chini wanaanguka,
Kwa pigo la Amerika,
Udachi linalofika,
Bila ya kuzuiwa.”

2231

“Mwaka jana mwaelewa,
Tulikwisha jifanyia,
Jeshi kubwa la hewa,
Katika hiki kisiwa.”

2232

“Na leo jeshi letu,
Halilingani na kitu,
Ila la rafiki yetu,
Amerika sikia.”

2233

“Umoja wa nguvu mbili,
Na udugu wa kweli,
Mazao yake awali,
Sitabiri kuyajua.”

2234

“Lakini mazao hayo,
Miezi haba ijayo,
Yatafanya matokeo,
Labda ya manufaa.”

2235

“Madege yetu elfu,
Yenda kwa wapotofu,
Adui kwa upungufu,
Kwetu huleta mia.”

2236

“Kwa siri kuambiana,
Habari kila namna,
Uongozi bora sana,
Umekwisha kutujia.”

2237

“Uongozi tumepata,
Tutakapo tunateta,
Na kuzuia matata,
Hata achoke mdawa.”

2238

“Tunatoa shukurani,
Kwa nguvu yetu barani,
Na ile ya baharini,
Pamoja na ya hewa.”

2239

“Shukurani tunatoa,
Tena tunatazamia,
Bora tutajitendea,
Ishuhudie dunia.”

2240

“Nguvu ya Wahuria,
Sasa imeenea,
Hitler ikimwendea,
Lazima atalemewa.”

2241

“Marafiki Russia,
Wangekosa kuelewa,
Dhiki zilizotujia,
Ajabu isingekuwa.”

2242

“Nchi yao ni ya bara,
Yenye nafasi bora,
Humo mara kwa mara,
Huweza kujitetea.”

2243

“Wao hawana hatari,
Ya kuvuka bahari,
Ila hukinga shari,
Bara na katika hewa.”

2244

“Lakini kwetu sisi,
Mwendo wetu wa utesi,
Ni mbalimbali halisi,
Si sawa na Warussia.”

2245

“Kwetu ikizuka shari,
Tuna dhiki za bahari,
Zitakazo ujasiri,
Mwingi kuzitangua.”

2246

“Watu wa Uingereza,
Na Amerika sikiza,
Sana wamependezwa,
Na ushindi wa Russia.”

2247

“Mara kwa mara nasema,
Nimetoa heshima,
Juu ya matendo mema,
Kuwasifu watu hawa.”

2248

“Sasa imenilazimu,
Niwambie mfahamu,
Maendeleo muhimu,
Yaliyotendwa na hawa.”

2249

“Majeshi ya Russia,
Adui yalimtoa,
Maili tisa mia,
Katika mwaka mmoja.”

2250

“Yalimwegema kwa kondo,
Yakamvunjia mwendo,
Akafukuzwa kando,
Hitler ya Russia.”

2251

“Mpaka wa wakatili,
Huko Russia awali,
Maili elfu mbili,
Ulivunjwa mara moja.”

2252

“Tangu niliponena,
Na nyinyi mwaka jana,
Maadui wengi sana,
Wamepotea Russia.”

2253

“Watu wa Russia,
Bahati wamejaliwa,
Kwa vile kujipatia,
Stalin shujaa.”

2254

“Huyu Amiri hodari,
Kaongoza askari,
Kwa ustadi mzuri,
Hata wamefanikiwa.”

2255

“Pale nilipowambia,
Hungary inaandaa,
Hitler kumrukia,
Sababu yake sikia.”

2256

“Sababu yake Warussi,
Wanatia wasiwasi,
Hungary na Balkans,
Hitler kuchafukiwa.”

2257

“Nimekwisha waambia,
Vita vilivyo Ulaya,
Vingine vimebakia,
Nataka waelezea.”

2258

“Vita vilivyobakia,
Hulingana sawasawa,
Kwa ushenzi na ubaya,
Na vya Hitler Ulaya.”

2259

“Ni vita vya Japani,
Vilivyomo mkononi,
Mwa Amerika baharini,
Bara na katika hewa.”

2260

“Uongozi wa bahari,
Vyombo vinavyosafiri,
Pasific tulikiri,
Waamerika kupewa.”

2261

“Waamerika pia,
Nao walituridhia,
Uongozi kuchukua,
Wa bahari ya India.”

2262

“Twaona sana fahari,
Tumepata shime nzuri,
Upande huu wa shari,
New Zealand na Australia.”

2263

“Ziliteta na Japani,
Na Ulaya Britani,
Ilizuia Jermani,
Pamoja na Italia.”

2264

“Kila ilipo bendera,
Union Jack bora,
Tukumbuke kila mara,
Fadhili tuliyoopewa.”

2265

“Kwa kazi waliyoshika,
Wanamaji Amerika,
Sasa kwao imefika,
Heri na kufanikiwa.”

2266

“Askari wao pia,
Wametenda kama haya,
New Zealand na Australia,
Nyuma hazikuwa.”

2267

“Mwendo wa New Guinea,
Daima waendelea,
Na Japani atolewa,
Kwa haraka na fadhaa.”

2268

“Ushindi wa Amerika,
Pasific umeshika,
Visiwa vilivyotekwa,
Kwanza na Japania.”

2269
"Visiwa vya Marshall,
Vilivyotekwa awali,
Bendera ya wakatili,
Imekwisha kutuliwa."

2270
"Huu ni mfano,
Bora wa maungano,
Baharini kwa pigano,
Bara na katika hewa."

2271
"Sasa inatazamiwa,
Pasific ya kuwa,
Mwendo utaendelea,
Kuliko ulivyokuwa."

2272
"Zimetokea dalili,
Zinazoonyesha kweli,
Kuwa nguvu ya awali,
Japani imepungua."

2273
"Vyombo vyao vya mafuta,
Hasa madege ya vita,
Ulegevu yamepata,
Wajapani wajutia."

2274
"Wajapani wameona,
Sasa maana hapana,
Mpaka wa nje sana,
Kuzidi kushikilia."

2275
"Wanaona hatari,
Kuamru manowari,
Kuwa katika shari,
Mbali ya chao kisiwa."

2276
"Katika jambo hili,
Wamefanya akili,
Sababu wakiwa mbali,
Waona wanazidiwa."

2277
"Wameona kwa hakika,
Nguvu ya Amerika,
Pwani haina mpaka,
Hata katika hewa."

2278
"Hiana ya kurukia,
Pearl Harbour kwa hatia,
Sasa imewaletea,
Wajapani udhia."

2279
"Japani alipotaka,
Kuteta na Amerika,
Nguvu isiyo mpaka,
Ujingani alingia."

2280
"Alingia ujingani,
Watu watazame shani,
Amerika na Japani,
Ni tofauti si sawa."

2281
"Waingereza na Waamerika,
Ahadi wameweka,
Japo kwa kubwa sadaka,
Kuteta na Japania."

2282
"Vita vikidumu sana,
Tumeapa kupigana,
Vita vikitisha sana,
Tumeapa kufa pia."

2283
"Japani katupa madhara,
Mengi kuliko hasara,
Zilizovuta hasira,
Ya Amerika elewa."

2284
"Mateso tuliyopata,
Yashinda yaliyovuta,
Wenzetu katika vita,
Na silaha kuinua."

2285
"Katika vita vya Burma,
Na Bengal lazima,
Kiume tutasimama,
Na msaada kutoa."

2286
"Vita tutavishika,
Tuwape Waamerika,
Msaada wa haraka,
Pamoja na China pia."

2287
"Kila tunapokutana,
Na Japani kupigana,
Tutaharibu sana,
Nguvu yake ya hewa."

2288
"Wavulana wenye nguvu,
Stadi na welekevu,
Wenye mishipa mikavu,
Sukani wamepewa."

2289
"Admeli Mountbatten,
Kaamsha majeshini,
Nguvu na matumaini,
Ya watu aliopewa."

2290
"Majeshi aliyopewa,
Hasa yamekusudiwa,
Burma kuikomboa,
Na kutetea India."

2291
"Yamekusudiwa sana,
Yafungue njia tena,
Inayokwenda China,
Kama ilivyokuwa."

2292
"Twaweza kupeleka,
Shambulio likafika,
Hata nyuma ya mpaka,
Wa Wajapani sikia."

2293

“Wajapani kadhalika,
Waweza kuzunguka,
Hata nyuma ya mpaka,
Fujo wakatutilia.”

2294

“Mapigano ya kutisha,
Mbele yanaendeshwa,
Bali sitabahatisha,
Matokeo kuwambia.”

2295

“Zaidi ya mara tatu,
Au mara nne watu,
Hufa kwa silaha zetu,
Hilo latosha kujua.”

2296

“Sifa ya uhodari,
Wa vita katika pori,
Tuliyopata habari,
Ya Japani imevia.”

2297

“Waingereza na Wahindi,
Wamechukua ufundi,
Wajapani hawashindi,
Kama walivyokuwa.”

2298

“Kasikazini kwa mbali,
Jemadari Stilwell,
Yumo katika shughuli,
Vita kuvishikilia.”

2299

“Amepewa askari,
Waamerika hodari,
Kwa vita katika pori,
Kazi inaendelea.”

2300

“Amepewa na Machina,
Wawezao kupigana,
Vita kila namna,
Porini vikitokea.”

2301

“Manowari zimetiwa,
Bahari ya India,
Chini ya mtu shujaa,
Kulinda kila njia.”

2302

“Admeli Somerville,
Yuko upande ule,
Na manowari teule,
Tayari kushambulia.”

2303

“Japani akichagua,
Pasific kukimbia,
Bahari ya India,
Atakuta angojewa.”

2304

“Karibu itatubidi,
Kufanya jitihadi,
Kubwa inayotubidi,”
Hotuba ikatulia.

2305

Wakati wa kusemeka,
Hayo niliyoandika,
Vilikuwa vikiwaka,
Vita namna moja.

2306

Viliwaka mfulizo,
Kila upande mkazo,
Ukawapa mzozo,
Watu waliozuia.

2307

Ngurumo za mizinga,
Na ndege katika anga,
Masikio zilifunga,
Kwa wingi zilivyokuwa.

2308

Shindo la mabombomu,
Utadhani Jahanamu,
Na wakati umetimu,
Dunia kuhukumiwa.

2309

Shindo la makombora,
Yaliyotia hasara,
Lilitaka watu bora,
Wawezao vumilia.

2310

Tena mafaru ya chuma,
Kwa nguvu yalititima,
Pakawa kama kiama,
Karibu kitatokea.

2311

Namna yalivyovuma,
Hayo mafaru ya chuma,
Kama si shujaa mwema,
Woga utakuingia.

2312

Juu kulifunga wingu,
Kwa madege ya Kizungu,
Na mabomu machungu,
Chini yakatapakaa.

2313

Zilijimwaga risasi,
Zikatata kama bisi,
Vita vikashika kasi,
Kuliko vilivyokuwa.

2314

Watu waliozimwaga,
Kwao walikwisha aga,
Kitu kiitwacho woga,
Kabisa hawakujua.

2315

Kwao woga ni mgeni,
Ambaye hajulikani,
Asiyetia moyoni,
Shaka wala fadhaa.

2316

Kwao kizito chepesi,
Na kigumu ni rahisi,
Tisho si wasiwasi,
Kwao yote sawasawa.

2317

Walikuwa ni watesi,
Wasio na wasiwasi,
Na shabaha hawakosi,
Bunduki wakiinua.

2318

Shabaha wakichagua,
Ni vigumu kukosea,
Na kama haikuua,
Jeraha itatia.

2319

Kila mtesi ni simba,
Mwenye ari ya kugomba,
Na imara kama mwamba,
Hali alivyokuwa.

2320

Watesi wa Kidachi,
Ambao vita hawachi,
Na Wahuri kuku kuchi,
Vita wakavizua.

2321

Ndipo aliposimama,
Kesselring kusema,
“Wadachi msende nyuma,
Wala kujitolea.”

2322

“Yatupasa kusimama,
Tupigane heshima,
Bila mtu kutetema,
Wala kubadili nia.”

2323

“Shime tutetee Rumi,
Ili tuwe na ulimi,
Wa kutangaza uvumi,
Kuwa sisi mashujaa.”

2324

“Rumi ikitupotea,
Shindo kubwa litakuwa,
Kuliko lililokuwa,
Paris tulipotwaa.”

2325

“Tulipoteka Paris,
Watu wengi walikisi,
Wadachi hawakosi,
Watatawala dunia.”

2326

“Hata sasa dhana hiyo,
Watu wengine wanayo,
Tukaze mashambulio,
Ama tutabeuliwa.”

2327

“Kubeuliwa vibaya,
Mtu hawi na wasaa,
Na taifa hulemewa,
Na dharau ya dunia.”

2328

“Watu watuheshimuo,
Wakiona twenda mbio,
Watavunjikwa na moyo,
Haifai hili kuwa.”

2329

“Nimeandika barua,
Kwa Hitler kumwambia,
Rumi nitaizuia,
Awni nikiletewa.”

2330

“Kama barua kapata,
Yamkini ataleta,
Watu na zana za vita,
Kwa haraka Italia.”

2331

“Hivi sasa nafikiri,
Majeshi ya askari,
Yamo katika safari,
Kuja kutusaidia.”

2332

“Shaka acheni kutia,
Wala kuwa na fadhaa,
Awni itatujia,
Nisemayo naelewa.”

2333

“Shikeni yangu kauli,
Ninayowambia kweli,
Msibadilishe hali,
Rumi ikatupotea.”

2334

“Rumi ikitupotea,
Hapana asiyejua,
Sifa ya ushujaa,
Udachi itapotea.”

2335

“Itapotea fahari,
Pepo ya uaskari,
Majeshi ya uhuri,
Rumi yakiingia.”

2336

“Fahari ikiondoka,
Kurudi tena mashaka,
Shime vita kuvishika,
Tuzuie hili kuwa.”

2337

“Kushindwa kunakera,
Kwa taifa ni hasara,
Bei ya roho hasira,
Afadhali kujifia.”

2338

“Heri tufe twapigana,
Kuliko mwisho kuona,
Heshina hapana tena,
Imekwisha chukuliwa.”

2339

“Yatupasa tusimame,
Meno yetu tuyaume,
Na tupigane kiume,
Hali itakavyokuwa.”

2340

“Imepasa tujikaze,
Mapigano yafulize,
Wala tusichezecheze,
Wakati umewadia.”

2341

“Vita vya kwanza si kitu,
Vya leo ndiyo msitu,
Na wakutane watu,
Kufyeka wanaojua.”

2342

“Watu nilio nao,
Najua katika moyo,
Kuwa ndiyo tegemeo,
Langu la kutegemea.”

2343

“Heri wote tungekufa,
Kuliko kukosa sifa,
Haliwi bora taifa,
Kama halikusifiwa.”

2344

“Shime vita tuendeshe,
Mauti yasitutishe,
Hata sisi sote twishe,
Ama tushinde dunia”

2345

“Mauti ya askari,
Nyuma huacha fahari,
Ambayo watakariri,
Watu wajao nyuma.”

2346

“Ni urithi maridhawa,
Kwa watakozaliwa,
Kuja kuona haya,
Ambayo tutawaachia.”

2347

“Hitler alitutaka,
Tuondoke Afrika,
Ili tuweze kushika,
Hivi vita vya Ulaya.”

2348

“Hili nawajulisha,
Kusudi kuwakumbusha,
Kuwa tuli amrishwa,
Kule majeshi kutoa.”

2349

“Hitler aliona,
Kuwa hapana maana,
Kuzidi kupigana,
Pande zile za dunia.”

2350

“Lakini hapa tulipo,
Ndipo yeye atakapo,
Sisi tuape kiapo,
Kuonyesha ushujaa.”

2351

“Haitupasi kuchoka,
Wala nyuma kugeuka,
Dunia itatucheka,
Kama tutajitolea.”

2352

“Linaishi kila mara,
Duniani jina bora,
Unapokwenda ahera,
Mwili na kujiozea.”

2353

“Katika vita vya kwanza,
Sisi na Waingereza,
Ushindi tulipoteza,
Kwa hiana kutokea.”

2354

“Mambo yaliyotokea,
Elfu na tisa mia,
Kumi na nane sikia,
Ni aibu tena kuwa.”

2355

“Vita vimeandaliwa,
Aibu kuizuia,
Tusiingie fadhaa,
Mioyo ikalegea.”

2356

“Vimeandaliwa sana,
Fedheha isije tena,
Mwisho umeonekana,
Kuwa tutafanikiwa.”

2357

“Na tupige moyo konde,
Vita vikubwa tutende,
Tutete hata tushinde,
Ishuhudie dunia.”

2358

“Tumwonyeshe adui,
Kwamba hatupendelei,
Kila tukiwa hai,
La unyonge kutendewa.”

2359

“Moyoni tutie wivu,
Tusifanye ulegevu,
Tena tukaze mbavu,
Aibu kuiondoa.”

2360

“Vita hivi vya hiari,
Tupigane kwa dhamiri,
Tena bahati nzuri,
Mwisho imetabiriwa.”

2361

“Hitler tulimkiri,
Si faida kughairi,
Aibu ya askari,
Ni amri kukataa.”

2362

“Jicho la Hitler kali,
Huona yaliyo mbali,
Na mambo mbalimbali,
Yeye huyapambanua.”

2363

“Mtu akitoa hoja,
Kuvunja wetu umoja,
Afahamu yamngoja,
Hukumu ya kuuawa.”

2364

“Heri kufa kwa adui,
Kuliko kubaki hai,
Na kuona vita hii,
Kuwa imetupotea.”

2365

“Nafahamu kwa hakika,
Kila jambo hugeuka,
Mwisho wetu wa mashaka,
Heri itatuchekea.”

2366

“Tuunge kama mkufu,
Tupigane bila hofu,
Ama sivyo utukufu,
Wetu utapotea.”

2367

“Tuwe kama mnyororo,
Bila kiungo chororo,
Tuwaonye mgogoro,
Watu wanaotujia.”

2368

“Mnyororo nisemao,
Ukikatika leo,
Watoto wetu wajao,
Kuunga hawatajua.”

2369

“Watabatika vijana,
Walani yetu majina,
Haya shime kupigana,
Mpaka kufanikiwa.”

2370

“Tuunge kama mpira,
Usiokatika mara,
Tena tufanye duara,
Hitler kumtetea.”

2371

“Tujiunge kwa tabaka,
Tupigane tukicheka,
Mwisho wa jua masika,
Nadhani mwaelewa.”

2372

“Nasikitika kunena,
Adui mwerevu sana,
Lakini ndivyo namna,
Ya vita inavyokuwa.”

2373

“Adui huyu mwerevu,
Anataka ushupavu,
Na mapigo ya nguvu,
Yafulize kumwendea.”

2374

“Adui yetu jasiri,
Kila wakati hodari,
Nawambia askari,
Mzidi kujiandaa.”

2375

“Adui yetu tayari,
Kama simba wa pori,
Hapana hila nzuri,
Yeye asiyoelewa.”

2376

“Adui huyu thabiti,
Anapigana kwa dhati,
Sharti tuwe madhubuti,
Katika kumzuia.”

2377

“Ana nguvu ya kukinga,
Na atakapo husonga,
Kila nikivipanga,
Vita hunichafukia.”

2378

“Milele vita vya juu,
Sisi sifa yetu kuu,
Lakini wakati huu,
Naona si sawasawa!”

2379

“Hili linanishangaza,
Silijui la kuwaza,
Wala la kufanyiza,
Natunga na kutangua.”

2380

“Kwanza alijilegeza,
Tukadhani tutaweza,
Mwisho kumwangamiza,
Kumbe vile ni hadaa!”

2381

“Kila nikirakibisha,
Njia ya kumtisha,
Huwa yeye amekwisha,
Mwendo wangu kuelewa.”

2382

“Tulidhania dhaifu,
Kumbe vile maarufu,
Wala hajui hofu,
Katika kushambulia.”

2383

“Anaposhika kashika,
Mkono shida kutoka,
Mashujaa nawataka,
Wawezao kuzuia.”

2384

“Adui yetu stadi,
Ana moyo wa juhudi,
Anataka ukaidi,
Umwendee kila saa.”

2385

“Nashangaa nikiwaza,
Mambo ya Waingereza,
Jinsi wanavyotengeza,
Vita na kushambulia.”

2386

“Adui nimemsifu,
Kusudi kuwaarifu,
Mashujaa watukufu,
Wajue la kutumia.”

2387

“Kitu usichokijua,
Pengine kina udhia,
Ndipo nikasema haya,
Watu wapate elewa.”

2388

“Kusudi nimemsifu,
Tuandae marudufu,
Pigo la kutia hofu,
Adui akitokea.”

2389
"Hilo tusipolitenda,
Lazima Alexander,
Italia atashinda,
Tuzidi kuchafukiwa."

2390
"Nataka wote tuape,
Kuwa na moyo mweupe,
Hitler tusimtupe,
Watu wakatzomea."

2391
"Tutafanywa si kitu,
Mbele ya macho ya watu,
Kama huyu bwana wetu,
Hana pa kutegemea."

2392
"Ingawa kila mkubwa,
Hufanya mdogo mbwa,
Na asemalo huzibwa,
Vema ni kuvumilia."

2393
"Neno la uhaini,
Mwaelewa nadhani,
Kuwa hutoa thamani,
Taifa likiambiwa."

2394
"Kisa cha kutaja mbwa,
Msiudhike wakubwa,
Nataka lililozibwa,
Liwe wazi mara moja."

2395
"Njia ya mafafanuzi,
Usemalo liwe wazi,
Ni kuwapa wasikizi,
Mfano wanaojua."

2396
"Kisa cha kusema hivi,
Msidhani ni mlevi,
Wala nia ya ujuvu,
Sina nawaapia."

2397
"Nia mfano wa hiyo,
Haimo katika moyo,
Ila nimesema hayo,
Kusudi kufafanua."

2398
"Kabla haya mashaka,
Hitler angenitaka,
Shauri ningetamka,
Kuwa hatafanikiwa."

2399
"Lakini kauli hiyo,
Hakupata kuwa nayo,
Kukimbia maji siyo,
Nguo ukiyavulia."

2400
"Ukivua nguo oga,
Aibu kusagasaga,
Miguu chini kwa woga,
Maji ukayakimbia."

2401
"Yatakayokuja kesho,
Leo yasitupe tisho,
Na la jana sikitisho,
Vema kutokumbukia."

2402
"Haifai kukimbia,
Wala vita kuachia,"
Mwisho wa kusema haya,
Kesselring kanyamaa.

2403
Alexander halafu,
Watu aliwaarifu,
"Tumepewa utukufu,
Tulioko Italia."

2404
"Sisi tumetukuzwa,
Tupige konde la kwanza,
Na majeshi yatengezwa,
Ufaransa kuingia."

2405
"Hii kwetu ni alama,
Bora sana ya heshima,
Ambayo itasimama,
Hata mwisho wa dunia."

2406
"Kufutika ni vigumu,
Kumbukumbu hii tamu,
Kila watu wakidumu,
Hapa watakumbukia."

2407
"Imepasa kazi hii,
Ifanywe kwa bidii,
Afukuzwe adui,
Rumi iwe huria."

2408
"Kesselring ni Amiri,
Lakini sifikiri,
Kuwa atapata heri,
Katika Italia."

2409
"Upande usio haki,
Daima hupata dhiki,
Na mimi sisadiki,
Wadachi kufanikiwa."

2410
"Mungu asiye hiana,
Mambo hubadili sana,
Usiku na mchana,
Ni mfano tumepewa."

2411
"Mfano huu ni bora,
Kwa watu wenye busara,
Kuwa dunia ni dira,
Huzunguka kama pia."

2412
"Kuzunguka kama pia,
Ndiyo mwendo wa dunia,
Na lisilotazamiwa,
Huweza likatokea."

2413

“Mfano tumewekewa,
Kusudi kutegemea,
Na mimi natazamia,
Tutashinda Italia.”

2414

“Vitani tumeingia,
Wanyonge kuwatetea,
Mungu akipendezewa,
Msaada tutapewa.”

2415

“Mungu apendaye haki,
Hatatuacha na dhiki,
Ushindi sisadiki,
Wa Wadachi kutokea.”

2416

“Wadachi shujaa sana,
Lakini haki hawana,
Inatosha kuwa laana,
Juu ya watu hawa.”

2417

“Isitoshe nguvu yetu,
Na idadi ya watu,
Na kila zana za vitu,
Matumaini hutia.”

2418

“Nguvu tuliyo nayo,
Yatosha kwa tegemeo,
Naamuru shambulio,
Mbele kuendelea.”

2419

“Siku nyingi zisipite,
Nataka atiwe pete,
Adui mahali pote,
Katika Italia.”

2420

“Siku nyingi hazipati,
Tutakuwa na sauti,
Ya kuwambia umati,
Rumi imeokolewa.”

2421

“Siku nyingi hazishi,
Nguvu zetu za majeshi,
Zitakomesha ubishi,
Na kutuliza dunia.”

2422

“Hasa nia yangu mimi,
Nataka tufike Rumi,
Kabla ya siku kumi,
Tusizidi kuchelewa.”

2423

“Na kila ukipungua,
Muda niliowambia,
Kwangu ndiyo sawasawa,
Tena ndiyo maridhawa.”

2424

“Nataka tushike chuma,
Bila kutazama nyuma,
Adui asipohama,
Rumi awe kazingiwa.”

2425

“Kila mpiga mzinga,
Aupige kwa kulenga,
Bila moyo kumtanga,
Na shabaha kuchagua.”

2426

“Kila mpiga risasi,
Asiwe na wasiwasi,
Afanye kazi halisi,
Ambayo ameijia.”

2427

“Wapigaji bombomu,
Nao imewalazimu,
Kuwa na moyo mgumu,
Watimize ushujaa.”

2428

“Wapiganao kwa singe,
Nawataka wajiunge,
Wapigane kama nge,
Bila shaka kutia.”

2429

“Wapigao makombora,
Nataka watie fora,
Kwa kueneza hasara,
Kila panapotakiwa.”

2430

“Askari wa mafaru,
Nao nawaamru,
Kila panapodhuru,
Wasihofu kuingia.”

2431

“Na askari wa ndege,
Naamru wavuruge,
Kama kundi la nzige,
Shambani likiingia.”

2432

“Kwa tabia yetu nzuri,
Wadachi wanafikiri,
Kuwa hatuwezi shari,
Tena tumelegea.”

2433

“Tuwaonyeshe mishipa,
Ya nguvu isiyonepa,
Ili wapate ogopa,
Tena kutuchezea.”

2434

“Shime wanaume shime!
Vita hivi tuegeme,
Vimalizike tuheme!”
Alexander katua.

2435

Vita vilizidi moto,
Kila upande mzito,
Kuzidi kwa fukuto,
Wadachi wakalegea.

2436

Mara walipolegea,
Kwa hasara kuwangia,
Rumi waliiachia,
Wahuri wakaingia.

2437

Walikimbia wenyewe,
Kama kuku na wanawe,
Anapotokea mwewe,
Hushindwa kuwatetea.

2438

Hapa sasa tubadili,
Twende mpaka wa pili,
Ambao Churchill,
Amekwisha kutwambia.

2439

Twende kwenye mpaka,
Vita vilikofanyika,
Wahuri waliposhuka,
Ufaransa kukomboa.

2440

Staghafiru kauli,
Kabla ya kwenda mbali,
Mawazo ya awali,
Ya Hitler 'tawambia.

2441

'Tafanya muhtasari,
Kwa michache misitari,
Hitler yake dhamiri,
Nipate kusimulia.

2442

'Tasimulia kiada,
Bila kupoteza muda,
Nifunue na rada,
Ya kunuia mabaya.

2443

Adui alitangaza,
Ya kuwa Waingereza,
Kushuka hawataweza,
Na kiapo akatoa.

2444

Kiapo alifanyiza,
Wakija Waingereza,
Wote wataangamizwa,
Bila mtu kubakia.

2445

Au watakuta vita,
Vikubwa vyenye matata,
Na njia hawatapata,
Kurudi Britania.

2446

Kwanza wafanye mirathi,
Watoto wao warithi,
Sababu bila hadithi,
Wajao watapotea.

2447

Viko vita vya kioja,
Ng'ambo vinawangoja,
Harudi mtu mmoja,
Kwao kusimulia.

2448

Kama mtu asemalo,
Hutokea lilo hilo,
Angepata atakalo,
Huyu Hitler kwa haya.

2449

Alikuwa ni mwepesi,
Kwa ulimi kujilisi,
Na maneno ya kughasi,
Watu kuwatolea.

2450

Alikuwa na maneno,
Ya sifa na majivuno,
Na mwisho wa mapigano,
Alijidai kujua.

2451

Alitangaza kwa watu,
Muda wa siku tatu,
Ataandaliwa vitu,
Na chai Britania.

2452

Kutoka Berlin,
Kwa vita hata London,
Kwa muda huu duni,
Fikira au kichaa!

2453

Lakini neno si tendo,
Na kujisifu si kondo,
Yote hujitenga kando,
Kweli ikitokea.

2454

Kweli ina bumbuazi,
Hata mbele ya wajuji,
Hufanya maamuzi,
Watu wakaajabia.

2455

Tazameni ubazazi,
Mtu huuzaje ngozi,
Ya simba mwenye pumzi,
Kabla ya kuuawa!

2456

Acha simba hata chui,
Ikiwa bado yu hai,
Ngozi yake kujidai,
Kuuza wajizuzua.

2457

Simba akificha kucha,
Watu huacha kumcha,
Siku atoapo kucha,
Hujuta kumchezea.

2458

Siku ya kuzuka koto,
Midomo huwa mizito,
Ukawa kama mtoto,
Kusema usiyojua.

2459

Kinywa hukauka mate,
La kusema usipate,
Na ukitaka ujute,
Hapana wa kusikia.

2460

Wepesi wa ulimi,
Wa kutangaza uvumi,
Hupotewa na usemi,
Bumbuazi likajaa.

2461

Wadachi kito cha sifa,
Elimu na maarifa,
Wasomaji taarifa,
Kama hii hushangaa.

2462

Watashangaa kuona,
Taifa bora sana,
Kuongozwa kupigana,
Na mtu asiyefaa.

2463

Wadachi watu wa kazi,
Stadi wa maongozi,
Hushangaza wasikizi,
Hili wakilisikia.

2464

Hushangaa na kucheka,
Kusikia alishika,
Enzi na mamlaka,
Mbele ya watu hawa.

2465

Linashangaza ya kuwa,
Kusikia watu hawa,
Vita hivi walitiwa,
Na huyu mtu baa.

2466

Cheo namna hii,
Kupata huyu laghai,
Udachi nzima kutii,
Hutaajabu dunia.

2467

Hushangaa watu wengi,
Kuwa mpakaji rangi,
Aliweza kuwa Mangi,
Wadachi wakaridhia.

2468

Huyu mtu mtundu,
Kawatia penye tundu,
Kusudi rangi nyekundu,
Ya damu kuangamia.

2469

Huwaje taifa hili,
Hitler kumkubali,
Mtu wa tepe mbili,
Mbele ya watu kukaa!

2470

Taifa la wagunduzi,
Lijualo maamuzi,
Herr Hitler bazazi,
Kaweza hulihadaa!

2471

Taifa la wasanifu,
Kila jambo kusarifu,
Katika uharibifu,
Mtu huyu kalitia.

2472

Hili jambo la ajabu,
Latia kinywa ububu,
Alivyoweza ghilibu,
Watu namna ya hawa.

2473

Labda miujiza,
Huyu aliyofanyiza,
Hata haya akaweza,
Wajao watafunua.

2474

Watayafunua wazi,
Wafanye na maamuzi,
Ambayo mimi siwezi,
Leo kuwafanyia.

2475

Maamuzi sitatoa,
Leo hapa nachelea,
Nisihesabu hatia,
Mahali pa haki kuwa.

2476

Ila hapa nawataka,
Tutazame mpaka,
Nyuma niliotamka,
Na vita vilivyokuwa.

2477

Wajibu niseme mwaka,
Na tarehe ya kushuka,
Majeshi ya Washirika,
Katika bara Ulaya.

2478

Mwanzo kuweka mwishoni,
Yalishuka mwezi Juni,
Nne na arobaini,
Elfu na tisa mia.

2479

Tarehe bila matata,
Iliposhuka vita,
Ilikuwa Juni sita,
Mwaka umetangulia.

2480

Siku napenda waone,
Watu wasibishane,
Ilikuwa Jumanne,
Siku ya matendo haya.

2481

Tena Normandy nataja,
Mfahamu mara moja,
Wageni waliokuja,
Ndiko walikoshukia.

2482

Isitoshe natakasa,
Mfahamu kabisa,
Hapa ni Ufaransa,
Waliposhuka huria.

2483

Wakati wa alfajiri,
Nuru bado kudhihiri,
Meli na manowari,
Shehena zilipakua.

2484

Wakati wa asubuhi,
Kabla stafutahi,
Wadachi kutanabahi,
Vita wameletewa.

2485
Wameletewa vita,
Ambavyo bado kupata,
Duniani kupita,
Wala kutazamiwa.

2486
Vita wasivyoota,
Ndivyo vilivyowakuta,
Pakaenea matata,
Pote walipokuwa.

2487
Mwaka huu wa tano,
Tangu kuwa mapigano,
Ikawa ajabu mno,
Wadachi kuona haya.

2488
Na zaidi ya habari,
Churchill Waziri,
Alikuwa na dhamiri,
Ashuke na mashujaa.

2489
Alitaka mwenyewe,
Mbele ya vita awe,
Na mashujaa wenziwe,
Siku ilipowadia.

2490
Alitamani ashuke,
Vita naye akashike,
Na mashujaa wenzake,
Hali itakavyokuwa.

2491
Alitaka naye ende,
Katikati ya makonde,
Awezalo akatende,
Kwa ari ya ushujaa.

2492
Alikuwa askari,
Mwenye jina mashuhuri,
Na moyo wa ujasiri,
Kijana alipokuwa.

2493
Ni simba katika kondo,
Kwa maneno na matendo,
Wala hahofu mshindo,
Yajua yote dunia.

2494
Simba katika mshindo,
Ndipo afanyapo kondo,
Kuzidi kukaa kando,
Hakuweza vumilia.

2495
Simba anapochokochwa,
Ndipo apigapo kucha,
Churchill kujificha,
Nyuma hakuridhia.

2496
Kiu ya upiganaji,
Haizimiki kwa maji,
Wala haina kinywaji,
Ila kujipigania.

2497
Waziri vitani kwenda,
Wengi hawakupenda,
Sababu wa kutenda,
Kaziye hakutokea.

2498
“Wewe kwetu kama rasi,
Usifanye wasiwasi,
Twachie sisi utesi,”
Churchill kaambiwa.

2499
“Waachie vita vijana,
Wewe usende pigana,
Na inshallah utaona,
Mwisho utakavyokuwa.”

2500
“Usitie moyo joto,
Vita wachie watoto,
Kazi yako nyuma nzito,
Nani utamwachia?”

2501
“Wote Waingereza,
Kupigana tunaweza,
Lakini unavyowaza,
Hapana anayejua.”

2502
“Wewe ukenda vitani,
Nyuma atakaa nani?
Tafadhali Winston,
Hili hatupendi kuwa.”

2503
“Kazi ya nyuma twaona,
Ilivyo nzito sana,
Inataka bega pana,
Dogo halitachukua.”

2504
“Tena tunakukumbusha,
Vita kwetu vilitisha,
Mungu kavibadilisha,
Wewe ulipotokea.”

2505
“Jambo hili ni thabiti,
Halitaki matafiti,
Na bila ya tofauti,
Twaweza kukuapia.”

2506
“Twaweza kuapa kuwa,
Tangu ulipotokea,
Vita ukaviandaa,
Adui yetu kavia.”

2507
“Kavia hana wasaa,
Imemjaa fadhaa,
Na sasa kutupotea,
Hili hatutaridhia.”

2508
“Sisi wengine wote,
Tutakwenda tukatete,
Mradi wetu tupate,
Uongozi maridhawa.”

2509

"Mungu ametupa sudi,
Mbele ya ukaidi,
Kazi yako ya juhudi,
Kuikosa twahofia."

2510

"Bahati tuliyopata.
Hatupendi kuikata,
Na kila anayetweta,
Mtu atakufidia."

2511

"Jambo hili twatamani,
Tupe usituhini,
Yaliyo mwako moyoni,
Sema utatendewa."

2512

"Lo lote tutatenda,
Isipokuwa twapenda,
Wewe uache kwenda,
Kama ulivyoniua."

2513

"Usiwe na mshawasha,
Vita karibu ya kwisha,
Utakalo amrisha,
Lazima litakuwa."

2514

"Tuongoze tushinde,
Vita kila upande,
Lakini wewe usende,
Tukapatwa na ukiwa."

2515

"Uliyotenda yatosha,
Jina kulisimamisha,
La ukumbusho maisha,
Lako katika dunia."

2516

"Yanatosha kuandika,
Jina lisilofutika,
Na moyoni kukumbuka,
Kila kizazi sikia."

2517

"Wewe umetenda shani,
Kubwa isiyo kifani,
Kufutika abadani,
Katika hii dunia."

2518

"Umebadili matata,
Mazito tuliyopata,
Kama umeme kumeta,
Hapana asiyejua."

2519

"Kipawa cha maongozi,
Alichokupa Mwenyezi,
Kimeleta waziwazi,
Faida Britania."

2520

"Kimeokoa Enzi,
Ambayo chama cha Nazi,
Kilikusudia wazi,
Heshima kuivunjia."

2521

Walikutana mabwana,
Maarufu kwa majina,
Wateule kwa kunena,
Nasaha hii kutoa."

2522

Mfalme jambo hili,
Naye hakulikubali,
La kumwacha Churchill,
Vitani kujitia."

2523

Basi alinasihiwa,
Atakalo kutokuwa,
Hata alipotulia,
Rai nyingi zimekuwa."

2524

Churchill kuridhika,
Silaha kutokushika,
Majeshi yaliyoshuka,
Ng'ambo yamefanikiwa."

2525

Wadachi kuona hali,
Vita vimejibadili,
Wakaulizana swali,
"Nani sasa katujia?"

2526

"Namna ya shambulio,
Tujuayo sasa siyo,
Tena twaona tokeo,
Ghafia kuchafukiwa."

2527

"Amiri wa maadui,
Wa sasa hatumjui,
Na vita namna hii,
Kwetu bado kutokea."

2528

"Huyu tangu ashuke,
Twaona mwendo wake,
Hataki apumzike,
Kusita na kushangaa."

2529

"Kila apigapo kumbo,
Hutuharibia mambo,
Na tangu ashuke ng'ambo,
Vita vimetuchachia."

2530

"Ndege zisizo rubani,
Tumeeneza hewani,
Lakini si kifani,
Bora za Britania."

2531

Wakaambiwa habari,
"Kashuka Montgomery,
Huyo ndiye jemadari,
Attendaye mambo haya."

2532

"Katika wasifiwao,
Anatajwa mtu huyo,
Tena hajui kileo,
Tangu alipozaliwa."

2533

“Kimo chake wastani,
Ana akili razini,
Bado kwenda ulevini,
Tumbaku hajatumia.”

2534

“Ndiye aliyetukuka,
Vita vya Afrika,
Akatanua mpaka,
Sicily na Italia.”

2535

“Na nyuma kategemea,
Eisenhower shujaa,
Huyo akiandaa,
Huyu hushambulia.”

2536

“Wa tatu katika hawa,
Alexander sikia,
Hapa hajatokea,
Bado yuko Italia.”

2537

“Hitler amekubali,
Kumleta Rommel,
Akipata dalili,
Ya Benard kutujia.”

2538

Hitler alisadiki,
Rommel hashindiki,
Na kila penye dhiki,
Yeye huwa kama dawa.

2539

Benard Montgomery,
Na Rommel nakariri,
Walikwisha fanya shari,
Rommel akakimbia.

2540

Walionyeshana vita,
Haraka bila kusita,
Rommel hakupata,
Hila ila kukimbia.

2541

Laiti asingeruka,
Akatoka Afrika,
Angalikuwa mateka,
Bila jingine kuwa.

2542

Sasa kuja kwake mbio,
Katika mashambulio,
Akakutana na kwao,
Ndege za Britania.

2543

Hizi zilitafuta,
Njia atakayopita,
Siku zilipopata,
Jeraha akatiwa.

2544

Hili jeraha baya,
Nguvu lilimtoa,
Kila alivyotibiwa,
Afya haikurejea.

2545

Jeraha lilimdhili,
Baada ya juma mbili,
Mauti ya Rommel,
Watu wakatangiwa.

2546

Salama yake ile,
Nyembamba kama unywele,
Ya kuepa vita kule,
Tena haikutokea.

2547

Paris wakati huo,
Wadachi hawanayo,
Wamekwisha kwenda mbio,
Na vita vinawendea.

2548

Vinawendea kwa kasi,
Bila kuwapa nafasi,
Wakawa na wasiwasi,
Mioyoni na fadhaa.

2549

Mfalme Uingereza,
Hili lilimpendeza,
Cheo akaagiza,
Montgomery kupewa.

2550

Alimpa uamiri,
Juu ya ujemadari,
Zaidi hidaya nzuri,
Ngao ya ushujaa.

2551

Hii ni ngao ya mti,
Yenye vito bora kati,
Apataye hii sharti,
Awe ni mtu shujaa.

2552

Ina sanamu za simba,
Kumi na nane kwa namba,
Kwa nakshi imepambwa,
Dhahabu ndiyo maua.

2553

Imefunikwa hariri,
Rangi yake yanawiri,
Kama johari nzuri,
Zambarau shabihia.

2554

Tena imeandikwa:—
“Kwa Mfalme yatoka,
George aliyetukuka,
Wa Sita Britania.”

2555

“Mfalme Ireland,
Hata Bara ya Hindi,
Na nchi nyingine kundi,
Milki za dunia.”

2556

“Tunu hii ya Amiri,
Benard Montgomery,
Shujaa mashuhuri,
Ambaye kajiteua.”

2557

"Huu ni ushahidi,
Wa kutimiza muradi,
Kwa moyo wa juhudi,
Kama ulivyotakiwa."

2558

Mwezi mosi Septemba,
Siku yake ya kupambwa,
Montgomery kilemba,
Heshima ya ushujaa.

2559

Kadhalika naarifu,
Tuepuke upungufu,
Tupate ukamilifu,
Mambo yaliyotokea.

2560

Mfalme kadhalika,
Alipenda kumvika,
Mtu aliyewekwa,
Kilemba Italia.

2561

Huyu ni Alexander,
Ambaye alitenda,
Vita hata akashinda,
Na Rumi kuiokoa.

2562

Alipewa uamiri,
Kama Montgomery,
Na zawadi mashuhuri,
Kama nilivyowambia.

2563

Harold Alexander,
Cheo chake kilipanda,
Rumi iliposhindwa,
Juni nne Italia.

2564

Elfu na tisa mia,
Arobaini pamoja,
Nne mwisho ikitiwa,
Mwaka wao wa hidaya.

2565

Simba wa kwanza Harold,
Na wa pili ni Benard,
Ndiyo wazimao radi,
Ya vita ikatulia.

2566

Hawa watu wawili,
Ndiyo vitara vikali,
Wametukuka kwa kweli,
Upande wa Britania.

2567

Ni mashujaa halisi,
Vitani hawapapasi,
Adui hana nafasi,
Hawa wakihudhuria.

2568

Kila vinapowaka,
Vita hawa wakifika,
Moto wake huzimika,
Ukawa kama makaa.

2569

Hawa wanapobarizi,
Vitani kwa shambulizi,
Adui yao hawezi,
Kabisa kufanikiwa.

2570

Mahali penye matata,
Wakifika yatatota,
Ndiyo wazimao vita,
Kama maji kumwagiwa.

2571

Wakimwegema hasidi,
Kama nyuma harudi,
Hatimizi muradi,
Ila kuangamia.

2572

Wakiteta na adui,
Kama nyuma hakimbii,
Atapoteza uhai,
Ghafla bila kujua.

2573

Hiyo ndiyo mizimu,
Watu wanayoheshimu,
Achezeaye hadumu,
Mara huaga dunia.

2574

Majina yao yavuma,
Katika dunia nzima,
Tena yatasimama,
Hata mwisho wa dunia.

2575

Hawa tuwaache sasa,
Kipo kingine kisa,
Sipendi wakakikosa,
Wasomaji wa haya.

2576

Yupo shujaa Mdachi,
Mkorofu vita hachi,
Habari yake sifichi,
Hapa kusimulia.

2577

Mtu huyu ni wa pili,
Wa mfano wa Rommel,
Jina nitalinakili,
Mzidi kufunukiwa.

2578

Aitwa Von Rundstedt,
Kaja kuhani mauti,
Mwamuzi wa umati,
Rommel kumlilia.

2579

Von Rundstedt hirizi,
Kwa Hitler ni kipenzi,
Na katika shambulizi,
Akiwapo huwa baa.

2580

Ni askari mweledi,
Imara na mkaidi,
Aliyetoa ahadi,
Hitler kumtetea.

2581

Katika uaskari,
Cheo chake ni Amiri,
Mkali kama namiri,
Au chui wa Asia.

2582

Huyu alijivuna,
Kwa kujua kupigana,
Vita vya kila namna,
Hana mwenziwe wa sawa.

2583

Alikuwa ni jahili,
Wa kupenya mahali,
Kama vile methali,
Sindano au shazia.

2584

Vita kwake kitambaa,
Hupenya na kutoboa,
Hajapata kukwaa,
Tangu alipozaliwa.

2585

Jeshi lake kwa mfano,
Nafananisha maneno,
Watu waelewe mno,
Kama hivi lilikuwa.

2586

Lilikuwa kama uzi,
Usio na kizuizi,
Hupita palipo wazi,
Ilipopenya shazia.

2587

Ni jeshi la askari,
Lililowekwa tayari,
Lenye silaha nzuri,
Na watu wa kuchagua.

2588

Hilo liliandaliwa,
Makusudi kuzuia,
Siku inapotokea,
Udachi kushambuliwa.

2589

Liliandaliwa sana,
Kwa zana kila aina,
Lipigane kiungwana,
Siku ya kutakiwa.

2590

Lipigane kwa juhudi,
Pasipo nyuma kurudi,
Liweke na ushahidi,
Kwao wa ushujaa.

2591

Lipigane bila hofu,
Kutetea utukufu,
Bila kuona uchofu,
Uvivu na kulegea.

2592

Na huyu aliyekaa,
Mbele kutangulia,
Kama ilivyotakiwa,
Alikuwa sawasawa.

2593

Hana usiri kidogo,
Mara huanzisha pigo,
Kubwa la mvurugo,
Linaloleta fadhaa.

2594

Hana zohali kupiga,
Kama jiwe la kusaga,
Akabilipo huchaga,
Vita vikatishia.

2595

Kwao watu humsifu,
Vita vilivyo na hofu,
Kwake huwa hafifu,
Mara akihudhuria.

2596

Hana hofu wala shaka,
Tisho kwake ni dhihaka,
Ndivyo anavyosifika,
Huyu ninayewambia.

2597

Sifa za ushujaa,
Zote alizosifiwa,
Kutimiza kanuia,
Bila moja kupungua.

2598

Sifa mfano wa hizi,
Kuzitimiza ni kazi,
Lakini huyu Nazi,
Fahari zilimtia.

2599

Aliona mzigo,
Wa sifa hizi mdogo,
Kwa sababu ya togo,
Nyingi alizopewa.

2600

Kwa sifa hizi za kwao,
Alijidhani ni ngao,
Akaja vitani mbio,
Kutimiza mambo haya.

2601

Alitaka kutimiza,
Wengine wasiyoweza,
Mbele ya Waingereza,
Kwa vile kusifiwa.

2602

Kakuta upiganaji,
Sasa uko Belgiji,
Hapo akahitaji,
Marafiki kuzuiwa.

2603

Kabla vita kuanza,
Alifanya baraza,
Hotuba akaeleza,
Ya ari kwa mashujaa.

2604

“Kesho vita nitaanza,
Ili kuzuia giza,
Ambalo limeanza,
Udachi kukaribia.”

2605

"Nawataka mwende mbele,
Mfano kama mshale,
Hapana polepole,
Sasa wala kuchelewa."

2606

"Nataka askari,
Kwenda nyuma wasikiri,
Wala hapana usiri,
Niwezao vumilia."

2607

"Kwa heshima kupotea,
Sihimili kukawia,
Dakika naona saa,
Na siku mwaka mmoja."

2608

"Shime kuangamiza,
Majeshi ya Waingereza,
Sifa yetu inaoza,
Kwa sababu ya hawa."

2609

"Mataifa ya Ulaya,
Nadhani mwaelewa,
Karibu kujitolea,
Kama si watu hawa."

2610

"Kama si Waingereza,
Vitani kujiingiza,
Tungekwisha angamiza,
Wengine wote Ulaya."

2611

"Waingereza daima,
Hutuvunjia heshima,
Na hili kulitazama,
Moyo waona vibaya."

2612

"Wanavunja utukufu,
Wetu na umaarufu,
Sisi na watu dhaifu,
Pamoja twahesabiwa."

2613

"Pato letu hawapendi,
Uingereza na Poland,
Kati maili kundi,
Lakini wamejitia."

2614

"Urafiki wetu sisi,
Na Stalin Mrussi,
Ulikuwa muhtasi,
Hawa wameufumua."

2615

"Wamevuta Amerika,
Vita kuvishika,
Ambayo kwa hakika,
Imetengwa na Ulaya."

2616

"Wameleta na Wanyika,
Watu wa Afrika,
Rangi yao kutupaka,
Tuzomewe na dunia."

2617

"Watu weusi wabaya,
Wasiojua tabia,
Vile vile wametiwa,
Vitani kusaidia."

2618

"Zaidi ya Ugiriki,
Sasa hata Uturuki,
Na Misri ni rafiki,
Kwao zimeingia."

2619

"Asia imo vitani,
Kupigana na Jermani,
Isipokuwa Japani,
Kando imejikalia."

2620

"Kwa vile kukaa kando,
Imo katika mshindo,
Tazameni matendo,
Haya ya Britania!"

2621

"Wamefanya tashtiti,
Hata wametusaliti,
Tupigane na umati,
Wote katika dunia."

2622

"Mara wakisikia,
Sisi tunaendelea,
Bure hutukamia,
Mwendo wakatufujia."

2623

"Hii ni tabia yao,
Waliozoea kwao,
Kupigana na wenzao,
Japo hawana hatia."

2624

"Ni walimu wakuu,
Wafundishao makuu,
Hata yakatudharau,
Mataifa ya dunia."

2625

"Hawataki zuio,
Kwa mambo wayatendayo,
Lakini wengineo,
Wakiyatenda hatia."

2626

"Dunia waiamru,
Yote iwe na uhuru,
Hili sawa na kufuru,
Wote kuwa sawasawa."

2627

"Wote wakiwa sawa,
Kama watakavyo hawa,
Siku itatokea,
Tule na wanyama bia."

2628

"Wanatakiwa washenzi,
Nao wawe na enzi,
Hili kwa chama cha Nazi,
Haliwezi kuridhiwa."

2629

“Siku hiyo ya vioja,
Duniani ikija,
Itaondoa faraja,
Na kuvunja mazoea.”

2630

“Kwa Waingereza si neno,
Kwa Wadachi zito mno,
Mishipa yetu na kano,
Haiwezi kuchukua.”

2631

“Hitler amenuia,
Jambo hili kuzuia,
Na sisi twatazamiwa,
Sadaka tutajitoa.”

2632

“Hili tukilitenda,
Sifa yetu itapanda,
Ama sivyo itakwenda,
Watu wasikorejea.”

2633

“Nia tusibadili,
Tuzuie jambo hili,
Hitler chakula hali,
Tumboni kikatulia.”

2634

“Chakula chake hali,
Kikatulia na mwili,
Na usingizi halali,
Kwa mawazo na fadhaa.”

2635

“Riziki haoni tamu,
Kwa wasiwasi na hamu,
Anataka yatimu,
Mambo aliyonua.”

2636

“Adui mambo hayo,
Asema kuwa ni choyo,
Lakini ndiyo upeo,
Na ubora wa dunia.”

2637

“Na juzijuzi karibu,
Ingetokea aibu,
Ambayo wangehesabu,
Watu nia yetu mbaya.”

2638

“Hitler alitegewa,
Bomu kumpasukia,
Karibu angeuawa,
Lakini kajiokoa.”

2639

“Chini alianguka,
Watu wakastuka,
Wakadhani yamefika,
Mauti kumchukua.”

2640

“Waliotenda hili,
Wanasemwa si wa mbali,
Ila ni wafedhuli,
Waliobadili nia.”

2641

“Hawa watatahayari,
Siku ikidhihiri,
Ya kufikia fahari,
Ambayo tumenuia.”

2642

“Sasa wajibu wetu,
Ni kupigana tu,
Hata heshima yetu,
Irudi kiasilia.”

2643

“Na huyo Montgomery,
Amiri wao hodari,
Nimemwandalia shari,
Tutazame majaliwa.”

2644

“Shari nimemwandalia,
Yeye na Eisenhower,
Watu wawili hawa,
Hadhi wametuvunjia.”

2645

“Kwa hila nitawahizi,
Wakome na uchokozi,
Watakuwa kama mwezi,
Mimi niwe kama jua.”

2646

“Jua linapotokeza,
Mwezi hauna mwangaza,
Nuru zote humezwa,
Jua likipamba hewa.”

2647

“Kama jua mshumaa,
Bora katika hewa,
Wadachi watazamia,
Ubora wa dunia.”

2648

“Vita sawa na kamari,
Humpa tuzo jasiri,
Haiji bahati nzuri,
Pasipo kujaribiwa.”

2649

Asubuhi kufika,
Yote aliyotamka,
Alitaka kutendeka,
Kama alivyonua.

2650

Alichomoa ghafla,
Kitara katika ala,
Akaonyesha mahala,
Watu pa kushambulia,

2651

Kitara alipofuta,
Na kuwa katika vita,
Upande uliotota,
Nguvu mpya ukajaa.

2652

Nguvu alijaa tele,
Adui wakati ule,
Mfano kama mshale,
Ulio katika hewa.

2653

Rundstedt kama nyoka,
Aliupenya mpaka,
Akapata kuzunguka,
Nyuma ya Wahuria.

2654

Shindo kubwa lilikuwa,
Kwa kitali kuingiwa,
Na watu mashujaa,
Wa adui na huria.

2655

Shindo lililotitima,
Hata siku za nyuma,
Halikupata kuvuma,
Wala kushuhudiwa.

2656

Vita vya siku ile,
Katika vyuo vya kale,
Mfano namna ile,
Bado kusimuliwa.

2657

Hili lilipotendeka,
Montgomery kazuka,
Machache akatamka,
"Bahati imetokea."

2658

"Nilikuwa natafuta,
Adui mjua vita,
Tupate sawa kuteta,
Leo amenijia."

2659

"Kuteta simba kwa simba,
Ndiyo sawa ya kugomba,
Dua niliyoomba,
Sasa nimetimiziwa."

2660

Hakuzidisha maneno,
Shujaa hasemi mno,
Akaamru pigano,
Liwe linaendelea.

2661

Kaamru mpaka,
Ule uliobomoka,
Kujiunga kwa haraka,
Kama ulivyokuwa.

2662

Ulijiunga upesi,
Akazungukwa mtesi,
Asipate nafasi,
Ndogo ya kujiokoa.

2663

Uliwazunguka moshi,
Wadachi ukawaghashi,
Kila njia haipishi,
Jinsi walivyozingwiwa.

2664

Moshi huo tazameni,
Ulizuia uoni,
Cha karibu hukioni,
Ikawa kubwa ghasia.

2665

Katika vita vya bara,
Hii ni ya kwanza mara,
Wahuri kutia fora,
Kwa moshi kuutumia.

2666

Wadachi hawakujua,
Namna ya kujitoa,
Katika ile ghasia,
Mpya iliyotokea.

2667

Zaidi ya jambo hili,
Lilisonga jeshi kali,
Rundstedt akili,
Yote ikamwishia.

2668

Jeshi lake Rundstedt,
Lilizingiwa kati,
Likachaguzwa mauti,
Ama kujitolea.

2669

Jumla watu jeshini,
Walikuwa milioni,
Moja mazingioni,
Hawana pa kutokea.

2670

Rundstedt mtukutu,
Kaokoka bila kitu,
Wala hana hata mtu,
Wote wamepotea.

2671

Hili lilipotokeza,
Hitler aliagiza,
Rundstedt kugeuzwa,
Kwa hali ya kuchukiwa.

2672

Kesserling akaletwa,
Kuja kuzuia vita,
Upande aliopata,
Rundstedt ukiwa.

2673

Baba hamwambii mwana,
Kuwa mimi si mwungwana,
Ila mwana ataona,
Siku ya kunaziiwa.

2674

Na Hitler kadhalika,
Kuungama hakutaka,
Kuwa ameanguka,
Wala hatainukia.

2675

Alizidi kujigamba,
Kuwa aweza kugomba,
Hali amekwisha simba,
Chini kumwinamia.

2676

Furaha na huzuni,
Kwa viumbe duniani,
Vimo katika mizani,
Sawa vining'inia.

2677

Kwa uzazi tunakopa,
Kwa mauti tunalipa,
Kwayo siwezi kuepa,
Hapa kusimulia.

2678

Franklin Roosevelt,
Alipatwa na mauti,
Akatoka katikati,
Ya marafiki huria.

2679

Ulienea msiba,
Kama wingu la dhoruba,
Wakati yalipoziba,
Maisha bora haya.

2680

Uingereza na Amerika,
Ulaya na Afrika,
Kila nchi washirika,
Huzuni iliwajaa.

2681

Kwa kifo cha Roosevelt,
Kapewa kushika kiti,
Truman madhubuti,
Badala yake akawa.

2682

Hili lilitokea,
Amani ilipokuwa,
Sana imekaribia,
Kupamba tena dunia.

2683

Na kabla ya kucheka,
Adui na kuridhika,
Mauti yakamfika,
Mussolini Italia.

2684

Kifo alihukumwiwa,
Na watu wa Italia,
Kwa sababu ya kutia,
Nchi katika hatia.

2685

Huyu mpenda kuua,
Kwa tamaa ya dunia,
Mwisho ameuawa,
Tazama hii hekaya!

2686

Binadamu kipofu,
Katika uharibifu,
Ambao anasanifu,
Mwenyewe atajitia.

2687

Baada ya kuwa haya,
Yako mambo Italia,
Bado hatujayajua,
Lazima kusimulia.

2688

Mambo hayo muhimu,
Lazima yawe humu,
Kwa hivi yanilazimu,
Kurudi Italia.

2689

Baada kutekwa Roma,
Wahuri hawakukoma,
Adui kumwandama,
Kila dakika na saa.

2690

Hawakumpa nafasi,
Ya kukaa kujilisi,
Wala ya kutanafusi,
Kwa fadhaa kutiwa.

2691

Akisema: nisimame,
Hapa kidogo niheme,
Hupambana na waume,
Jasho wakamtoa.

2692

Akisema: nijifunge,
Hapa vita nikinge,
Wanaume wenye singe,
Mara humwelelea.

2693

Akisema: nisite,
Kwa nguvu hapa nitete,
Huona wake wote,
Watu wana fadhaa.

2694

Kila apigapo konde,
Moyo nyuma asende,
Huona wake upande,
Umetiwa ghasia.

2695

Umetiwa ghasia,
Kwa pigo unalopewa,
Kubwa lililopungua,
Chini na katika hewa.

2696

Mambo namna hii,
Yalimwendea adui,
Hata akawa hajui,
Njia ya kuchagua.

2697

Heinrich Wetinghof-Scheel,
Lilipotokea hili,
Aliona afadhali,
Kuwaza la kutumia.

2698

Huyu ni kiongozi,
Na Jemadari wa Nazi,
Aliyekuwa na kazi,
Ya vita Italia.

2699

Aliona kupigana,
Zaidi hakuna maana,
Hasara kila namna,
Zimekwisha mfikia.

2700

Kwa Hitler kumpenda,
Heinrich alitenda,
Kila hila ya kushinda,
Bali hakufanikiwa.

2701

Kwa Hitler kumkiri,
Wadachi walihari,
Kufanya ujasiri,
Wa kushangaza dunia.

2702

Hitler walimtii,
Mfano kama nabii,
Hata walikinai,
Hana mwenziwe wa sawa.

2703

Walimfanya mtume,
Kwa sifa za kiume,
Wepesi kama umeme,
Wa elimu alipewa.

2704

Bali huyu kiongozi,
Alipoona upuuzi,
Sasa umekuwa wazi,
Wajumbe aliandaa.

2705

Kila upande kakunjwa,
Kila dhiki ameonja,
Hakuwa na ujanja,
Ila wajumbe kutoa.

2706

Alituma watu kwenda,
Hata kwa Alexander,
Kusema kuwa apenda,
Amani akiridhiwa.

2707

Vita vimemchokesha,
Hawezi kuviendesha,
Vizuri akijibishwa,
Silaha ataachia.

2708

Hawezi kuendelea,
Kupigana Italia,
Na kama ataridhiwa,
Mara atajitolea.

2709

Iliandikishwa hati,
Isiyo na masharti,
Wadachi wawili kati,
Mikono wakatia.

2710

Walitia mikono,
Yamekoma mapigano,
Tena wameshindwa mno,
Hata wamejitolea.

2711

Hili lilipodhihiri,
Alexander Amiri,
Kaarifu askari,
Hivi wakatangiwa:-

2712

“Mwatangiwa habari,
Jamii ya askari,
Wa bara na bahari,
Pamoja na wanahewa.”

2713

“Mapigano makali,
Muda wa miaka miwili,
Yaliyoanza Sicily,
Leo yameishilia.”

2714

“Vita vya mfulizo,
Hasara mzo kwa mzo,
Jumla ya siku hizo,
Tuzo vimewaletea.”

2715

“Dhiki zimepita nyuma,
Na leo mmesimama,
Mbele ya heshima,
Bora katika dunia.”

2716

“Ametuomba adui,
Kuwa sasa hana rai,
Ya kushinda vita hii,
Ila kujitolea.”

2717

“Ushindi mliopata,
Umekomesha matata,
Tena umekwisha futa,
Fujo Mediterraneana.”

2718

“Kwa kutoa wachokozi,
Wote wa chama cha Nazi,
Mmewapa ukombozi,
Watu wa Italia.”

2719

“Haya ni masikani,
Ya watu milioni,
Zaidi ya arobaini,
Ambayo mmekomboa.”

2720

“Masalia ya jeshi,
Lililokuwa na mashi,
Leo hii halitishi,
Silaha limeachia.”

2721

“Jumla watu jeshini,
Ni moja milioni,
Wenye zana mikononi,
Pengo hazikutiwa.”

2722

“Hazina pengo na kutu,
Na zilishikwa na watu,
Ambao kwa utukutu,
Walitingisha dunia.”

2723

“Mwaweza jifaharisha,
Kwa mliyokamilisha,
Sifaye haitakwisha,
Katika historia.”

2724

“Mfano wa kulingana,
Na sifa yenu hapana,
Kwa ushindi bora sana,
Ambao mmefikia.”

2725

“Nawapa shukurani,
Kwa fahari moyoni,
Kila nililotamani,
Mmetenda Italia.”

2726

“Kila nililotaka,
Kwenu limetendeka,
Daima nitakumbuka,
Fadhili niliyopewa.”

2727

“Namna ushindi huu,
Hivi ulivyo mkuu,
Kuwa Amiri Mkuu,
Wenu nimependezewa.”

2728

“Imenijaa fahari,
Kwa kuona askari,
Chini ya yangu amri,
Mwisho wamefanikiwa.”

2729

Na Churchill Waziri,
Aliipasha habari,
Baraza ya Mashauri,
Tokeo la Italia.

2730

Hotuba yake Waziri,
Kwa Halmashauri,
Hapa nitakariri,
Nizidi kuelewa.

2731

Kama sikuikariri,
Kama ilivyodhihiri,
Kalamu yangu fakiri,
Fasaha haitatoa.

2732

“Kurudi niliahidi,
Barazani ikibidi,
Jambo kubwa zaidi,
Ghafa likitokea.”

2733

“Nitarudi nitake,
Baraza shauri lake,
Na machache itamke,
Kadiri inavyofaa.”

2734

“Jambo hilo muhimu,
Tulilongoja kwa hamu,
Sasa limekwisha timu,
Kwa hivi nimerejea.”

2735

“Adui kajitolea,
Katika Italia,
Na tunayotazamia,
Karibu yatatokea.”

2736

“Jeshi letu maarufu,
Alipewa kusarifu,
Jemadari mwaminifu,
Katika Italia.”

2737

“Chini yake tuliweka,
Jemadari Mwamerika,
Mtu aliyetukuka,
Mark Clark shujaa.”

2738

“Kushuka kwetu Salerno,
Na tisho la mapigano,
La Anzio ni mifano,
Mikubwa kukumbukia.”

2739

“Kutekwa mji wa Roma,
Na kwenda mbele daima,
Uzito wake nasema,
Jeshini ulilemea.”

2740

“Uzito na hasara,
Walipata kila mara,
Askari wetu bora,
Kwa vita kuendelea.”

2741

“Lililozidisha shida,
Jeshi hili kila muda,
Ilikuwa kawaida,
Ya msaada kutoa.”

2742

“Kila mahali dhalili,
Lilitakwa jeshi hili,
Lipeleke tasihili,
Awni kusaidia.”

2743

“Watu wa jeshi hili,
Kwa kupelekwa mahali,
Kwa vita mbalimbali,
Sana lilipungukiwa.”

2744

“Kwa nguvu lilikuwa,
Jeshi limepungukiwa,
Nguvu ilipodhaniwa,
Ya adui maridhawa.”

2745

“Zaidi ya hii hali,
Watu wa jeshi hili,
Walikuwa mbalimbali,
Kwa makabila si sawa.”

2746

“Lilitaka mtu bora,
Imara hana harara,
Anayejua busara,
Ya kuunga watu hawa.”

2747

“Shangwe langu la kushinda,
Kwa Amiri Alexander,
Kila alilotenda,
Sifa nimeamtolea.”

2748

“Na juu ya udhaifu,
Kama nilivyoarifu,
Jeshi halikuhalifu,
Limetimiza murua.”

2749

"Kutengana kwa kabila,
Na tofauti za mila,
Hakukutia ila,
Umoja wa watu hawa."

2750

"Na sasa tuzo yao,
Imekuja watu hao,
Nafurahi tuzo hiyo,
Hivi ilivyotokea."

2751

"Imekuja kwa wakati,
Ushuhudie umati,
Wingi wa madhubuti,
Wa jeshi ulivyokuwa."

2752

"Limeleta na fahari,
Ya kazi ya askari,
Kubwa haina kadiri,
Leo katika dunia."

2753

"Na Alexander Amiri,
Ambaye ilimkiri,
Baraza ya Mashauri,
Sifa amejipatia."

2754

"Sifa amepata hasa,
Bora iliyopasa,
Fahari kubwa kabisa,
Baraza kailitea."

2755

Sasa wajibu nirudi,
Hata Stalingrad,
Nisimulie zaidi,
Mwendo wa Warussia.

2756

Hili kama sikusema,
Wenzetu wajao nyuma,
Watalaumu lawama,
Choyo nimewafanyia.

2757

Stalingrad na Berlin,
Kwa umbali yamkini,
Elfu nyingi njiani,
Maili huhesabiwa.

2758

Safari hii si ndogo,
Na kila mara mapigo,
Ya nguvu na vurugo,
Njiani yalitokea.

2759

Kwa Wadachi ulikuwa,
Mwendo huu si udhia,
Sababu karibu njia,
Yote walielewa.

2760

Walielewa mapito,
Lilipo ziwa na mto,
Penye miba na tototo,
Waliweza kuambaa.

2761

Tena walikwisha fika,
Hata ng'ambo ya mipaka,
Ikabakia kuteka,
Mji wa chuma pua.

2762

Lakini kwa Warussia,
Mashaka ya hii njia,
Mengi yaliwatokea,
Katika kila hatua.

2763

Walikutana na taabu,
Nyingi mno kuhesabu,
Na vita vya ghadhabu,
Mbele yao kila saa.

2764

Hii safari ndefu,
Iliyoenea ufu,
Uongozi wa safu,
Zhukov alipewa.

2765

Katikati ya sufufu,
Ya waongozi wa safu,
Jina hili maarufu,
Limeenea dunia.

2766

Jina limefika mbali,
Na watu wamekubali,
Kuwa ni shujaa kweli,
Kati ya mashujaa.

2767

Jina hili mashuhuri,
Na kati ya maamiri,
Zhukov ni johari,
Bora katika Russia.

2768

Huyu ni mtangulizi,
Aliyeanza kuhizi,
Maamiri wa Nazi,
Na hadhi kuwavunjia.

2769

Alivunja na kiburi,
Cha wengi majemadari,
Ambao walikiri,
Hitler kumtetea.

2770

Adui aliyepata,
Na Zhukov kuteta,
Nishani zake na nyota,
Fedhehani zilitiwa.

2771

Kila aliyetukuka,
Kwake aliaibika,
Hitler akaudhika,
Kwa kuona mambo haya.

2772

Hasa wazo la aibu,
Lilivunja taratibu,
Na kuamsha ghadhabu,
Ya Hitler kuua.

2773

Alitangaza ya kama,
Kila arudiye nyuma,
Kuuawa ni lazima,
Na nishani kuvuliwa.

2774

Katika kila maili,
Wadachi walikabili,
Mapigano makali,
Lakini hawakufaa.

2775

Njia ya kumzuia,
Zhukov hawakujua,
Watu wakaangamia,
Kama matone ya mvua.

2776

Wakigeuka kushoto,
Hupata pigo zito,
Kulia hupata moto,
Na mbele yao ghasia.

2777

Kama wakirudi nyuma,
Kidogo wapate hema,
Hitler bila huruma,
Watu wake aliua.

2778

Katika kila hatua,
Huyu alipotokea,
Adui alijaa,
Hofu na fadhaa.

2779

Katika kila unyayo,
Watu Hitler moyo,
Walikuwa hawanao,
Kwa nguvu kuzidiwa.

2780

Walizidiwa kwa nguvu,
Akili na welekevu,
Na Amiri Zhukov,
Simba wa Russia.

2781

Hata ilipotiwa,
Berlin mazingiwa,
Zhukov alichagua,
Wadachi kuarifiwa.

2782

Wajumbe walitolewa,
Wadachi kwenda wambia,
Mji umezingiwa,
Yawapasa kuchagua.

2783

Wachague wokofu,
Wa mji wao nadhifu,
Au uharibifu,
Watakalo litakuwa.

2784

Wakitaka salama,
Waache silaha hima,
Au mji lazima,
Majivu utakuwa.

2785

Wajumbe waliotumwa,
Hili kwenda kusema,
Hawakurudi nyuma,
Wadachi waliwaua.

2786

Kwa wajumbe kuuawa,
Na wakati kupotea,
Zhukov alichukiwa,
Vita vikaamriwa.

2787

Vita vilinguruma,
Mji karibu kuzama,
Nywele zikasimama,
Kwa hofu na kutishiwa.

2788

Majemadari mia,
Zhukov alitumia,
Berlin kushambulia,
Na zaidi ya hawa.

2789

Watu sitini na tano,
Waliongoza pigano,
Kali lisilo mfano,
Katika kila mtaa.

2790

Katika mabarabara,
Zilienea hasara,
Kwa bomu na makombora,
Moto na moshi kupaa.

2791

Mavunjiko ya nyumba,
Yalivuma kama mwamba,
Kwa fitina wakaomba,
Wadachi kusaidiwa.

2792

Wadachi walifitini,
Russia na Britani,
Zitoke shirikani,
Kwa kusema ya kuwa:-

2793

*Kwa kuteta Berlin,
Hitler ana yakini,
Atetea Britani,
Kurukiwa na Russia.*

2794

*Ushenzi wa Russia,
Kujieneza Ulaya,
Hitler anazuia,
Wajibu kusaidiwa.*

2795

*Ulaya ustaarabu,
Tuliopata kwa taabu,
Watazamiwa karibu,
Kuvunjwa na Russia.*

2796

*Ikishindwa Jermani,
Amerika isidhani,
Kuwa ina amani,
Wala Britania.*

2797

*Kwani haziungani,
Amerika na Britani,
Ufaransa na Jermani,
Kupigana na Russia!*

2798

*Tusipojiunga tena,
Na kusahau ya jana,
Russia shaka hapana,
Itatawala dunia.*

2799

*Urafiki wa furaha,
Umetutia jeraha,
Kujiunga ni mzaha,
Yo yote na Russia.*

2800

*Russia haipendeki,
Haiwezi urafiki,
Sisi imetupa dhiki,
Dunia yashuhudia.*

2801

*Kabla hatujashindwa,
Msaada mkitenda,
Sisi nanyi tutakwenda,
Kupigana na Russia.*

2802

*Msaada tumesihhi
Tunataka mtuwahi,
Mkikawia zihhi,
Yetu itapungua.*

2803

*Tumesema waziwazi,
Kila neno mmaizi,
Mkifanya ni upuuzi,
Wakati utatokea.*

2804

*Utatokea wakati,
Wa kujuta umati,
Onyo hili madhubuti,
Kama hamkutumia.*

2805

*Wakati utafika,
Wa watu kusikitika,
Kwa kuacha kushika,
Onyo tunalotoa.*

2806

*Hiki kilikuwa chambo,
Cha kuchafua mambo,
Wapigane kwa makumbo,
Watu walio bia.*

2807

*Chambo hakikushawishi,
Hata mmoja mtashi,
Kikapita kama moshi,
Hewani na kupotea.*

2808

*Vita muda wa juma,
Moja bila kusimama,
Berlin yote nzima,
Iitekwa na Russia.*

2809

*Kushindwa kwa Berlin,
Amiri Jeshi Stalin,
Alitangaza ilani,
Watu kuarifiwa.*

2810

*"Jeshi chini ya Zhukov,
Pamoja na Koniev,
Limevunja ushupavu,
Adui amelegea."*

2811

*"Mji mkuu Berlin,
Fahari ya Jermani,
Umetiwa mikononi,
Na jeshi la Russia."*

2812

*"Berlin ni tuta,
Milele panapoota,
Uchokozi wa vita,
Na fitina ya dunia."*

2813

*"Fitina ya mji huu,
Hushusha vilivyo juu,
Vikakanyagwa miguu,
Na heshima kuvunjiwa."*

2814

*"Tuta hili la mbolea,
Linalokuza mimea,
Isiyo na manufaa,
Sasa limeharibiwa."*

2815

*"Imeharibiwa mbegu,
Ioteshayo magugu,
Katika moyo na sugu,
Mtu akawa mbaya."*

2816

*"Imekatwa na mizizi,
Isitoe chipukizi,
Tena ya chama cha Nazi,
Kilichoudhi dunia."*

2817

*"Mmea wa tunda chungu,
Vinywani mwa walimwengu,
Kwa msaada wa Mungu,
Shina limeng'olewa."*

2818

*"Fahari ya utukutu,
Iliyowalevya watu,
Iko chini ya viatu,
Vumbini yagaagaa."*

2819

*"Mizinga yaamriwa,
Moscow kushangilia,"
Kwisha kutamka haya,
Shangwe kubwa likawa.*

2820

*Kwa jumla ililia,
Mizinga thelatha mia,
Kushangilia shujaa,
Berlin waliotwaa.*

2821

Na mizinga mingine,
Yatuhusu tunene,
Ishirini na nne,
Juu ya thelatha mia.

2822

Mara mbili darzeni,
Mfulizo tazameni,
Ilinguruma hewani,
Mizinga shangwe kutoa.

2823

Ilinguruma kwa shindo,
Ukenda mbali mshindo,
Hata nchi za kando,
Zikapata kusikia.

2824

Mwisho wa habari hiyo,
Yalivutwa masikio,
Juu ya mafanikio,
Mapya yaliyotokea.

2825

Ilitangazwa habari,
Amiri Montgomery,
Naye wake askari,
Hamburg wameingia.

2826

Huu ni mji wa pili,
Maarufu hata mbali,
Hapa kila shughuli,
Wadachi waliandaa.

2827

Kabla ya kumaliza,
Watu hili kusikiza,
Udachi ilitangazwa,
Yaomba kujitolea.

2828

Udachi ilipeleka,
Maombi Amerika,
Na Uingereza kutaka,
Amani kufanyiwa.

2829

Kwa kutotajwa Russia,
Wakuu wa Britania,
Na wa Amerika pia,
Hili halikuwafaa.

2830

Wakatangaza habari,
Amani watafikiri,
Udachi ikikiri,
Imeshindwa na Russia.

2831

Walitaka na Hitler,
Asimtume Himmler,
Wala mwingine badala,
Amani kumwomba.

2832

Amani itatendeka,
Kama mwenye mamlika,
Atasimama kutaka,
Jambo hili kutendewa.

2833

Akatangaza Himmler,
"Anaugua Hitler,
Kwa dawa na kila hila,
Atibiwa hajapoa."

2834

"Ampatwa na maradhi,
Yatazamiwa faradhi,
Kumtenga na ardhi,
Kabla ya kuchwa jua."

2835

"Natangaza msadiki,
Hitler atafariki,
Na sisi tunayo dhiki,
Begani yatuchubua."

2836

"Vita vimetulegeza,
Twaomba Waingereza,
Wazidi kusikiliza,
Maombi tunayotoa."

2837

"Vita vimetufuja,
Sasa twataka faraja,
Utii wetu wangoja,
Amri kutolewa."

2838

"Na zaidi ya hili,
Lazima niseme kweli,
Hatuwezi kuhimili,
Vita vya robo saa."

2839

"Nguvu ya kupigana,
Sasa hatuna tena,
Kisha tumeshindwa sana,
Tayari kujitolea."

2840

"Imepigwa taaban,
Na kushindwa Jermani,
Na nguvu ya Britani,
Amerika na Russia."

2841

"Sasa hatuna hiari,
Mpendalo tutakiri,
Mara ikija amri,
Yenu itatiiwa."

2842

"Waongozi wa uhuru,
Lo lote wakiamuru,
Sisi hatuna udhuru,
Mwema wa kuwazuia."

2843

"Amani kweli twataka,
Msifikiri dhuhaka,
Tukipewa kwa haraka,
Shukurani tutatoa."

2844

"Jemadari Jodl,
Mjumbe wa jambo hili,
Ametumwa kukabili,
Kwenu ujumbe kutoa."

2845

"Huyu akiwasilisha,
Ujumbe tutaanzisha,
Majeshi kuamrisha,
Silaha kuachia."

2846

Adui Jumanne,
Mei tarehe nane,
Hakutenda jingine,
Ila kujitolea.

2847

Amiri Jeshi Keitel,
Friedeburg Admeli,
Na Stumpf walikubali,
Hati mikono kutia.

2848

Wadachi watatu hawa,
Ndiyo waliotia,
Sahihi kushuhudia,
Kuwa wamejitolea.

2849

Na upande wa Wahuri,
Arthur Tedder mashuhuri,
Na Zhukov Amiri,
Nao walishuhudia.

2850

Hati hii ya amani,
Ya kushindwa Jermani,
Iilitiwa Berlin,
Mikono na watu hawa.

2851

Katikati ya usiku,
Wa huku haendi huku,
Ndiyo wakati wa siku,
Yalipotendeka haya.

2852

Mwaka huu ulikuwa,
Elfu na tisa mia,
Arobaini tia,
Pamoja na tano pia.

2853

Haya yalipodhihiri,
Alisimama Waziri,
Kutangaza habari,
Toka Britania.

2854

Kwa kuwa sina elimu,
Ya kueleza magumu,
Hotuba yake tamu,
Lazima kukaririwa.

2855

Nitakariri machache,
Rahisi nisiwafiche,
Na magumu niache,
Wengine watatwambia.

2856

"Natangaza Jermani,
Majeshi yake barani,
Baharini na hewani,
Yamevunjwa vibaya."

2857

"Vita hapa Ulaya,
Sasa vimejishia,
Amani imerejea,
Tena kupamba dunia."

2858

"Baada ya matengezo,
Miaka mingi mfulizo,
Udachi kwa mzozo,
Poland ilirukia."

2859

"Mwanzoni Septemba,
Tulitangaza ya kwamba,
Imepasa kugomba,
Udachi na Britania."

2860

"Elfu na mia tisa,
Thelathini na tisa,
Ndiyo mwaka kisa,
Hiki kilipotokea."

2861

"Baada ya Ufaransa,
Nchi shujaa hasa,
Iliposhindwa kabisa,
Peke tulibakia."

2862

"Peke yetu tuliteta,
Hata mwaka ukapita,
Bahati ikaleta,
Msaada wa Russia."

2863

"Halafu Amerika,
Ilijiunga haraka,
Ikawa ni mshirika,
Upande wa Britania."

2864

"Tulilala wakiwa,
Kuamka tumekuwa,
Tuna nguvu maridhawa,
Himaya imeenea."

2865

"Tulilala maskini,
Duni hatuna thamani,
Kuamka awni,
Bora imetujia."

2866

"Leo adui tajiri,
Ameamka fakiri,
Utukufu na fahari,
Vyote vimempotea."

2867

"Shukurani zetu zenda,
Kwa wote waliotenda,
Bidii za kuunda,
Umoja wa huria."

2868

"Mwisho dunia yote,
Ilijiunga itete,
Hata adui ajute,
Na sasa kajitolea."

2869

“Mawazo yetu halisi,
Leo yatuhusu sisi,
Kesho ndiyo nafasi,
Ya kusifu Warussia.”

2870

“Tutasifu ushujaa,
Wa majeshi ya Russia,
Na yalivyosaidia,
Ushindi wa jamia.”

2871

“Basi tushangilie,
Na kidogo tupumue,
Lakini tukumbukie,
Dhiki zinatungojea.”

2872

“Tukumbuke ya kuwa,
Japani yatungojea,
Na hivi yaandaliwa,
Siku ya kuendewa.”

2873

“Wajapani wenye hila.
Na choyo katika mila,
Bado kutawaliwa,
Wala kujitolea.”

2874

“Nguvu zetu na uwezo,
Tuzitie mkazo,
Hata tuone timizo,
La kazi limetimia”

2875

“Uingereza endelea,
Uhuru uishi pia,
Mungu pokea dua,
Mfalme kumwoko.”

2876

Baadaye Churchill,
Katika Whitehall,
Watu aliwakabili,
Hotuba kuwatolea.

2877

“Mungu wape baraka,
Wote waliofika,
Leo kukutanika,
Ushindi kushangilia.”

2878

“Ushindi uliokuja,
Si wa mtu mmoja,
Wenu wote pamoja,
Katika nchi huria.”

2879

“Katika mapokeo,
Yetu tukumbukayo,
Siku mfano wa leo,
Haijapata tokea.”

2880

“Katika historia,
Yote ya Britania,
Siku bado kutokea,
Na ya leo kuwa sawa.”

2881

“Siku hii haina,
Mfano wa kufanana,
Na sisi bado kuona,
Kuwa katika dunia.”

2882

“Kila mtu kafanyiza,
Bidii aliyoweza,
Na leo mwangaza,
Wa uhuru unang'aa.”

2883

“Kila mume na mke,
Katenda sehemu yake,
Hata leo makeke,
Yemekwisha Ulaya.”

2884

“Katika miaka mitano,
Ya hatari kubwa mno,
Na makali mapigano,
Sisi hatukulegea.”

2885

“Taifa la Uingereza,
Adui hakuweza,
Kidogo kulilegeza,
Wala hofu kulitia.”

2886

Churchill kutua,
Shangwe lililotokea,
Bado watu kusikia,
Whitehall kuwa.

2887

Hapa nataka wasome,
Wake na wanaume,
Mtukufu Mfalme,
Hotuba aliyotoa.

2888

Mkuu wa maamiri,
Katika uaskari,
Wa bara na bahari,
Pamoja na wanahewa.

2889

Mkuu wa marubani,
Katika eroplani,
Hata sabmarini,
Mashuhuri na shujaa.

2890

Mkuu wa waongozi,
Kila namna ya kazi,
Vyeo nimeweka wazi,
Watu wapate elewa.

2891

Mkuu wa maidara,
Yenye kazi za busara,
Hotuba yake bora,
Hapa nimewachujia.

2892

Hotuba nimeichuja,
Neno moja kwa moja,
Yote yenye haja,
Hapa mimewapangia.

2893
"Twamshukuru Mwenyezi,
Mungu mwenye mapenzi,
Leo kwa wokozi,
Bora uliotujia."

2894
"Nasema usemi huu,
Katika mji mkuu,
Wa Ufalme huu,
Vitani uliotiwa."

2895
"Vitani ulipotiwa,
Alama ya kutishiwa,
Haikupata kuwa,
Kwa dakika au saa."

2896
"Nasema toka London,
Nawaomba jiungeni,
Tushukuru Rahmani,
Aliyeumba dunia."

2897
"Udachi nchi hasimu,
Iliyovuta kaumu,
Vitani kwa udhalimu,
Imeshindwa na kuvia."

2898
"Mashariki ya Mbali,
Bado tuna vita kali,
Na adui katili,
Ambaye kayakinia."

2899
"Tutaingia vitani,
Tupigane na Japani,
Kwa nguvu na makini,
Yote tunayofikia."

2900
"Bali tisho la awali,
Sasa limekwenda mbali,
Kwa hivi yastahili,
Shukurani kutoa."

2901
"Tukumbuke idadi,
Ya watu wasiorudi,
Uthabiti na juhudi,
Sadaka waliyotoa."

2902
"Tukumbuke na unyofu,
Wao na uaminifu,
Mbele ya uharibifu,
Wa adui wa dunia."

2903
"Tukumbuke watu wote,
Katika kazi zote,
Na wanawake wote,
Maisha waliotoa."

2904
"Dhiki zetu na mashaka,
Mwisho wake tumefika,
Hawa hawakuokoka,
Kurudi kushangilia."

2905
"Hawa hawakurejea,
Leo pamoja tukawa,
Kufurahia saa,
Ya amani Ulaya."

2906
"Tutoe maamkizi,
Kwa Mungu Mwenyezi,
Kwa fahari na mapenzi,
Kwa ushindi kutujia."

2907
"Waliofanya kazi,
Kusifu wote siwezi,
Kwa kupanga waziwazi,
Au kwa kupambanua."

2908
"Yote waliyotenda,
Yamesaidia kwenda,
Juu hata tumeshinda,
Adui yetu mbaya."

2909
"Askari na raia,
Wake na waume pia,
Uhuru wametetea,
Na dhiki kuvumilia."

2910
"Dhiki zilizotokea,
Na zilivyovumiliwa,
Hapana anayejua,
Kama ninavyoelewa."

2911
"Na kwa kuwa Mfalme,
Wenu lazima niseme,
Nashukuru wanaume,
Wote na wake pia."

2912
"Nashukuru kwa furaha,
Walioshika silaha,
Bila hofu ya jeraha,
Bara na katika hewa."

2913
"Nashukuru kwa fahari,
Askari wa bahari,
Na hali walivyokiri,
Raia kuvumilia."

2914
"Vita tulivyoteta,
Karibu miaka sita,
Kurabukumbu huleta,
Ya hali tuliyokuwa."

2915
"Tulivumilia bia,
Mateso na udhia,
Fikira ya mambo haya,
Hapana la kuondoa."

2916
"Kwa hakika kila kitu,
Katika milki yetu,
Na uhuru wa watu,
Hatarini vilikuwa."

2917
"Hadhi yetu na maisha,
Hivi vilihatarishwa,
Bali tumevidumisha,
Kwa tulivyojitetea."

2918
"Fahari kukumbukia,
Tulipoteta ya kuwa,
Tumeokoa dunia,
Uhuru na sharia."

2919
"Mataifa ya Ulaya,
Utumwa yaliyotiwa,
Kwetu yalitazamia,
Kuwa tutayakomboa."

2920
"Na matumaini yao,
Kwetu yalikuwa ndiyo,
Yaliyo katika moyo,
Na imani kututia."

2921
"Tulijua ya kuwa,
Heri isipotujia,
Udhalimu utakuwa,
Bwana katika dunia."

2922
"Bali hatukulegea,
Wala hatukumwachia,
Adui kupata njia,
Kama ilivyodhaniwa."

2923
"Ahadi tuliipeana,
Pamoja tukaungana,
Hata pakawa hapana,
Njia ya kutufumua."

2924
"Tena mara kwa mara,
Marafiki wetu bora,
Tuliwaonya imara,
Ya umoja na nia."

2925
"Tazama umoja huo,
Umetuchukua mbio,
Hata hivi leo,
Ushindi tumefikia."

2926
"Tumepita hatari,
Nyingi hazina kadiri,
Zilizoonya dhahiri,
Mambo ya kutishia."

2927
"Tumeyavuka mambo,
Ya matata kama fumbo,
Leo tumefika ng'ambo,
Heri inatuchekea."

2928
"Basi tuyakinishe,
Umoja tuendeshe,
Hata mashaka yeshe,
Mbele yanayongojea."

2929
"Tena kazi ya kughasi,
Iliyo ngumu halisi,
Bado yatungoja sisi,
Kujenga Britania."

2930
"Itabidi kutengeza,
Nchi ziwe kama kwanza,
Hapa Uingereza,
Na nyingine za dunia."

2931
"Adui alipovunja,
Jengo jipya lilingoja,
Ili wapate faraja,
Nyumba waliovunjiwa."

2932
"Na hili limetujia,
Baada wote kutoa,
Bora tuliyojaliwa,
Miaka mitano ya baa."

2933
"Muda huu na zaidi,
Tulifanya jitihadi,
Kuzuia uhasidi,
Usimeze dunia."

2934
"Sana tuliuzuia,
Shimoni kutotutia,
Ambalo lilikuwa,
Kinywa wazi langojea."

2935
"Moyo na ubongo,
Mishipa na maungo,
Vilipangwa mpango,
Nazi kuwaelelea."

2936
"Heri imetujia,
Tutashika tena njia,
Tumfuate mdawa,
Ambaye amebakia."

2937
"Mimi na Malkia,
Hatari tunaelewa,
Na mateso mabaya,
Waliyopata raia."

2938
"Wote twaona fahari,
Kila tunapofikiri,
Tulishariki hatari,
Sisi na nyinyi bia."

2939
"Tena tunaelewa,
Kuwa tutakuwa bia,
Kumwandama mdawa,
Kwa ushujaa na nia."

2940
"Tutamwonya mdawa,
Nguvu zake si sawa,
Na nguvu zetu za bia,
Mizanini zikitiwa."

2941

"Hili akibaini,
Atajuta kutamani,
Kuingia vitani,
Kuteta na huria."

2942

"Tuna faraja moyoni,
Kuwa miaka ya huzuni,
Na hatari duniani,
Nyuma imekwisha kuwa."

2943

"Miaka ya dhiki nzito,
Waliyoona watoto,
Imekwisha fanya pito,
Wala haitarejea."

2944

"Bure vita kushika,
Na damu kumwagika,
Ushindi tuliota,
Amani usipozaa."

2945

"Kama amani hapana,
Baada ya kupigana,
Ushindi hauna maana,
Kwa walioufikia."

2946

"Damu ya wapenzi wetu,
Haitafidia kitu,
Bila kuungana watu,
Kwa haki na sharia."

2947

"Sharti watu waungane,
Haki washarikiane,
Bila uovu mwingine,
Wa kuchafua dunia."

2948

"Katika shangwe la heri,
La huzuni na fahari,
Msingi tufikiri,
Wa amani ya dunia."

2949

"Tusitende neno duni,
Litakaloshusha chini,
Ubora wa wapigani,
Wetu waliopotea."

2950

"Tutengeneze dunia,
Iwapendeze wakiwa,
Wa waliojitoa,
Sadaka kututetea."

2951

"Tuifanye iwe njema,
Iwaridhi mayatima,
Walioachwa nyuma,
Na watoto wetu sawa."

2952

"Kazi hii ya heshima,
Mbele iliyosimama,
Yataka itendwe hima,
Kama tukijaliwa."

2953

"Wakati wa majonzi,
Tulimwamini Mwenyezi,
Kwa ngao yake Azizi,
Mwisho tumefanikiwa."

2954

"Tushukuru Mungu mwema,
Kwa uwezo na huruma,
Katutenga na nakama,
Na kumshinda mdawa."

2955

"Mkononi mwa Mwenyezi,
Twaweka yetu kazi,
Inshallah kwa maongozi,
Yake tutafanikiwa."

2956

Mfalme Mtukufu,
Halafu alimwarifu,
Mkuu maarufu,
Wa Amerika sikia.

2957

"Mkuu wa heshima,
Tangu Ulaya kukoma,
Vita nimefanya hima,
Shangwe kukuletea."

2958

"Shangwe nakuletea,
Juu ya wetu mdawa,
Ambaye tumejaliwa,
Kumshinda Ulaya."

2959

"Kama tulivyoandaa,
Majeshi yetu ya bia,
Ya Uingereza na Russia,
Na Amerika pia."

2960

"Haya yaliendelea,
Toka machweo ya jua,
Na kusini kupitia,
Chini ya Eisenhower."

2961

"Na wa pili Amiri,
Mkuu mwenye amri,
Kuongoza askari,
Alexander akawa."

2962

"Kazi yaliyoagizwa,
Majeshi yametimiza,
Matisho yamefukuzwa,
Na kukomboa Ulaya."

2963

"Matisho ya Udachi,
Ya kuzitawala nchi,
Rohoni hayafikichi,
Yote yameondolewa."

2964

"Miaka iliyopita,
Ya hatari na vita,
Nchi mbili zimepata,
Nguvu na ujamaa."

2965
"Udugu imefufua,
Mwingi wa kuajabiwa,
Amerika imekuwa,
Pamoja na Britania."

2966
"Sasa nchi hizi mbili,
Zimeungana kwa kweli,
Kisha zitamkabili,
Japani kwa ushujaa."

2967
"Na mimi natazamia,
Umoja na ujamaa,
Wetu utaendelea,
Hata ashindwe mdawa."

2968
"Na ashindwapo Japani,
Ninayo matumaini,
Urafiki wa thamani,
Wetu hautapotea."

2969
"Utazidi kudumu,
Uwafae wanadamu,
Ambao yawalazimu,
Kuishi bia dunia."

2970
"Tena natazamia,
Siku inakaribia,
Ya kushindwa mdawa,
Sasa aliyebakia."

2971
"Zaonyesha dalili,
Ushindi hauko mbali,
Wala hapana zohali,
Ushindi utatokea."

2972
"Na nguvu za Utawala,
Wetu kila mahala,
Zitakusanywa jumla,
Japani kumwendea."

2973
Kwisha haya kunena,
Alitia nguvu tena,
Uingereza na China,
Jinsi zilivyo bia.

2974
Jemadari Kai-Shek,
Kaambiwa urafiki,
Kuwa hauvunjiki,
Kati ya watu huria.

2975
Na juu ya Ufaransa,
Alisema kuwa sasa,
Tumeungana kabisa,
Kuliko tulivyokuwa.

2976
Aliarifwiwa hili,
Jemadari de Gaulle,
Mkuu wa Serikali,
Ya Ufaransa kujua.

2977
Tena ilimlazimu,
Mfalme mahashumu,
Kupeleka salamu,
Kushangilia Russia.

2978
Wilhelmina Malkia,
Wa Netherlands pia,
Naye alisalimiwa,
Shangwe akapelekewa.

2979
Wakili wa Ufalme,
Belgiji wa kiume,
Salamu za Mfalme,
Nyingi zilimfikia.

2980
Na Luxemburg Shekha,
Mwenye ulua na jaha,
Salamu za furaha,
Alipelekewa pia.

2981
Kwa Mkuu wa Poland,
Salamu za ushindi,
Zilipelekwa kundi,
Kutoka Britania.

2982
Na Mfalme Haakon,
Norway mwenye idhini,
Lilitoka Britani,
Shangwe kumshangilia.

2983
Ugiriki na Yugoslavia,
Denmark an Czechoslovakia,
Huko wakuu pia,
Shangwe liliwafikia.

2984
Na zaidi ya korja,
Salamu kwa Maharaja,
Wa Nepal alitajwa,
Mtukufu wa India.

2985
Kwa Mkuu Brazil,
Salamu ziliwasili,
Na wengine mbalimbali,
Pia walikumbukiwa.

2986
Truman Amerika,
Na yeye alitamka,
"Siku ya kukumbuka,
Kubwa imetokea."

2987
"Hasa mimi natamani,
Roosevelt Franklin,
Angekuwa duniani,
Hili kulishuhudia."

2988
"Ningefurahi upeo,
Angeishi hata leo,
Akaona matokeo,
Ya adui Ulaya."

2989
“Mapigo yetu yakini,
Yatamwendea Japani,
Hata aweke chini,
Silaha na kutubia.”

2990
“Vita tumevizatiti,
Japani kitu hapati,
Ila kupiga magoti,
Chini na kujitolea.”

2991
Na Stalin Russia,
Hotuba alitoka,
Ndogo kusema haya,
Chini yaliyotiwa.

2992
“Wakati wetu wa vita,
Sasa umekwisha pita,
Na mwingine tumepata,
Kustawisha dunia.”

2993
“Hapana tofauti,
Wajua wote umati,
Imepigishwa magoti,
Jermani na Russia.”

2994
“Kwa nguvu ya Britania,
Na ya Amerika bia,
Jermani imetambua,
Kushindwa kwake vibaya.”

2995
“Czechoslovakia kikosi,
Kidogo kina mkosi,
Bali sina wasiwasi,
Kitafundishwa tabia.”

2996
“Hawawezi kukimbia,
Ushindi kuwafikia,
Kuepa hawana njia,
Wadachi Czechoslovakia.”

2997
Kumalizika haya,
Moscow lilitokea,
Shangwe katika hewa,
Kubwa la kuajabiwa.

2998
Mizinga makusudi,
Elfu mbili idadi,
Ya ngurumo kama radi,
Kwa nguvu ililia.

2999
Hasa mara thelathini,
Ilinguruma hewani,
Kushangilia amani,
Na kushindwa mdawa.

3000
Tangu kuumbwa dunia,
shangwe bado kutokea,
La mizinga kulia,
Kama hili la Russia.

Utenzi huu unasimulia habari za Vita Vikuu vya Pili—1939 mpaka 1945. Kwa utungo fasaha, Shaaban Robert, yule mshairi mashuhuri wa Afrika ya Mashariki, anaeleza kwa nini vita hivi vilipiganwa na vililendeshwa namna gani na pande zote mbili. Karibu kila kitu muhimu cha vita hivi kinaelezwa katika utenzi huu. Hotuba muhimu zilizotolewa na viongozi mbalimbali, na hata simu walizopelekeana, zote zimo. Mashairi yenyewe yametungwa kwa lugha nyepesi.

bei shs. 12.00 (Afrika ya Mashariki)



OXFORD UNIVERSITY PRESS

8
C
C00 10701